ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba - Tarehe 30 Oktoba, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe.Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na shughuli zetu na leo tunao wageni, wageni waliopo leo katika ukumbi wetu pale juu ni vijana wetu, wenetu, watoto wetu ambao jumla yao ni 28 na vijana hawa ni vijana wa michezo ambao wamekuwa ni mabingwa wa soka la wanawake Zanzibar yaani *new generation,* ambao wametwaa ubingwa huu baada ya kuwafunga timu ya *women fighter* ya Kikwajuni mabao 4-1. Mchezo huo ambao wamenyakua mabao 4-1 ulifanyika katika uwanja wa Aman. Wageni hao 28 wanaongozwa na viongozi wao ambao ni:-

1) Leila Said Abdalla - Katibu wa Timu
2) Ali Abdalla Rashid - Kocha Mkuu
3) Masoud Farahan - Kocha Msaidizi
4) Ali Abdul Ali - Msemaji Mkuu wa timu

Wageni hao ni wageni wa Mhe. Ali Salum Haji wa Jimbo la Kwahani. Kwa pamoja sasa nawaomba wageni wetu wote wasimame ili kuwasalimia waheshimiwa Wajumbe.

Vijana karibuni sana na kombe lile pale. Ahsanteni sana na karibuni sana katika shughuli zetu.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hati mezani yenye mnasaba na ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hati mezani juu ya ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2012/2013.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani ya muhtasari wa ripoti ya hotuba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2012/2013.

Naomba kuwasilisha.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Mwaka 2012/13

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha siku hii ya leo kukutana hapa kwenye kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi, kwa lengo la kupokea ripoti ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Fedha kwa mwaka 2012/2013 tukiwa wazima na afya njema.

Mhe. Spika, napenda pia kutoa shukurani zetu za dhati kwako wewe binafsi kwa kuiwezesha Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inayoongozwa na Mhe. Salmini Awadh, mwakilishi wa wananchi kupitia Jimbo la Magomeni. Pamoja na kufanya kazi zake vizuri kamati pia imeweza kutoa ushauri na maelekezo kwa Wizara ya Fedha na hatimae kukuza utendaji wa Wizara yangu kwa ujumla.

Mhe. Spika, ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2012/2013 iliangalia utekelezaji wa malengo yanayoambatana na usimamizi wa fedha za umma ulio chini ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Pia iliangalia utekelezaji mzima wa bajeti kwa Wizara ya Fedha, Pemba na Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ ilioko Dar es Salaam pamoja na Utekelezaji wa bajeti kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha ambazo ni Mamlaka ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar *ZIPA*, Bodi ya Mapato Zanzibar *ZRB*, Chuo cha Uongozi wa Fedha, Shirika la Bima Zanzibar, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar na Mfuko wa Barabara Zanzibar.

Utekelezaji wa maagzio ya Kamati. Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo wakati ikiangalia utekelezaji wa programu ya usimamizi wa fedha za umma ilitoa maagizo manne yafutayo:-

1) Mpango wa kubadilisha wahasibu waharakishwe kwa lengo la kupatikana ufanisi wa kazi katika kada ya uhasibu.

2) Hesabu za Mabaraza ya Mji na Manispaa zipelekwe kwa Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi.

3) Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa wanaajiri wahasibu wenye sifa.

4) Utaratibu wa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya serikali uimarishwe na uende sambamba na kuziba mianya ya upotevu wa mapato.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kulieleza Baraza lako Tukufu kuwa utekelezaji wa maagizo hayo umefanywa kama ifuatavyo:-

1) Uhamisho wa Wahasibu wa Serikali katika Wizara zetu umekamilika. Wahasibu Wakuu waliokaa katika kituo kwa muda mrefu wamehamishiwa vituo vyengine kwa lengo la kuendelea na kazi zao.

2) Ofisi yangu tayari imeshawasiliana na uongozi wa mabaraza ya miji na manispaa na tumeshaweka utaratibu wa kuwasilisha na kwa wakati, hesabu za mabaraza ya miji na manispaa kwa mwaka 2013/2014 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha ripoti ya hesabu za mabaraza hayo kwa mwaka 2012/2013 tayari zimeshawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

3) Serikali imeajiri na itaendelea kuajiri wahasibu wenye sifa ambapo sifa za kuwa Mhasibu ni elimu isiyopungua Shahada ya Kwanza katika masuala ya fedha. Aidha watunza hesabu pia ni lazima wawe na elimu isiopungua Diploma katika masuala ya fedha.

4) Wizara imechukua na itaendelea kuchukua hatua mbali mbali katika kuongeza mapato na pia kuziba mianya ya upotevu wa mapato.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja zifuatazo:-

1) Kufanya marekebisho ya sheria ya *VAT* Namba 4 ya mwaka 1988 kwa lengo la kurekebisha viwango vya kutoza kodi.

2) Kupuguza misamaha kwa baadhi ya Taasisi Binafsi.

3) Kufanya marekebisho ya sheria ya Kodi Namba 1 ya mwaka 1995 kwenye kianzio cha kodi za hoteli.

4) Kufanya marekebisho ya sheria ya Kodi ya Mafuta Namba 7 ya mwaka 2001 kwa kuzikusanya kodi zote wakati wa uingizaji wa mafuta nchini, pamoja na kukusanya fedha za leseni kwa njia ya kupitia kwenye ununuzi wa mafuta.

5) Kufanya marekebisho ya sheria ya ushuru wa stempu Namba 6 ya mwaka 1996 kwa kubadilisha usajili, walipa kodi ambao wanaonekana wana sifa za kusajiliwa chini ya sheria ya *VAT*.

6) Kufanya marekebisho ya ada ya bandari, sheria Namba 2 ya mwaka 1999 kwa kupandisha kiwango cha ada ya uwanja kwa abiria wanaokwenda nje ya nchi kutoka dola 35 hadi dola 40.

7) Kufanya marekebisho ya sheria usajili ya usafiri wa barabarani Namba 7 ya mwaka 2003 na kanuni zake kwa kuongeza kiwango cha usajii wa leseni za udereva kutoka shilingi 15,000/- hadi shilingi 20,000/- kwa leseni ya mwaka.

8) Kwa kushirikiana na *TRA* Semina 11 zimefanyika Unguja na Pemba pamoja na kuendesha vipindi vya matangazo kwenye televisheni na radio kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa ulipaji kodi.

9) Kuimarisha uwezo wa watendaji kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali, kununua vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi pamoja na kutoa motisha, kazi ambazo zinaendelea kila mwaka.

Mhe. Spika, ripoti ya Kamati kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya Mamlaka ya Ukuzaji na Uendelezaji Vitega Uchumi kwa mwaka 2012/2013 ilitoa agizo moja na ushauri. Kwa upande wa agizo, Kamati iliitaka serikali kuangalia uwezekano wa kutunga sheria itakayosaidia kuondoa tatizo la wawekezaji wanaouza miradi yao baada ya muda wa msamaha wa kodi kumalizika.

Suala hili tumelipokea na tumeona umuhimu wake. Hata hivyo kwa hivi sasa sheria ya uwekezaji inafanyiwa marekebisho makubwa, marekebisho hayo yatalenga pia kuwabana wawekezaji wanaouza miradi yao baada ya muda wa msamaha unapomalizika kwa kuandaa utaratibu maalum.

Mhe. Spika, katika masuala mengine ya uwekezaji kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

1) Kamati imependekeza kukamilishwa miundombinu katika maeneo yanayokusudiwa kuwavutia wawekezaji kwa lengo la kuwa ni kichocheo cha Uwekezaji.

2) Kuandaliwe mpango madhubuti wa kuondosha uhalifu katika maeneo ya uwekezaji hasa katika mahoteli.

3) Juhudi za haraka zifanywe ili fedha za kuandaa master plan ya eneo la Fumba na Micheweni ziweze kupatikana.

4) Utaratibu mzuri wa Kuratibu sekta za uwekezaji kwa kuhusisha taasisi mbali mbali kama vile ardhi, mazingira, afya, kilimo na kadhalika uandaliwe kabla ya muekezaji hajapewa kibali cha kuekeza katika eneo husika.

Mhe. Spika, baada ya kupata ushauri huo kutoka kwa kamati serikali imechukua hatua zifuatazo:-

1) Matayarisho ya master plan katika eneo la Fumba yameanza na yanaendelea vizuri. Aidha, kazi ya kujenga miundombinu muhimu itafanyika baada ya kazi hiyo kukamilika.

2) Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na kwa kushiriikiana na wamiliki wa hoteli imeanza maandalizi ya ulinzi katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kuondosha uhalifu katika maeneo ya utalii.

3) Utaratibu uliopo wa uwekezaji unazishirikisha taasisi mbali mbali kupitia Kamati inayoangalia na kupitisha miradi ya uekezaji *ZIPA*. Aidha, serikali itazidi kuzingatia masuala yote haya kabla ya kibali kutolewa.

Mhe. Spika, kamati pia ilifanya ziara ya kuitembelea miradi mitatu ya wawekezaji katika sekta ya hoteli ambayo ni *Azanzi limited Matemwe, The Spice Island Hotel and Resort* Paje na Belrosa Michamvi na kutoa agizo la kuitaka Serikali kuifanyia marekebisho sheria ya ardhi namba 2 ya mwaka 1992, ili waziri anayeshulikia masuala ya fedha awe na uwezo wa kusimamia misamaha ya kodi ya ardhi.

Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Wizara ya Fedha imelizingatia suala hili na kuona kuwa kuna haja ya kuifanyia marekebisho sheria ya rdhi. Aidha, Kamati pia ilitoa ushauri ufuatao:-

a) Serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya suala zima la uekezaji kwa lengo la kuleta maelewano baina ya wananchi na wawekezaji. Hali hii itasaidia sana katika kuondosha migogoro inayojitokeza mara kwa mara baina ya wananchi na wawekezaji.

b) Kuwepo kwa utaratibu unaofahamika wa malipo ya fidia kwa wananchi ambao wanayatumia maeneo ya uekezaji kwa kilimo na shughuli nyengine kimaisha.

c) Utafiti wa Kina ufanyike kabla ya muekezaji yoyote kupewa eneo ili kuepusha migogoro kati ya wananchi na wawekezaji.

d) Kabla ya miradi kuanza ujenzi kufanyike utafiti wa mazingira ili kuwezesha miradi hiyo kutekelezwa kwa wakati sambamba na kudhibiti mazingira.

Mhe. Spika, ushauri huo wote umepokelewa na serikali kupitia mamlaka ya ukuzaji na uendelezaji vitega uchumi Zanzibar *ZIPA*. Kwa mtazamo huo serikali kupitia *ZIPA* itaendelea kutoa taaluma kwa wananchi juu ya uwekezaji na kuhakikisha kuwa utaratibu wa kulipa fidia wananchi, inakuwa wa uwazi na wenye kueleweka pamoja na kuhahakikisha kuwa migogoro kati ya wawekezaji na wananchi inaondoka.

Aidha, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa tayari utafiti umeanza kwa lengo la kufahamu kiini cha migogoro na hatimae kuondosha kabisa migogoro ya wawekezaji na wananchi. Pia suala la mazingira ni muhimu sana hasa tukizingatia kuwa Zanzibar ni Kisiwa kwa maana hiyo miradi itaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia mazingira yetu kwa ukamilifu.

Mhe. Spika, kamati baada ya kuangalia utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka 2012/2013 kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar *ZSFF*, kamati imeitaka serikali kuwachukulia hatua waajiri ambao hawapeleki michango ya wafanyakazi wao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wakati.

Aidha, Kamati pia iliishauri serikali yafuatayo:-

Mpango wa kuwawezesha wanachama kutumia michango yao kama dhamana ya kupata mikopo benki uharakishwe ili mfanyakazi aweze kutumia sehemu ya mchango wake kabla ya kustaafu. Mhe. Spika, serikali inawachukulia na itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria waajiri wote ambao hawapeleki michango ya wafanyakazi wao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wakati. Kuwachukulia hatua hizo za kisheria ni pamoja na

kuwapeleka mahkamani, baadhi ya waajiri kuomba usuluhisho nje ya mahakama na kusawazisha madeni yao kwa wakati.

Aidha, kwa upande wa mwanachama kutumia michango yake kama dhamana ya kupata mkopo. Wizara ya Fedha imo katika hatua za mwisho za kukamilisha marekebisho ya sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Kanuni zake ili kuwezesha kuhakikisha kuwa mfuko unakuwa endelevu na kuwanufaisha wananchama wake pamoja na kumuwezesha mwanachama kutumia mchango wake kama dhamana kwa lengo la kupata mkopo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyomo katika ripoti, sasa naomba uniruhusu nieleze maagizo ya ujumla ya kamati kama ifuatavyo:-

a) Udhibiti wa mapato ya viza uwanja wa ndege. Kamati iliagiza hatua za haraka zichukuliwe ili kudhibiti upotevu wa mapato hayo kwa kuweka mfumo wa malipo ambao hautahusisha ulipaji wa fedha mkononi.

b) Makusanyo ya fedha kwenye hoteli. Kamati iliagiza Wizara kuzipitia hoteli zote na kuhakikisha kodi inayolipwa ndio iliopaswa kulipwa.

c) Magendo ya mafuta. Serikali ipange mkakati kama ule wa kudhibiti magendo ya karafuu kwa kuunda kikosi kazi na kulifanyia kazi tatizo hili ambalo linaonekana kuwa sugu na kuikosesha mapato serikali.

Mhe. Spika, maagizo hayo yamechukuliwa hatua na Wizara ya Fedha kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeiandikia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar juu ya suala hili la kuiruhusu benki ya *CRDB* kuweka mashine za kukusanya mapato yatokanayo na viza yaani *POS* katika uwanja wa ndege wa kimataifa, Abeid Amaan Karume. Hata hivyo, uongozi wa mamlaka ya viwanja vya ndege bado haujatoa ruhusa ya kuanza kwa uwekaji wa mashine hizo, uwekaji wa mashine hizo kwa kiwango kikubwa ungepunguza upotevu wa mapato yanayotokana na viza.

b) Wizara ya Fedha kupitia Bodi ya Mapato inatekeleza agizo la kuzipitia hoteli ili kuhakikisha kuwa kodi inayolipwa ni halali. Mara kwa mara hoteli hupitiwa na inapobainika kuwa wamiliki wamefanya udanganyifu huchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

c) Bodi ya Mapato Zanzibar kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi inaendelea kudhibiti magendo ya mafuta. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kama hizi zifuatazo:-

1) Kufanya mawasiliano na mamlaka ya mapato Kenya ili kupata taarifa za viwango vya mafuta yanayochukuliwa kutoka Mombasa na kuletwa Zanzibar.

2) Kushirikiana na KMKM kufanya doria ya mara kwa mara katika sehemu mbali mbali za bahari.

3) Kushirikiana na serikali za Wilaya, Mikoa na wananchi ili kupata taarifa za watu wanaojihusisha na magendo ya mafuta. Serikali imeweka zawadi kwa yoyote atakayetoa taarifa za kufanikisha kukamata magendo ya mafuta.

4) Kupima kiwango cha mafuta kwenye vituo ili kuhakikisha mafuta yanayouzwa ndio yaliyoingizwa kwenye vituo vyao.

Hitimisho, Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano mnayoipa Wizara yangu. Pia ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mhe. Salmin Awadh pamoja na wajumbe wote wa kamati kwa ushauri na maelekezo yao ambayo yametusaidia sana katika kufanikisha majukumu yetu.

Nawaomba wasisite kutushauri wakati wowote, tutapokea ushauri wao kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu.

Mhe. Spika, matarajio yangu kuwa ufafanuzi nilioutoa umewasaidia sana waheshimiwa wajumbe kufahamu utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili.

Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha maagizo na ahadi za Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ukaribu na kufanya kazi zake kwa mashirikiano makubwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Aidha, tunaipongeza sana kamati kwa kuwa pamoja na wizara katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa kila mwaka, pamoja na maagizo yanayotolewa na Kamati katika kuhakikisha Wizara inafikia malengo yaliyowekwa.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imetoa maoni na maagizo 20 yakiwemo 16 mahsusi na 4 ya jumla. Wizara ya Kilimo na Maliasili imeyapokea maagizo hayo kupitia Idara zake zilizopo chini ya wizara na kuyatekeleza ipasavyo kwa mafanikio makubwa kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, agizo Namba 1 ni kwamba elimu ya kilimo bora kwa wakulima itolewe sambamba na kuelewesha namna ya kutumia fursa mikopo ya kukukuza mitaji ili uzalishaji uwe endelevu.

Utekelezaji:

Agizo linafanyiwa kazi wakati wa kuandaa mafunzo kwa wakulima katika vikundi vyao na skuli za wakulima. Mafunzo hayo hutolewa kwa mashirikiano kati ya wataalamu wa fani za kilimo na ushirika, ili kujenga uwezo wa kulima katika kuandaa miradi yao pamoja na kutafuta fursa ya mikopo na vyanzo vyengine vya mitaji. Mfano katika mradi wa *ASSP* jumla ya vikundi 30 vimepatiwa mafunzo yanayohusu ukuzaji wa mitaji yao.

Agizo la Namba 2 ni kwamba vikundi visaidiwe taratibu za kupata hatimiliki wanayotumia kwa kilimo. Mhe. Spika, utekelezaji ni kwamba wizara imevielimisha vikundi vya wakulima kuhusu utaratibu wa kupata haki ya matumizi ya ardhi. Vikundi hivi ni vile vinavyolima mabondeni, juu, na maweni. Mfano kwa kushirikiana na wizara inayoshughulikia ardhi, jumla ya mipango ya usimamizi wa misitu katika shehia 45 za Unguja na Pemba zimetambuliwa na kusajiliwa. Unguja 27, Pemba 18.

Agizo Namba 3 ni kwamba juhudi za kuwafikia wakulima wa vikundi vya maeneo mengine ziendelezwe. Mhe. Spika, utekelezaji ni kwamba juhudi za kuwafikia wakulima na vikundi vya maeneo mengine zinaendelezwa kwa kuwahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi.

Skuli za wakulima zimeongezwa ili kuingizwa vikundi vinavyozalisha mazao yote ya chakula na biashara. Baadhi ya wakulima wenye uwezo zaidi katika

kupokea mafunzo wamejengewa uwezo zaidi ili wawe walimu wa wenzao, ili kuwafikia wakulima wengi zaidi katika kuwapa mafunzo.

Mhe. Spika, agizo la 4 ni kwamba Wizara ya Fedha ihakikishe kutia saini mkataba wa maelewano ili kusaidia kuundwa kwa kitengo cha sera ya huduma za fedha vijijini. Mhe. Spika, utekelezaji ni kwamba Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari zimekamilisha rasimu ya makubaliano ya kuundwa kitengo cha huduma za fedha vijijini kinachosubiriwa ni maoni ya wanasheria na wadau wa maendeleo.

Agizo la 5 Mhe. Spika, ni kwamba tatizo la wataalamu litatuliwe haraka kwa Wizara ya Utumishi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya wafanyakazi wengine wenye uwezo na sifa zinazotakiwa. Utekelezaji Mhe. Spika, ni kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikaa pamoja na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na kulitekeleza agizo hili. Jumla ya nafasi 55 za ajira kwa kada mbali mbali zilitolewa, pamoja na kupeleka maombi maalum kwa ajili ya kuajiri wataalam wa kada nyengine.

Agizo la 6 ni kwamba kamati inashauri upungufu wa upatikanaji wa pembejeo kwa wakati yarekebishwe. Utekelezaji ni kwamba kuanzia msimu wa mwaka 2012 tatizo hilo limetatuliwa na kwamba pembejeo zote zimesambazwa kwa wakati hata kabla ya wakati wa kuanza kutumika. Tayari zilikuwa maghalani zinasubiri wakulima, utaratibu huu ninavyojua ni endelevu wa kila msimu ili kufanikisha uzalishaji.

Agizo la 7 Mhe. Spika, ni kwamba kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kwamba matrekta yanatayarishwa mapema ili msimu wa kilimo ukifika yawe tayari kuanza kazi. Utekelezaji ni kwamba suala hili limekuwa likifanyiwa kazi kila msimu. Mfano kwa msimu wa mwaka 2010/2011 matrekta yalianza kulima tarehe 7/10/2010, msimu wa mwaka 2011/2012 matrekta yalianza kulima tarehe 3/9/2012, na kwa msimu wa wakulima wa mwaka 2012/2013 matrekta yalianza kuingia mabondeni tarehe 20/7/2013. Hata hivyo, Mhe. Spika, wakulima walianza kujitokeza kuanzia tarehe 8/8/2013 kulipa kwa ajili ya kulimiwa, wengine walisema matrekta yamepelekwa mapema mno.

Agizo la 8, kamati inashauri kuchukuliwa hatua za kisheria kwa wale wote wanaojenga karibu na vyanzo vya maji. Utekelezaji ni kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili inahakikisha kwamba vyanzo vyote vilivyo chini ya Wizara vinahifadhiwa na hakuna chanzo hata kimoja ambacho watu wamejenga au kufanya makaazi.

Mfano vyanzo vya maji vilivyomo Chaani Masingini, Jozani Kiwengwa vyote vimehifadhiwa. Na kwa vile vyanzo vilivyokuwa havimo katika maeneo

yasiyokuwa ya hifadhi, wizara imeingia mkataba maalum na wanajamii kuvihifadhi vyanzo vya maji nchini, chini ya mpango wa usimamizi wa raslimali za misitu na hakuna chanzo cha maji kilichohoribiwa.

Agizo la 9 ni kwamba wizara itayarishe mpango wa matumizi ya ardhi, ili kuepuka utumiaji mbaya wa ardhi za kilimo, misitu na vyanzo vya maji. Utekelezaji Mhe. Spika, ni kwamba kazi ya kuyapima na kuyasajili maeneo yote, ukulima wa mpunga na maeneo yote ya hifadhi za misitu ya Unguja na Pemba inaendelea.

Maeneo ambayo kwa kipindi hiki yanafanyiwa kazi ni Hifadhi ya Msitu wa Kiwengwa/Pongwe, Hifadhi ya Taifa ya Jozani kwa Unguja na Hifadhi ya Ngezi, Vumawimbi na Msitu Mkuu wa Pemba. Na kwa upande wa mabonde ya kilimo cha mpunga maeneo ya Cheju, Kibonde Mzungu, maeneo yote ya Wilaya ya Mkoani yamepimwa. Maeneo ya utafiti ya Kizimbani, Kijichi, Selemu, Bambi, Makunduchi na Matangatuani tayari yameshapimwa.

Agizo la 10 Mhe. Spika, kupeleka umeme bonde la Mtwango. Utekelezaji ni kwamba njia kuu ya umeme tayari imefika Mtwango. Transfoma imewekwa na vibanda vya mashine vya kusukumia maji vimejengwa, kinachosubiriwa ni Shirika la Umeme kuunganisha umeme huo kwenye mashine za kusukumia maji.

Mhe. Spika, agizo la 11 ni kwamba wizara iwasaidie wakulima wa mpunga kwa kuwajengea miundombinu. Aidha, juhudi za makusudi zifanyike kukiimarisha kilimo cha umwagiliaji maji na kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua.

Utekelezaji Mhe. Spika, ni kwamba wizara tayari imetayarisha na inatekeleza mpango wa muda mrefu wa umwagiliaji maji. Hivi sasa tayari matayarisho ya kilimo cha umwagiliaji hekta 2,000 umeshaanza.

Agizo la 12 ni kwamba Idara ya Umwagiliaji Maji ipewe fedha zake mapema ili mipango yake ambayo inakwenda sambamba na msimu wa kilimo isikwame, kwa vile msimu hauwezi kusubiri.

Utekelezaji Mhe. Spika, ni kwamba tayari Wizara ya Kilimo na Maliasili imewasiliana na Wizara ya Fedha kuhakikisha fedha zinapatikana kwa mujibu wa *cash flow* ili kuondosha tatizo hili, tulitarajia kamati itaendelea kutusaidia kufanikisha azma hii.

Agizo la 13 ni kwamba kamati imeshauri Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Matangatuani kifanyiwe ukarabati na kupatiwa vifaa vya utafiti.

Utekelezaji ni kwamba wizara imetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Kituo cha Utafiti cha Matangatuani na ununuzi wa vifaa. Hata hivyo, fedha hizo bado hazijapatikana. Sambamba na hilo wizara imeomba vifaa kutoka kwa washirika wa maendeleo wakiwemo *COSTECH* na *IAEA.*

Mhe. Spika, agizo la 14 ni kwamba kwa kuwa wafadhili (KOREA) wamesita kumaliza ujenzi wa Kituo cha Usarifu wa Mazao Kizimbani ni vyema kwa serikali kuchukua hatua za kumaliza ujenzi huo.

Utekelezaji ni kwamba, katika robo ya kwanza serikali imeingiza jumla ya shilingi 39 milioni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huo. Aidha, pamoja na fedha zilizotolewa za *KOICA* wizara imeweza kutia milango, madirisha, sakafu pamoja na kuvuta umeme. Vile vile, wizara inategemea kumaliza ujenzi huo kupitia Mradi wa *MIVARF*.

Agizo la 15 ni kwamba maghala ya hifadhi ya chakula yatengenezwe ili mpango wa hifadhi wa chakula uanze mara moja.

Utekelezaji ni kwamba, Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari imeshapeleka waraka kwa Kamati ya Makatibu Wakuu kuomba uwezekano wa kuyatumia maghala ya serikali ambayo baadhi yao yapo chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kamati ya Makatibu Wakuu imewaelekeza Wizara ya Kilimo na Maliasili kufanya utafiti wa kina juu ya uendeshaji wa hifadhi ya chakula ya Zanzibar ikiwa ni maghala gani yanaweza kutumika kwa kuhifadhi chakula hicho.

Agizo la 16 ni kwamba miradi ya wananchi katika mpango huu ilenge kwenye malengo ya mradi wa kuwezesha wananchi hao kujitosheleza kwa chakula.

Utekelezaji ni kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari katika miradi yote ya kilimo imeshashajihisha wananchi katika kujitosheleza kwa chakula kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkuu wa Mapinduzi ya Kilimo. Mfano, miradi ya umwagiliaji maji kupitia *Exim Bank*, KOREA, *JAICA*, Skuli za Wakulima, kupitia *ASSP* na Miradi ya Maliasili kama hifadhi ya misitu na ufugaji wa nyuki.

Mhe. Spika, yapo maagizo ya jumla. Maagizo ya jumla la kwanza ni kwamba Sekta ya Chakula na Lishe bado haijakidhi matarajio. Hivyo, mpango wa kuwa na hifadhi ya chakula uwe ndio kipaumbele cha malengo yote ya sekta hiyo.

Utekelezaji ni kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili inakubaliana na maelezo ya Kamati ya Hifadhi ya Chakula ipewe kipaumbele. Hivyo bajeti hii tayari fedha zimetengwa kwa ajili ya kukarabati maghala kuelekea katika uhifadhi wa chakula. Pamoja na hayo, hatua zinazoendelea ni pamoja na kutoa elimu na kushajihisha wakulima katika kuzalisha chakula kwa wingi ili Zanzibar iweze kujitosheleza kwa chakula. Kuhamasisha na kutoa mafunzo ya matumizi bora ya vyakula vyenye virutubisho kwa wingi na matumizi kwa mama wajawazito.

Agizo la pili la jumla ni kwamba mashirikiano baina ya mabwana na mabibi shamba pamoja na wakulima yaongezwe badala ya kukaa maofisini.

Utekelezaji ni kwamba, kwanza naomba kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba mabwana na mabibi shamba hawatakiwi kuwepo maofisini kufanya kazi na kwa hivyo hawatarajiwi kukaa maofisini. Ofisi zao ni mashambani kwa wakulima na katika ofisi ya sheha. Wanakwenda Ofisi ya Kilimo ya Wilaya kwa mikutano mara moja kila mwezi kutoa taarifa za kazi zao. Wafanyakazi hawa mbali ya mafunzo yao ya cheti au diploma, pia huandaliwa mafunzo yanayohusiana na kazi zao. Mahusiano na wakulima wanaotarajiwa kusimamia kazi hizo, Maofisa wa Kilimo wa Wilaya na Mikoa, lakini masheha wana wajibu kamili wa kufuatilia utendaji wa kazi katika maeneo yao.

Agizo la tatu la jumla Mhe. Spika, ni kwamba usimamizi wa misaada ya wahisani hauridhishi, eneo hili lifanyiwe kazi zaidi.

Utekelezaji ni kwamba juhudi zinafanyika kuhakikisha kwamba fedha za misaada zinasimamiwa na kudhibitiwa kwa mujibu wa taratibu. Ukaguzi wa miradi pamoja na fedha zinazotumika unafanywa na wahisani wenyewe. Mfano Wizara ya Kilimo na Maliasili imepata tunzo kwa usimamizi mzuri wa fedha kwa programu ya *ASSP* na *ASDPL* kwa nchi za kanda za Mashariki ya Kusini mwa Afrika. Wizara pia imethibitisha udhibiti wake wa matumizi bora ya fedha kama ilivyoainishwa katika ripoti ya *COSTECH*.

Vile vile, Mhe. Spika, matumizi ya fedha za wahisani na za serikali yanakaguliwa na wakaguzi wa serikali wa ndani na nje.

Agizo la nne la jumla ni kwamba makusanyo ya fedha za mazao ya misitu yawekewe kumbukumbu vizuri, kwani ni eneo ambalo mapato hayakusanywi vizuri.

Utekelezaji ni kwamba juhudi zimefanyika za kudhibiti mapato ya makusanyo ya mazao ya misitu pamoja na maliasili zisizorejesheka. Kumbukumbu za

makusanyo zimeimarishwa, ukaguzi wa mara kwa mara unafanyika ili kuhakikisha kwamba mapato yanadhibitiwa. Pia wakusanyaji mapato wamekuwa wakibadilishwa mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba hawazoei katika eneo moja. Juhudi za kuwakamata wahalifu na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria pia kumesaidia sana kuongezeka kwa mapato ya serikali.

Mhe. Spika, kutokana na jitihada hizo wizara inazofanya katika ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, wizara imevuka malengo ya makusanyo ya fedha waliyopangiwa.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitumie fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza lako tukufu kwa miongozo, mashirikiano na ushauri wanaotupa katika kufanikisha malengo ya Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini na taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya (Kny: Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa ahadi na maagizo kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kuanza kutoa taarifa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia sote kuwa na afya njema na uzima uliotuwezesha kufika hapa leo na kuweza kutelekeza majukumu yetu ya kitaifa. Aidha, naomba kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuhusu utekelezaji maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni pamoja na wajumbe wake wa kamati kwa mashirikiano makubwa wanayotupa wizara yetu.

Maendeleo makubwa yanayopatikana katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa sehemu kubwa yanatokana na ushauri pamoja na miongozo inayochangiwa na kamati hiyo. Ushirikiano wetu baina ya kamati na wizara ni mzuri na ndio unaotufanya kuweza kutimiza majukumu yetu ya kuendeleza biashara, viwanda na kuwasaidia wazalishaji na wajasiriamali kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa napenda kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi kwa jinsi wanavyonipa ushirikiano wa dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa wizara yangu. Tunaamini kwamba maelekezo ya Baraza hili tukufu ni sehemu kubwa ya wizara yangu kupata mafanikio katika utekelezaji wa malengo yake. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote waendelee kushirikiana na wizara yangu ili tuweze kuimarisha na kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya shukurani naomba kueleza kwamba katika ripoti za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka 2012/2013, wizara iliweka ahadi na kuagizwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

a) Utekelezaji wa ahadi za wizara

Katika kutekeleza malengo yake wizara iliahidi kufungua duka la karafuu bandarini, kusimamia tatizo la bidhaa chakavu na kufuatilia suala la uwakala kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

Utekelezaji wa ahadi hizo Mhe. Spika, umefanyika, kwani duka limeshafunguliwa, taratibu za uwekaji wa viwango kwa bidhaa chakavu unaendelea na kuhusu suala la uwakala kuwaomba wafanyabiashara wa Zanzibar kuchangamkia fursa za uwakala, kwa wazalishaji wa bidhaa hizo moja moja viwandani na kufunga mkataba na wazalishaji hao. Ufafanuzi zaidi umetolewa katika kiambatisho Nam. 1. Naomba nikisome kwa ruhusa yako.

Kwanza, kufungua duka la karafuu bandarini, eneo kwa ajili ya duka la karafuu limeshapatikana na matengenezo yameshafanyika. Duka hilo limeshafunguliwa na kuanza mauzo yake kuanzia tarehe 2 Januari, 2014.

Pili, kulishughulikia tatizo la bidhaa chakavu kwa kuweka viwango vya ubora. Serikali inakusudia kupigwa marufuku uingizwaji wa bidhaa chakavu ambazo ni nguo za ndani za mitumba mara baada ya kuwekwa saini kwa sheria ya biashara ya mwaka 2013. Sheria ambayo inatoa masharti kuzuia bidhaa hizo.

Aidha, taratibu za kuweka viwango, kutayarisha kanuni na kuweka miongozo kwa bidhaa nyengine zinaendelea chini ya sheria ya viwango kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira ili kuhakikisha kwamba bidhaa chakavu zinadhibitiwa bila ya kuathiri maisha ya wananchi wa kawaida.

Tatu, suala la uwakala lisiwe kwa wafanyabiashara wa Tanzania Bara peke yake. Suala la uwakala linakubalika katika biashara kwa kuwa wazalishaji na wenye viwanda ni moja ya aina au nyezo ya utafutaji masoko ya bidhaa wanazozalisha.

Waagizaji wengi wa bidhaa huingia mikataba na wenye viwanda na huchapisha majina ya bidhaa zao kwa majina yao wenyewe. Kwa mfano bidhaa ya mafuta ya kula aina ya *Primium*, dawa ya mbu aina ya *HIT*, maziwa ya *NIDO* ni aina ya bidhaa zinazoingizwa na wafanyabiashara maalum ambao ndio wakala wa kuingiza bidhaa hizo.

Mhe. Spika: Naomba Waheshimiwa Wajumbe tuwe watulivu ili hotuba hii inayosomwa najua pengine mshaisoma, lakini hatimae tuweze kuichangia vizuri na shughuli yetu iwe nyepesi. Kwa hiyo, mazungumzo yakiwa mengi hatutaweza kusikia kile kinachoendelea na kusomwa na Mhe. Waziri. Nakuombeni sana, Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika. Suala la uwakala kwa upande wa wafanyabiashara wa Tanzania Bara pia liko kama mawakala wa biashara nyengine zilivyo. Hivyo, wizara inawaomba wafanyabiashara wa Zanzibar kufanya mazungumzo na wazalishaji wa bidhaa moja kwa moja viwandani na kuingia nao mikataba ili wapewe uwakala, na serikali itatoa msaada wa ufafanuzi kwa wabia hao.

Tano, kupunguza ushuru wa malighafi kwa wazalishaji wadogo. Wazalishaji wengi wadogo wadodo wanatumia malighafi za ndani ambazo hazitoleshwi ushuru. Aidha, wapo wazalishaji wanaoingiza malighafi kutoka nje ya nchi ambao wapo chini ya *ZIPA* na huombewa unafuu wa ushuru kupitia mamlaka hiyo chini ya sheria ya uwekezaji. Hivyo, ni vyema wafanyabiashara wanaohitaji malighafi kutoka nje wakasajiliwa chini ya sheria ya uwekezaji ambayo inaruhusu uingizaji malighafi bila ya ushuru.

Sita, kufanya malipo kupitia benki kwa wateja au wakulima wanaouza karafuu nyingi. Hatua mbali mbali zimechukuliwa za kuwahamasisha na kuwaelimisha wakulima kutumia huduma za kibenki kwa ajili ya kufanya malipo ya karafuu. Jambo ambalo linapelekea kuwepo usalama wa fedha zao. Hata hivyo, bado kuna muitikio mdogo kutoka kwa wakulima kutumia huduma za benki. Aidha, wizara inawaomba Waheshimiwa wote wa Baraza hili kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao kutumia huduma za kibenki kwani itapelekea usalama wa fedha zao.

Saba, kuongeza juhudi za kutoa elimu kwa wananchi ili kuondosha magendo ya karafuu. Juhudi mbali mbali zimechukuliwa za kutoa elimu kwa wananchi

juu ya athari za magendo ya karafuu na kuwaomba wananchi kuachana na vitendo hivyo. Elimu hiyo imetolewa kwa njia ya semina, warsha, makongamano, michezo ya kuigiza na kwa kutumia vipindi vya redio na televisheni. Juhudi hizo zimeleta mafanikio kwani ununuzi wa karafuu umeweza kuvuka malengo yaliyowekwa.

Nane, Shirika la *ZSTC* lipewe uhuru wa kufanya shughuli zake kama sheria yake ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Shirika la *ZSTC* limepewa uhuru wa kufanya shughuli zake, kwani tayari serikali imeshaunda Bodi ya Wakurugenzi inayosimamia utendaji na uendeshaji wa shirika hilo, ambayo ndio msimamizi mkuu wa shirika hilo.

Mhe. Spika, naomba nirudie sehemu ya pili sasa utekelezaji wa malengo ya kamati. Mhe. Spika, wizara iliagizwa na kamati kutekeleza maagizo mbali mbali yakiwemo utekelezaji wa mkakati wa *ZES* kwa kuzingatia miundombinu na suala la ardhi, kufanya ukaguzi wa viwanda, kutoa usaidizi wa *SME's*, kuondosha magendo ya karafuu, kupunguza ushuru kwa mali ghafi na kufanya malipo kupitia benki kwa wakulima wa karafuu.

Mhe. Spika, utekelezaji wa maagizo hayo ni kwamba maeneo yaliyopendekezwa na kamati katika utekelezaji wa *ZES* ni mtambuka na yatazingatiwa. Ukaguzi wa viwanda 30 umefanyika, usaidizi kwa baadhi ya miradi umetolewa na hatua mbali mbali za kuwaelimisha wananchi kuhusu athari za magendo ya karafuu zimechukuliwa.

Kuhusu msamaha wa malighafi ni vyema miradi hiyo ikasajiliwa chini ya sheria ya uwekezaji ili wajasiriamali waweze kufaidika. Mhe. Spika, bado kuna changamoto kutoka kwa wakulima wa karafuu kulipwa pesa zao kupitia benki, kwani wengi wao wanahisi kwamba wanakopwa fedha hizo. Kiambatisho nambari mbili kinafafanua, naomba nikisome kiambatisho hicho ili kukamilisha waraka huu.

Moja, mpango wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu la kiuchumi utafanikiwa ikiwa itakuwepo miundombinu ya barabara na bandari.

b) Maji na Nishati endelevu
c) Nguvu kazi za wataalamu
d) Mpango bora wa matumizi ya ardhi
e) Kutumia fursa za masoko ya nje kwa kuongeza uzalishaji na viwango; na
f) Umeme wa bei nafuu.

Utekelezaji. Maeneo yote yaliyoagizwa na kamati ni mtambuka na yanahitaji utekelezaji wa muda mrefu katika sekta husika. Hivyo maeneo hayo yatazingatiwa katika utekelezaji wa mkakati huo.

Mbili, wafanyabiashara wa Kiwanda cha *SAVANA* wakubaliane katika suala la muda wa kuanza kazi na kumaliza kazi. Wafanyakazi wa kiwanda hicho hivi sasa wanapata mapumziko kuanzia saa 6:45 mpaka saa 7:45 (muda wa saa moja mchana) na kumaliza kazi saa 10:00 jioni.

Tatu, kufanya ukaguzi katika viwanda mara kwa mara ili kuona mazingira ya kazi na usalama wa wafanyakazi. Jumla ya miradi ya viwanda 30 imekaguliwa katika kipindi hiki, kati ya lengo la kukagua miradi 120 kwa mwaka 2013/2014. Ukaguzi huo umeangalia pamoja na mambo mengine suala la mazingira ya kazi na usalama wa wafanyakazi na kutoa mapendekezo au kuelekeza hatua zinazostahiki kuchukuliwa.

Nne, kuwasaidia wazalishaji wadogo mitaji ya kukuza biashara zao. Wizara inaendelea kutoa usaidizi kwa wazalishaji wadogo. Miradi waliyopatiwa usaidizi ni mradi wa chumvi wa *AZASPO*, kikundi cha Ulezi una Kazi Fujoni, Jumuiya ya Wakulima wa Ndimu Chwaka na Kikundi cha *ZAIDATI and BASMA*. Usaidizi huo ulikuwa katika ununuzi wa mashine, ukarabati wa majengo na kusaidia mfumo wa uzalishaji chumvi wa Kiwanda cha *AZASPO*.

Mhe. Spika, pamoja na taarifa hiyo naomba rasmi kuwasilisha baada ya maelezo hayo ya jumla. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako wapitie viambatisho vya taarifa hii ili kupata ufafanuzi zaidi na agizo moja baada ya moja. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na utekelezaji wa maagizo ya Kamati hii, iliyoyatoa kwa wizara inazozisimamia kwa kipindi kilichopita cha mwaka 2012/2013. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kwa ajili ya kuwasilisha muhutasari wa ripoti ya Kamati hiyo kwa mwaka 2013/2014 kama ilivyoelezwa na kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza lako tukufu, Toleo la 2012.

Aidha, napenda kuitumia nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kukushukuru wewe Mhe, Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Mratibu wa Shughuli za Kamati na watendaji wako wote kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake zote bila ya matatizo kwa kipindi chote .

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee, napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano yao makubwa waliyayonesha katika kipindi chote cha utekelezaji wa kazi za Kamati. Ni ukweli usiopingika kuwa mashirikiano yao ndio nyenzo pekee iliyoifanya Kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, shukurani zangu maalum ziende kwa Waheshimiwa Mawaziri wakiwemo Waziri wa Fedha, Mhe. Omar Yussuf Mzee, Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pamoja na Naibu Waziri wa Wizara hio Mhe. Thuwibah Edington Kisasi.Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Suleiman Othman Nyanga, Kaimu Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban pamoja na Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak kwa mashirikiano makubwa waliyotupa wakati wa utekelezaji wa kazi za Kamati.

Mhe. Spika, nisingependa kusahau kutoa shukurani zangu za dhati kwa Makatibu Wakuu wao wa wizara hizo, Manaibu Makatibu Wakuu, Makamishna, Wakurugenzi, Maafisa Wadhamini walioko Pemba, Wakuu wa Vitengo na wa Taasisi mbali mbali pamoja na wafanyakazi wote wa wizara hizo kwa kushirikiana bega kwa bega na Kamati, wakati wote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106 ya Kanuni za Baraza lako tukufu toleo la 2012 . Aidha, majukumu ya Kamati hii yamefafanuliwa katika kanuni ya 110 ya kanuni hizo za Baraza. Katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati hii imepewa dhima ya kusimamia Wizara tatu (3) zifuatazo :-

1. Wizara ya Kilimo na Maliasili,
2. Wizara ya Fedha; na
3. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, kwa upande wa muundo wa Kamati, Kamati hii imeundwa na wajumbe saba(7) na makatibu wawili na kama nilivyoeleza hapo awali kuwa Kamati imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa baina ya Wajumbe pamoja na makatibu wake. Hivyo, kwa kuthamini mchango wao mkubwa, naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe na makatibu hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Hijja Hassan Hijja - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdu Haji - Mjumbe
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
5. Mhe. Hamad Masoud Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
8. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu
9. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu

Mhe. Spika, Kamati katika ripoti yake ya mwaka uliopita wa 2012/2013 ilitoa Maoni na Maagizo 26 kwa iliyokuwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ya Maendeleo ambayo sasa inaitwa Wizara ya Fedha ambayo hivi punde Baraza lako tukufu limepokea utekelezaji wa Maagizo hayo. Vile vile Mh. Spika, Kamati ilitoa Maoni na Maagizo 20 kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili ambapo hivi punde Baraza lako tukufu limepokea namna ya utekelezaji wake.

Aidha, Mhe. Spika Kamati yako ya Fedha, Biashara na Kilimo ilitoa Maoni na Maagizo manane (8) kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko amabayo nayo Waheshimiwa Wajumbe wamepokea taarifa ya utekelezaji wake.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita baina ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Kamati ilianza kutekeleza shughuli zake kwa Unguja, kuanzia tarehe 9/09/2013 hadi tarehe 20/09/2013. Aidha, Kamati ilikwenda Pemba na kufanya shughuli zake huko kuanzia tarehe 18/11/2013 hadi tarehe 29/11/2013. Katika mzunguko wa tatu, Kamati ilifanya kazi zake Unguja kuanzia tarehe 30/12/2013 hadi tarehe 3/1/2014. Na kumalizia mzunguko huo wa tatu kwa kufanya kazi zake huko Tanazania Bara kuanzia tarehe 6/1/2014 hadi tarehe 10/1/2014.

Mhe. Spika, Kamati yetu kimsingi imeridhika na utendaji wa wizara zote tatu ilizozitembelea ijapokuwa haikurihishwa na hali ya uingizwaji wa fedha kwa baadhi ya wizara hizo hususan Wizara ya Kilimo na Maliasili. Hata hivyo, Kamati inawapongeza kwa dhati watendaji wa wizara zote kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao, licha ya mazingira magumu wanayokabiliana nayo.

Mhe. Spika, naomba sasa niwasilishe mbele ya Baraza lako tukufu, muhutasari wa taarifa ya utekelezaji wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo

ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 kwa kuchambua wizara moja moja kama ifuatavyo:-

WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Mhe. Spika, Sekta ya Kilimo na Maliasili bado zinaendelea kuwa ni mihimili mikuu ya uchumi wa Zanzibar. Sekta hizi zinatoa mchango wa moja kwa moja kwa kujikimu kimaisha, na kuwa na uhakika wa chakula na lishe kwa wananchi waliowengi vijijini na mijini. Takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 sekta hizi zilichangia asilimia 30.2 ya Pato la Taifa na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea sekta hizi kwa kuwapatia ajira na kipato

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu mkubwa wa Sekta hizo za Kilimo na Maliasili kwa nchi yetu,bado uingizwaji wa fedha kwa Wizara ya Kilimo kama ni msimamizi mkuu wa kuziendeleza Sekta hizo umekuwa si wa kuridhisha. Katika taarifa ya utekelezaji wa malengo ya wizara kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2013, kamati imesikitishwa kuona kuwa mchango wa serikali kwa kazi za Maendelo ni asilimia 16 tu na zile za wahisani zilizopatikana hadi kipindi hicho ni asilimia 4 tu ya makadirio. Cha kusikitisha zaidi ni kuwa baadhi ya taasisi muhimu za Wizara hii zimekosa kabisa fedha za Maendeleo kwa kutoingiziwa fedha yoyote ya maendeleo kutoka serikalini.

Mhe. Spika**,** kutokana na hali hiyo kamati inaiomba sana serikali kutekeleza kwa vitendo, kauli mbiu zake ikiwemo kauli mbiu ya "Kuleta Mapinduzi ya Kilimo" kwa kuingiza fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza kazi mbali mbali za Maendeleo zinazotekelezwa na Wizara hii kwani kwa vyovyote vile asilimia 16 tu iliyoingizwa katika Wizara hii kati ya fedha za SMZ zilizokadiriwa kwa kazi za maendeleo ni finyu sana na kamwe haiwezi kutimiza kikamilifu azma ya serikali ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo hapa nchini.

Mhe. Spika, Idara hii ndio kiini cha Wizara hii kwa kuwa imebeba majukumu makuwa ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima, uhifadhi na ukaguzi wa mazao na kutoa mafunzo kwa wazalishaji.

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona kuwa idara hii imekuwa ikikabiliwa na deni kubwa amabapo kamati ilielezwa kuwa wakulima wa mikataba wanaozalisha mbegu za mpunga katika mabonde mbali mbali wanaidai Wizara jumla ya Tsh millioni 240 baada ya wizara

kuchukua mpunga huo bila ya kuwalipa kwa zaidi ya miezi minne ambapo wakulima wa bonde la Mtwango pekee ambao walikutana na Kamati mwezi wa Disemba 2013, wanaidai wizara Tsh Millioni 60.

Hali hii inawaumiza wakulima hao wanyonge ambao hutegemea fedha hizo kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Aidha, tatizo hilo linaweza kuathiri uzalishaji wa mbegu za mpunga kwa kuwa linawavunja moyo wakulima.

Mhe. Spika, kutokana na kusononeshwa sana na tatizo hili, Kamati imeiagiza Wizara ya Fedha ambayo pia inasimamiwa na Kamati hii kufanya kila iwezalo kuhakikisha kuwa inaingizia fedha Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa ajili ya kulipa deni hilo kwa wakulima na hivyo kuwaondolea dhiki wanayoendelea kuipata wakulima hao wanaozalisha mpunga wa mbegu hapa nchini.

Mhe. Spika, tatizo la uchelewaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo limekuwa likiathiri sana utekelezaji wa majukumu ya Idara hii hususan katika matayarisho ya kilimo mpunga kwa kutumia matrekta**.** Wakati Kamati ilipotembelea karakana ya matrekta, Chake Chake, Pemba mwezi Novemba 2013, ilielezwa kuwa kutokana na uchelewaji huo wa fedha Idara ilikuwa bado haijakamilisha kuzilima eka 556 za wakulima licha ya kuchukua fedha za wakulima hao kwa ajili ya matayarisho ya mashamba yao ya mpunga. Hivyo, Serikali inapaswa kuwa makini katika kulipa kipaumbele suala la matayarisho ya kilimo cha mpunga hasa ikizingatiwa kuwa kilimo chenyewe ni cha kutegemea mvua za msimu wenye wakati maalum.

Mhe. Spika, uhaba na uchakavu wa matrekta na vifaa vyake ni changamoto sugu inayochangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha na kucheleweshaji shughuli za kilimo. Kwa mfano mwezi wa Disemba, 2013 Kamati imeshuhudia kutokamilika kwa kazi za uburugaji katika bonde la mpunga Muyuni ambalo lilikuwa limeshalipiwa gharama zote kwa ahili ya kazi hiyo, lakini kuharibika kwa trekta lilikuwa likifanyakazi katika bonde hilo kwa wakati huo kulipelekea kusita kwa kazi hiyo kwa wakati huo ambao kamati ilikuwa ikilitembelea bonde hilo.

Katika kulifanyia kazi tatizo hilo, kamati inaipongeza wizara kwa kuandaa mpango wa kutaka kuleta matrekta 20 kwa ajili ya kusaidia shughuli hizo muhimu. Aidha, Kamati inaisihi wizara kuhakikisha kuwa ongezeko hilo la matrekta linaenda sambamba na ongezeko la watendaji kazi wakiwemo mafundi wa matrekta hayo ambao ni wachache.

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kaendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini pamoja na kutoa taaluma za kiufundi juu ya ujenzi na

ukarabati wa miundombinu pamoja na kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, Kamati ilipata nafasi ya kulitembelea bonde la Makombeni ambalo liliingizwa katika Mradi maalum wa kutaka kulifanya bonde hilo kuwa la umwagiliaji maji kwa kushirikiana na serikali ya Japan ambapo hadi sasa jumla ya Tsh 311,877,550 zimeshatumika katika mradi huo. Hata hivyo, kazi ya umwagiliaji katika bonde hilo bado hazijaanza kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo tatizo la ardhi hiyo kutowekwa sawa (*land levelling*) kwa ajiii ya kilimo cha umwagliaji maji, licha ya kuwa baadhi ya huduma zikiwemo za maji na umeme tayari zimeshakuwepo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mradi huo wa bonde la Makombeni limechukuwa muda mrefu kukamilika, Kamati inaona kuna haja ya kuwepo kwa nguvu za pamoja ikiwa ni pamoja na viongozi wa Wizara na watendaji wa Idara ya umwagiliaji maji, kukaa pamoja na wakulima wa bonde la Makombeni kwa ajili ya kujadiliana juu ya suala la kuweka sawa ardhi ya bonde la Makombeni ili kukubaliana juu ya hatua muafaka za kuchukuliwa kwa ajili ya kutatua tatizo hilo na hatimae lile lengo la kulifanya bonde hilo kuwa la kilimo cha umwagiliaji maji liweze kufikiwa.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa bonde la Mtwango**,** kamati ilijionea hatua mbali mbali zilizofikiwa katika kulifanya bonde hilo kuwa la umwagiliaji maji zikiwemo kuvutwa kwa umeme, kujengwa kwa vibanda viwili vya kuendeshea pampu za kusukumia maji pamoja na kuwepo kwa visima ambavyo vimekamilka kuchimbwa miaka mitatu iliyopita. Aidha, kamati ilipata fursa ya kuzungumza na wakulima mbali mbali wa bonde hilo.

Mhe. Spika, Kamati ilibaini kutoanza kutumika kwa visima vilivyochimbwa kwa ajili ya umwagiliaji maji kutokana na kutokamilika kwa kazi ya kushusha umeme na kuupeleka katika vibanda vya kuendeshea pampu za maji licha ya Shirika la Umeme kulipwa asilimia 60 ya gharama zote za Umeme (sawa na Tsh, 59 millioni kati ya Tsh 99 Millioni) zikijumuisha na gharama ya kazi hiyo, kama walivyokubaliana kati yake na wizara.

Mhe. Spika, kwa kupitia mkutano huu kamati inaliomba Shirika la Umeme kuharakisha na kukamilisha kazi iliyobakia ya kushusha umeme katika vibanda vya kuendeshea pampu za maji katika bonde la Mtwango kama walivyokubaliana kati yake na wizara. Aidha, Kamati inaiomba Wizara kwa upande wake kuongeza jitihada za kufuatilia Shirika la Umeme ili kuona kuwa kazi hiyo inakamilishwa ipasavyo.

Aidha, Kamati pia inaitaka wizara kuharakisha malipo ya Tsh millioni 6 kwa ajili ya fidia kwa wakulima na wananchi waliokatiwa miti na vipando vyao wakati wa kutaka kupitishwa umeme katika bonde hilo la Mtwango.

Mhe. Spika, jukumu kubwa la Idara hii ni kulinda na kuhifadhi misitu ya asili na wanyama pori, kusimamia mashamba ya misitu na mbegu, upatikanaji wa miche bora pamoja na kuratibu uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Spika, kwa kuwa sehemu kubwa ya utekelezaji wa majukumu ya Idara hii inahitaji ushirikishwaji mzuri wa wanajamii hasa walioko vijijini, Kamati inaomba Wizara kuzidisha juhudi za kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu kuhifadhi misitu ikiwa ni pamoja umuhimu wa kupanda miti na athari za kukatwa miti ovyo.

Mhe. Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu la kupanga na kutekeleza kazi za Utafiti katika sekta za Kilimo na Maliasili na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi na wadau wengine.

Mhe. Spika, pamoja na jukumu hilo kubwa ililopewa taasisi hii Kamati ilisikitishwa kuona kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2013, taasisi hii ilikuwa haijaingiziwa fedha yoyote kwa ajili ya kazi za maendeleo ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, ilitengewa jumla ya Tsh 140 millioni kutoka serikalini. Aidha, kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2012/2013 Taasisi hii iliingiziwa Tsh 41 millioni tu kwa kazi za maendeleo kati ya Tsh 400 millioni ilizoidhinishiwa sawa na asilimia 10 tu.

Mhe. Spika, hiki ni chuo pekee cha serikali chenye jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo, maliasili na mifugo katika ngazi tofauti hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio kadhaa yaliyofikiwa chuoni hapo, chuo bado kinaonekana kukabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo za ukosefu wa mtaalam wa maabara ya mifugo na kutokuwepo kwa ulinzi wa uhakika wakati wote Chuoni.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, kamati inaitaka Wizara kubuni mbinu za ziada ili Chuo cha Kilimo, Kizimbani kiweze kupata mtaalam wa maabara ya Mifugo. Aidha, Wizara inapaswa kuongeza jitihada zitazokifanya Chuo cha Kilimo Kizimbani kuwa na ulinzi wa uhakika wa masaa ishirini na nne kama vilivyo vyuo vyengine, ili kukiepusha Chuo hicho na hatari ya matukio ya wizi.

Mhe. Spika, madhumuni ya kuanzishwa Programu hii ni kuwawezesha na kuwaendeleza wafugaji na wakulima kuinua hali zao za kipato na kuwapunguzia umaskini kwa kuwapa taaluma ya kilimo na ufugaji bora.

Mhe. Spika, wakati Kamati ilipotembelea skuli za wakulima ilibaini changamoto ya Uhaba wa maji katika mashamba.Changamoto hii husababisha usumbufu mkubwa katika kuendesha kilimo katika mashamba hayo. Aidha, kumekuwa na gharama kubwa za huduma ya maji kwa matumizi ya shamba hizo pamoja na zile za wanajamii wenyewe waliopata taaluma ambapo wakulima hutakiwa kulipa Tsh 20,000 kwa mwezi.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo**,** kamati inaiomba wizara kwa kushirikiana na mamlaka inayohusika na huduma ya maji zikae pamoja kwa ajili ya kuona uwezekano wa namna ya kuwasaidia wanajamii hao juu ya kupata unafuu wa gharama za matumizi ya maji katika mashamba yao na katika maeneo yao mengine ya kilimo. Aidha, Kamati inaitaka Wizara ianze kubuni miradi mengine mipya ya kuwanufaisha wafugaji na wakulima waliopata taaluma ya kutosha ili iweze kuwaendeleza baada ya miradi iliyopo kumaliza muda wake.

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba ni kiunganishi katika kuhakikiha kuwa majukumu, malengo na shabaha zote za Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa upande wa Pemba, zinatekelezwa kama zilivyokusudiwa. Msimamizi Mkuu wa ofisi hii ni Afisa Mdhamin akisaidiwa kwa karibu na wakuu wa Idara mbali mbali walioko Pemba.

Mhe. Spika Kamati imebaini kuwa Wakuu wa Idara walioko Pemba wa wizara hii na wa wizara nyengine hawalipwi stahiki zozote zinazolingana na nyadhifa zao isipokuwa mshahara wa kawaida tu. Ni vizuri ikakumbukwa kuwa Wakuu wa Idara Pemba hufanya kazi ngumu zaidi za kumsaidia Afisa Mdhamin Pemba na pia huwasaidia wakurugenzi wa Idara walioko Unguja. Hivyo, kuwaacha Wakuu hawa wa Idara Pemba bila ya kuwatizama kimaslahi si haki hata kidogo na kunawavunja moyo na ari ya kufanya kazi hasa ikizingatiwa kuwa Maofisa Wadhamin na Wasaidizi wahasibu walioko Pemba maslahi yao ni mazuri.

La kusikitisha zaidi, kwa utaratibu huu uliopo sasa unawafanya Wakuu wa Idara kupitwa kimshahara na watendaji wanaowaongoza wenye elimu za juu zaidi kuliko wao. Hivyo, ni vyema kwa serikali kuangalia upya maslahi ya Wakuuu wa Idara Pemba ili yaweze kulingana na nyadhifa pamoja na majukumu mazito waliyonayo.

Mhe. Spika, Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji wa Umma. Idara hii ina majukumu mbali mbali yakiwemo kufuatilia taratibu za ununuzi na uhakiki

wa Mali za Serikali pamoja na kuendeleza tathmini ya mali za serikali katika wizara mbali mbali

Mhe. Spika, wakati ilipokuwa katika kazi zake kisiwani Pemba, kamati ilipata taarifa juu ya changamoto kubwa inayoikabili Idara ya ukosefu wa taarifa za uhakika kuhusu mali za serikali na maeneo zilipo hususan mashamba kutokana na mabadiliko mbali mbali yaliyotokea katika maeneo ambayo mali hizo zipo.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, kamati inaiomba wizara kupitia Idara ya Uhakiki Mali iwe na ushirikiano wa karibu kati yake na taasisi nyengine za serikali ili kupatikana usahihi wa taarifa za kumbukumbu za Mali za Serikali zilizo sawa kwa pande zote mbili ili kuondoa migongano ya taarifa hizo baina ya Idara ya Uhakiki Mali na taasisi nyengine za serikali.

Mhe. Spika, Kamati inaupongeza uongozi na watendaji wa Mfuko wa *ZSSF* kwa utendaji mzuri wa kazi zao na jitihada mbali mbali wanazozichukua katika kuwasaidia wananchi katika kuhifadhi na kuwapatia mafao yao ikiwemo kuanzisha huduma ya uchangiaji kwa hiari *Voluntary Scheme* inayowapa fursa hata watu binafsi waliojiajiri wenyewe kuweka fedha zao na kufaidika na huduma zinazotolewa na Mfuko huo .

Mhe. Spika, hata hivyo. Kamati unautaka Mfuko uongeze njia za kutoa taaluma juu ya huduma mbali mbali zinazotolewa na Mfuko huo ili wananchi wengi zaidi wawe na mwamko wa kuzitumia fursa zinazotolewa na Mfuko huo. Aidha, ni vyema kwa uongozi wa Mfuko kufikiria suala la kuongeza idadi ya wafanyakazi ili kuongeza ufanisi katika kazi za kila siku za Mfuko huo kwa Pemba kwani idadi ya wafanyakazi wa taasisi hii kwa Pemba ni wachache sana.

Mhe.a Spika**,** Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi *ZIPA* ina jukumu kubwa la Mamlaka hii ni kushajiisha wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza nchini pamoja kuwasaidia wawekezaji kufikia malengo yao ya uwekezaji.

Mhe. Spika, katika kufanikisha kikamilifu lengo la kuanzishwa kwa taasisi hii, Kamati inaona kuna haja kubwa kwa wizara kufanya kila inaloliweza kuhakikisha kuwa fedha kwa ajili ya utayarishaji wa *"Master Plan"* ya maeneo huru, Fumba zinapatikana na hivyo kazi hiyo kukamilishwa kama ilivyokusudiwa. Aidha**,** Kuna haja kwa mamlaka hii kuzidisha utoaji wa elimu kwa wananchi, viongozi na wawekezaji mbali mbali juu ya taratibu za serikali katika ardhi ya wawekezaji hapa nchini.

Mhe. Spika, kamati ilipata nafasi ya kutembelea ofisi mbali mbali za Shirika la Bima zilizopo Pemba, Arusha na Dar-es-salaam ambapo kimsingi imeridhishwa sana na utendaji mzuri wa kazi wa Shirika hili katika ofisi hizo uliopelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika Shirika hilo kwani takriban ofisi zote hizo zimevuka lengo la makusanyo ya mapato.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika shirika hili, kamati inaona ipo haja kwa uongozi wa shirika kufikiria kuongeza wafanyakazi katika ofisi yake iliyoko Pemba kutokana na wingi wa kazi ilizonazo, kwani hadi Kamati ilipokuwa ikiitembelea ofisi hiyo mwezi wa Novemba, 2013, Ofisi hiyo ilikuwa ina wafanyakazi wawili tu, Meneja na Mhasibu wake.

Aidha, Kamati inasisitiza kuwa Shirika libuni mbinu na mikakati imara itakayowezesha kukabiliana na ushindani unaotokana na ongezeko la kampuni nyingi za Bima hapa nchini ikiwemo ya kujitangaza ili kufahamika zaidi kwa wananchi na kwa makampuni mbali mbali. Kamati pia inaliomba Shirika kuzitumia kikamilifu huduma za Benki ya *PBZ* hususan kwa ofisi za Shirika hili zilizoko Tanzania Bara ili kusaidia kuimarisha Benki hiyo.

Mhe. Spika**,** kwa kuwa kuna hofu kuwa eneo lililokusudiwa kujengwa ofisi za shirika hili huko Pemba haliko katika mazingira mazuri, ni vyema kwa serikali kulifikiria kwa moyo wa huruma suala la kulipatia Shirika la Bima eneo jengine kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Shirika hilo kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, Benki ya Watu wa Zanzibar ina jukumu kubwa la kupokea amana za wateja wake na kukopesha kwa wanaohitaji pamoja na kuwapatia wateja huduma mbali mbali za kibenki.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaupongeza sana uongozi na watendaji wa *PBZ* kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Benki hiyo siku hadi siku. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Benki hiyo, Kamati inaiomba serikali kuiongezea mtaji Benki ya Watu wa Zanziabar ili iweze kupanua masoko yake ya kifedha na kuweza kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya teknolojia za kibenki Duniani hivi sasa.

Kamati inatoa msisitizo huo kwa serikali kwa kuwa ni muda mrefu sasa serikali haijaiingizia mtaji Benki yake hiyo jambo ambalo linahatarisha utendaji wa Benki hiyo kwa vile Mabenki mengi hivi sasa huwa yanaingiziwa mitaji na wamiliki wake kila baada ya muda ili kuweza kukabili ushindani wa huduma za mabenki na kwenda sambamba na ukuaji wa teknolojia za kisasa inayotawala katika huduma za mabenki hivi sasa hapa nchini.

Mhe. Spika, kamati pia inapenda kutoa wito kwa taasisi na mashirika mbali mbali ya serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenye ofisi zao Tanzania Bara kuyatumia kikamilifu matawi ya Benki hiyo yaliyoko huko Tanzania Bara kwa kuweka fedha zao katika matawi hayo ili kukuza na kuendeleza huduma za benki hiyo.

Mhe. Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar *ZRB* imeanzihwa chini ya sheria namba 7 ya mwaka 1996 kama Taasisi ya ukusanyaji mapato ya serikali yatokanayo na vyanzo vya ndani ambapo mnamo mwezi wa Septemba, 1998 Bodi hii ilianza kazi zake rasmi.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza sana *ZRB* kwa kazi nzuri ya kuhakikisha inafikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kama inavyopangiwa, Hata hivyo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaamini kuwa mapato mengi zaidi yanaweza kupatikana iwapo Bodi hii itaweka mikakati madhubuti ya kuziba mianya ya upotevu wa mapato ikiwemo kuiga mbinu zilizotumiwa na nchi jirani ikiwemo Kenya za kuwafanya wafanya biashara hata wadogo kutoa risiti kwa hiari baada ya mauzo.

Aidha, ushirikiano wa karibu zaidi baina ya *ZRB*,vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi ndio njia pekee ya kutokomeza biashara ya magendo hususan mafuta ambayo huikosesha mapato serikali. Aidha, Kamati inaisisitiza Bodi kuendelea kuimarisha elimu kwa walipakodi na wananchi kwa ujumla, ili kujua kikamilifu taratibu za ulipaji kodi na kuweza kulipa kodi kwa hiari.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA*. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inapokea taarifa ya utekelezaji wa Mamlaka hii katika Ofisi ya Zanzibar kwa kipindi cha Julai Disemba, 2013 ilielezwa kuwa Mamlaka katika kipidi hicho imeweza kukusanya mapato kwa asilimia 90.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa miongoni mwa sababu zilizopelekea kutofikia lengo ni kuwa Miradi yote ya Kitaifa (*Strategic Investment*) iliyosajiliwa *ZIPA* imesamehewa na serikali kulipia kodi ya asilimia 15. Ingawa wakati wa upangaji wa malengo ilikuwa imeamuliwa na serikali kuwa wawekezaji wote wangelipia asilimia 20 ya msamaha watakaopewa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014. Hivyo, *TRA* waliikosa asilimia 20 hiyo yote.

Mhe. Spika, Pamoja na faida inayopatikana kutokana na miradi hiyo ya kitaifa ikiwemo upatikanaji wa fursa za ajira na nyenginezo, Kamati inaona kuna haja kwa serikali kufanya utafiti wa kina ili kujua kwa kiasi gani misamaha ya kodi inalinufaisha Taifa hili na haiwanufaishi watu wachache tu.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipata pia nafasi ya kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa Huduma za Jamii Mijini (*ZUSP*) ambao umekuwa ukiulizwa sana na wananchi na baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na ukimya wake wa muda mrefu.Mradi huu unakusudia kuimarisha na kuendeleza huduma pamoja na kujenga uwezo wa kitaasisi wa Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji Mikuu ya Chake Chake, Wete na Mkoani.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepata wasi wasi juu ya kutopatikana kikamili kwa mafanikio katika Mradi huu kutokana sababu zifuatazo:

i. Kukosekana umakini na utaalamu wa kupanga bajeti za Miradi kumepelekea kuwepo na bajeti iliyo tofauti na mahitaji halisi ya fedha katika utekelezaji wa miradi midogo midogo ya mabaraza ya Miji. Kwa mfano Mradi wa *'Stand*" ya magari ya Michakaeni ulikisiwa kuhitaji Tsh billioni 8 wakati fedha zilizopo kwa ajili ya mradi huo ni Tsh Billioni 2 tu.

ii. Kutopatikana kwa ufanisi kwa kazi ambazo zimeshaanza kutekelezwa ikiwemo kazi ya ujenzi wa vibaraza vya kuwekea kontena za taka. Kamati ilibaini kuwa hadi mwezi wa Septemba, 2013 kiasi ya vibaraza 40 tu kati ya 190 ndivyo vilivyojengwa. Tatizo lililojitokeza kwenye shughuli hiyo ni kuwa maeneo mengi yaliyokusudiwa kujengwa vibaraza hivyo yalikuwa yameshavamiwa na wananchi, pamoja na kukataa kwa wananchi wa baadhi ya maeneo kujengewa vibaraza hivyo. Aidha,baadhi ya maeneo yalikuwa hayawezi kufikika vizuri.

Mhe. Spika, Mradi wa *E- Govvernment* ni mradi ulioibua mjadala mkali katika Baraza wakati wa mkutano wake wa kumi na mbili wa Bajeti, mwaka 2013/2014 kwa sababu mbali mbali, zikiwemo hoja za kwamba gharama za Mradi huu ambazo ni dola za Marekani Millioni 20 ni kubwa na kwamba mradi haujaleta manufaa. Hivyo, ikaonekana ipo haja kwa Kamati za Kisekta kufuatilia Mradi huu licha ya baadhi ya Wajumbe kutaka iundwe Kamati Teule ya Baraza kwa ajili ya kuuchunguza Mradi huu.

Mhe. Spika, Katika kazi zake za kawaida za kufuatilia utekelezaji wa kazi za wizara zilizo chini yake, zilizo fanyika mwezi wa Septemba, 2013 Kamati ilipata fursa ya kufuatilia Mradi huu kwa kupata taarifa ya utekelezaji wa

mradi huu na kutembelea kituo cha mitambo (*Data Centre*) kilichopo Mazizini mnamo tarehe 17/9/2013. Aidha, katika kazi kama hizo za kawaida zililzofanyika mwezi wa Novemba, 2013 Kamati ilipata nafasi ya kupewa taarifa fupi kuhusu utekelezaji wa mradi huo kwa Pemba tarehe 27/11/2013.

Mhe. Spika**,** pamoja na kupata taarifa ya mradi huu kama inayoonekana katika Ripoti ya Kamati, Kamati ilielezwa na kubaini changamoto mbali mbali kama ifuatavyo:-

i. Mradi unaonekana kuwa ni mpya na mgeni kutekelezwa hapa nchini jambo ambalo linaonekana kuwa ni sababu inayoonekana kupelekea kutokuwepo kwa uhakika wa kujua makisio halisi ambayo yangehitajika katika utekelezaji wa mradi huu.

ii. Ukubwa wa Mradi na Ufinyu wa muda wa kazi za Kamati ulitoa changamoto kubwa kwa Kamati kuweza kuuchunguza ipasavyo mradi huu ikizingatiwa kuwa Kamati pia ilihitaji kufuatilia utekelezaji wa kazi za taasisi mbali mbali za wizara ambazo inazisimamia.

iii. Kuchelewa kupatikana kwa manufaa ya mradi. Mradi ulizinduliwa rasmi mwezi Januari mwaka 2013 baada ya kukamilika kuwekwa Mkongo na vifaa katika kituo cha mtandao *"Data Centre"*. Ambapo hadi sasa ni taasisi nne tu zilizotajwa ambazo tayari zinanufaika na mtandao huo. Aidha, hadi sasa bado hakujawa na mauzo ya uwezo wa ziada kwa matumizi binafsi na hivyo, Mkongo kutochangia mapato ya serikali.

iv. Ofisi ya Afisa Mdhamin Wizara ya Fedha, Pemba kutoshirikishwa katika miradi inayotekelezwa Pemba ambayo inasimamiwa na Wizara ya Fedha na hivyo, kukosa taarifa zinazohusiana na miradi hiyo. Changamoto hii iliibua usumbufu wakati Kamati ilipotaka kufuatilia Mradi huu kwa upande wa Pemba ikiwemo baadhi ya maeneo ya utekelezaji wa mradi huu.

v. Kukatwa kwa waya wa mkonga wa Taifa. Maeneo mengi ya Unguja na Pemba sehemu ambayo umepita Mkonga wa Taifa umeharibiwa na kukatwa mara kadhaa licha ya kuwepo alama *stone mark beacon* zinazoonesha sehemu ulimopita mkonga huo. Miongoni mwa sababu zinazochangia kuwepo kwa tatizo hili la kukatwa kwa waya wa mkonga ni kutozikwa kwa kina kirefu kwa mkonga wenyewe.

vi. Uelewa mdogo wa umuhimu wa matumizi ya mkonga. Elimu kwa umma bado ni ndogo juu ya suala zima la Mkonga, ulimopita, umuhimu wake na athari zitakazopatikana pale patakapoharibiwa miundombinu ya mkonga. Aidha, walengwa wa mtandao wakiwemo wanajamii hawana elimu ya kutosha juu ya matumizi ya mtandao.

vii. Kamati imebaini changamoto inayoelekea kuikabili serikali juu ya hatma ya baadhi ya majengo yaliyokodiwa na serikali ambayo yatahitaji kupitishwa mitambo hiyo na namna hali itavyokuwa iwapo mikataba ya kukodishwa majengo hayo itaposita au kumalizika wakati mitambo hiyo itapokuwa imeshafungwa.

Mhe. Spika, kutokana na yote hayo Kamati inapendekeza yafuatayo:

1) Kwa kuwa Mradi *E-Government* ni mgeni na umetumia miundombinu ya kisasa, na kwa kuwa mradi huu ni mpana sana ambapo utekelezaji wake unahusisha vipengele na sekta nyingi, na kwa kuwa Mkonga umeshakabidhiwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na uratibu wa *E-Government* upo kwa Wizara ya Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora, na kwa kuwa Kamati za Kisekta hazina muda wa kutosha kufuatilia kazi maalum na kubwa kama hii wakati zinatakiwa pia kufuatilia utekelezaji wa kazi za taasisi nyengine mbali mbali zinazozisimamia, Kamati inaona ni vyema kwa Baraza kuunda Kamati maalum ya Baraza ambayo itapewa muda na fedha za kutosha kuweza kuuchunguza Mradi huu pamoja na kuipatia usaidizi wa mtaalam wa teknolojia ya kisasa inayohusiana na miundombinu ya Mradi huu ili kuweza kuuchunguza kwa kina zaidi Mradi huu.

2) Elimu ya kutosha inahitajika kutolewa kwa wafanyakazi na wananchi mbali mbali kuhusu masuala ya *E-Government* pamoja na uhifadhi wa mkonga ili kujua matumizi halisi ya mtandao wenyewe, thamani yake na athari zake pindi utapoharibika.

3) Maandalizi ya kutosha yanahitajika kufanywa kwa taasisi za serikali ambazo zinatarajiwa kuunganishwa na mkonga ili kupata vyumba vya mitambo (*Server room*) vinavyokidhi vigezo.

4) Serikali ianze kufikiria namna itakavyo chukua hatua muafaka kuhusu hatma ya kuunganisha mtandao wa *E-Government* katika majengo ambayo serikali imeyakodi kwa ajili ya shughuli zake.

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ina jukumu la kusimamia masuala ya biashara na maendeleo ya viwanda nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunakuwa na masoko ya uhakika ya bidhaa zetu ndani na nje ya nchi yetu.

Mhe. Spika, majukumu haya sio madogo, ni makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa ukizingatia kuwa sekta hii ya biashara na viwanda ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya uchumi popote pale duniani.

IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO

Mhe. Spika, Idara hii ina dhamana ya kusimamia masuala ya biashara na kukuza masoko. Katika kutekeleza wajibu wake, Idara hii pia ina wajibu wa kuzitafutia masoko endelevu ya ndani na nje bidhaa zinazozalishwa nchini na kuitangaza Zanzibar katika masoko ya ndani na nje.

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar kwa asilimia kubwa unategemea sekta hii ya biashara, Hivyo, ni jukumu la Wizara hii kusimamia masuala ya biashara ili kukuza uchumi sambamba na kutafuta masoko ya uhakika iwe ya ndani au nje ya nchi yetu.

Mhe. Spika, suala la kuwa na masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa ni muhimu sana, kwani inaonekana kuwa changamoto kubwa inayowakabili wajasiriamali wetu ni ukosefu wa mitaji ya kutosha pamoja na masuala ya masoko ya uhakika kwa bidhaa wanazozalisha.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wajasiriamali hao ili waweze kufikia malengo waliyokusudia.

IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UKUZAJI UJASIRIAMALI

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Viwanda ina wajibu wa kuimarisha Sekta ya Viwanda kwa kutekeleza majukumu mbali mbali yakiwemo ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda. Uanzishwaji wa

Idara hii unaenda sambamba na umuhimu wa kuwa na viwanda ili kukuza uchumi wa nchi yetu. Ni dhahiri kuwa, nchi zilizoendelea zimeweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo kutokana na kutia nguvu katika sekta ya viwanda. Hivyo basi, ni vyema kwa serikali kuipa msukumo unaostahiki sekta hii ili kukuza kasi ya maendeleo ya uchumi hapa nchini.

Pamoja na utendaji mzuri wa kazi katika Idara hii, bado ukosefu wa wafanyakazi wenye sifa limekuwa ni tatizo kubwa katika kufikia kikamilifu maazimio na malengo ya Idara.

Mhe. Spika, Kamati imesikitishwa sana kuona kuwa, hadi wakati ilipoitembelea Wizara hii mwezi Januari, 2014 bado haijalifanyia ukarabati jengo la Saateni lililokusudiwa kufanywa kituo cha wajasiriamali kwa kuwa serikali imeshindwa kuikabidhi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko jengo hilo. Na hivyo, kuifanya kazi iliyokusudiwa ya kuanzisha kituo cha kufundishia na kuwaendeleza wajariamali waliopo hapa nchini kushindwa kufanyika**.**

KIWANDA CHA SUKARI MAHONDA

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilifanya ziara katika Kiwanda cha Sukari na shamba la miwa la kiwanda hicho Mahonda mwezi Januari, 2014 na kujionea hali halisi ya ukarabati mkubwa uliokuwa ukifanyika kiwandani hapo. Kamati ilifurahishwa na hatua kubwa ya kimaendeleo iliyofikiwa na kiwanda hicho. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto kadhaa zinazokikabili kiwanda hicho zikiwemo za kutokukabidhiwa kwa uongozi wa kiwanda hicho nyumba 150 za kiwanda hicho ambazo zimekuwa zikikaliwa na wananchi. Aidha, Kamati ilibaini kujitokeza kwa uharibifu katika shamba la miwa unaosadikiwa kufanywa na wananchi wa maeneo hayo kwa makusudi.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba serikali kukabidhi nyumba 150 za Kiwanda cha Sukari Mahonda kwa uongozi wa kiwanda hicho ili waweze kuzitumia kwa ajili ya wafanyakazi wake na kutimiza lengo lililokusudiwa la kujengwa kwa nyumba hizo. Pia, Kamati inatoa wito kwa taasisi zinazohusika pamoja na wananchi kutoa mashirikiano ya dhati kwa uongozi wa Kiwanda cha Sukari katika kudhibiti vitendo vya kukihujumu kiwanda hicho vikiwemo uharibifu na wizi wa miwa kwa vile manufaa ya kiwanda hicho zikiwemo ajira ni za wananchi wenyewe.

TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR *(ZBS)*

Mhe. Spika, Taasisi ya Viwango Zanzibar imeanzishwa kwa lengo la kuweka viwango na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma hapa nchini. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipata nafasi ya kutembelea taasisi hiyo pamoja na ofisi zake ikiwemo eneo lililotengwa kwa ajili ya maabara.

Mhe. Spika, kasi ya uendelezaji wa taasisi hii bado hauridhishi kutokana na ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi ambavyo ndio muhimili wa maendeleo ya taasisi hiyo.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaishauri Wizara husika kufanya jitihada za kutafuta wataalamu wa fani zinazohitajika katika Taasisi ya Viwango Zanzibar ili taasisi hiyo iweze kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi. Pia, Kamati inaiomba serikali kujizatiti kikamilifu kwa kuiingizia fedha za kutosha taasisi hii ili malengo ya kuanzishwa kwa taasisi hii yaweze kufanikiwa, ikiwemo kuanzisha kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa bidhaa mbali mbali.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA *(ZSTC)*

Mhe. Spika, Kamati ilipata taarifa kuhusu mageuzi ya Shirika ambapo hatua mbali mbali zilichukuliwa katika mageuzi hayo zikiwemo kutayarisha Mpango Kazi, Muundo wa Utumishi, Kanuni za Utumishi na Kanuni za Fedha, Uanzishwaji wa Tovuti ya Shirika, Kupunguzwa Wafanyakazi wa Shirika, Uajiri wa Watumishi Wapya, Ununuzi wa Mizani, Ununuzi wa Magari, Uuzaji wa Bidhaa katika Soko la Ndani na Ujenzi wa Vituo vya Ununuzi wa Karafuu.

Aidha, Kamati ilifanya vikao na viongozi wa Shirika na kutembelea shamba la Mtakata Chake Chake, baadhi ya vituo vya ununuzi wa karafuu na ghala za karafuu pamoja na kuzungumza na wachukuzi katika ghala ya karafuu Mkoani, Pemba.

Mhe. Spika, Kamati imebaini changamoto kadhaa zinazolikabili Shirika hilo ikiwemo tabia ya watendaji wa Shirika kuzichukua karafuu kidogo zinazobakia bila ya ridhaa ya muuzaji baada ya kupimwa. Pia, Kamati imegundua kuwa biashara ya magendo ya karafuu bado ni tatizo ambapo maeneo ya vijijini kunaonekana kushamiri kwa biashara hiyo. Aidha, magendo ya karafuu na kujitokeza kwa aina mpya ya wizi wa karafuu kwa kukatwa matawi ya mkarafuu yaliyozaa karafuu kwa wingi, ni miongoni mwa changamoto nyengine inayoikabili biashara ya karafuu.

Mhe. Spika, Kamati inaona ipo haja kubwa kwa Shirika kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza ununuzi wa mizani za kisasa za upimaji wa karafuu ili kuondoa malalamiko mbali mbali yanayohusiana na upimaji wa karafuu. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama izidishe juhudi za kudhibiti magendo ya karafuu kwa kuwa karibu zaidi na wanachi ili kuweza kutambua mbinu mbali mbali zinazotumiwa na wajanja wanaosafirisha karafuu kwa njia za magendo na kuchukua hatua zinazofaa.

Vile vile, Kamati inalitaka Shirika kuhakikisha kuwa karafuu kidogo zinazobakia baada ya kupimwa zinarudishwa kwa wauzaji wenyewe na iwapo zitahitajika na Shirika, zilipiwe au zichukuliwe na Shirika baada ya kupatikana ridhaa kutoka kwa wauzaji wenyewe.

Mhe. Spika, hapa tumebaini kwamba wakulima wanapokwenda kuuza karafuu, karafuu zinazobakia kama robo zile zinakuwa hazilipiwi zinachanganywa. Kwa hivyo, kutokana na thamani ya karafuu kiwango kile ni kikubwa na wananchi tunakuwa tunawadhulumu. Kwa hivyo, tunaliomba sana Shirika karafuu zinazobakia japo kidogo hazitimii kilo ama warejeshewe wenyewe au waulizwe kwa ridhaa zao. Badala ya karafuu zile kukusanywa na kuchanganywa na nyengine.

Mhe. Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea ofisi za Shirika hili zilizopo Dar-es-Salaam na kupata taarifa ya utekelezaji wa kazi za ofisi hiyo kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2013.

Mhe. Spika, Kamati inaona kuwa bado kuna umuhimu wa ofisi hii kuendelea kuwepo huko Dar-es-Salaam kwa kuwa ofisi hii itaweza kutangaza bidhaa za Shirika na Zanzibar katika Soko la Afrika Mashariki na kwengineko. Aidha, Kamati inaona ipo haja kubwa kwa Shirika kufanya utafiti wa kina juu ya namna ya kituo hicho kitakavyoendelezwa. Kamati pia inaiomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar iongeze nguvu katika jitihada zake ilizoanza kuzifanya za kutaka jengo linalotumiwa na *ZSTC* Dar-es-Saalam liuziwe Shirika hilo.

HITIMISHO

Kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza kwa dhati Wizara hizo tatu zinazosimamiwa na Kamati hii pamoja na taasisi zao kwa juhudi wanazochukua katika utekelezaji wa kazi zao. Kamati pia inapenda kutoa shukrani tena kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii pamoja na wale wote waliofanikisha kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa usikilizaji wao mzuri wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii. Kamati inatoa wito kwa serikali kutekeleza kwa vitendo yale yote yaliyoagizwa na kushauriwa na Kamati ili kuongeza ufanisi katika Wizara hizo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kwa uwasilishaji huo mzuri wa ripoti ya Kamati yako. Sasa Waheshimiwa Wajumbe basi tuzijadili ripoti hizo za utekelezaji pamoja na ripoti hii ya Kamati. Nimkaribishe basi kama kawaida Mhe. Makama Mshimba Mbarouk, wakati Mhe. Asha Bakari Makame, anajitayarisha. Mhe. Makama Mshimba Mbarouk, tunasisitiza kwamba kazi hii nayo inakusudiwa kumalizika leo. Kwa hiyo, twende kwenye *point* moja kwa moja. pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine watakaokuwa na nia ya kuchangia tupa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, basi na mimi nakupa shukrani kidogo angalau kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia asubuhi hii.

Mhe. Spika, mimi kwanza namuunga mkono Mwenyekiti wa Kamati kusema kuwa kuundwe Kamati Teule kwa kuweza kuchunguza suala hilo. Hilo moja naunga mkono kabisa sina wasiwasi nalo.

Lakini Mhe. Spika, naomba nitoe ushauri wangu kwa Wizara ya Fedha. Mhe. Spika, hapa ndio kwenye fedha. Huwa kuna vilio vya mishahara. Ushauri wangu wa bure naomba nimpe Mhe. Waziri, kuwa serikali ikipunguza kodi mara nyingi sana inakuwa haipati hasara. Kwa hiyo, naomba iangalie katika maeneo hayo ya kupunguza kodi ili watu waweze mshahara kuona kile walichokipata kiwe kinastahiki. Kwa sababu Mhe. Spika, leo mtu akiongezewa mshahara kesho vyakula vinapanda, sasa utakuta ile hali halisi akija hapa hajafanya uchunguzi kwa kina kabisa. Kila siku tutasema mishahara haitoshi, lakini kumbe haitoshi kutokana na hali halisi tuliyokuwa nayo ya kupanda bei ya vyakula.

Sasa hapa serikali kama itaweza kudhibiti, basi naamini hicho hicho tunachopewa cha shilingi laki mbili au laki moja utaona kinatosheleza kutokana na hali. Naomba sana Mhe. Spika, hilo Mhe. Waziri, alifikirie kwa kina kabisa akae na wataalamu.

Lakini Mhe. Spika, tusitafute mshauri mwelekezi tunao wenyewe. Sasa mimi naomba washauri waelekezi wa kizalendo tupewe haki ya kuweza na sisi tuitwe katika Mawizara kusaidia. Kwa sababu ni ushauri wa bure tu kwangu mimi. Ninaomba sana hili suala liangaliwe kwa kina kabisa tatizo la

mishahara tukifanya hivyo litaondoka. Tufanye hii *practical* wenyewe mara moja Mheshimiwa.

Lakini Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa pili wa hiyo hiyo *TRA.* Utaratibu wa kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuimarisha na uendaji salama. Mhe. Spika, kwanza hapa nimpe pongezi sana Mhe. Waziri, lakini namuomba sana ushauri wangu hapa awe na *special team* ya kwenda kuangalia masuala kama haya. Jana ulitaja vizuri jinsi gani ulivyo-*improve* kukusanya kodi utapata mara tatu zaidi.

Lakini kutoka mwenyewe tu si kwamba uende ukakague inakuwa haiwezekani. Iweke *special team* kazi yao iwe hiyo tu na ikupe ripoti uone tumefikia hivi. Mhe. Spika, hilo suala litatusaidia hapa. Hajaingia mtaalamu wa kizungu hapa nimeingia mimi. Mhe. Spika, naomba na ule ushauri wangu unisikilize kwa makini sana na kuweza kuutekeleza.

Lakini Mhe. Spika, ndio yale niliyoyasema kuwa leo tunaweka kodi ya juu kabisa kwa shilingi ishirini elfu, sasa ona hatari yake inakuwa kama hivi. Mhe. Spika, tukiweka kwa kiwango kile kile cha kumi na tano mimi sioni kama tutakuwa na hasara kubwa, lakini nitakuonesha njia ya kupata fedha si ya kuongeza fedha kodi.

Mhe. Spika, njia moja tu, na kama tutakuwa tunafanya hivyo, basi nafikiri *alhamdulillah.* Kwanza, hiyo huko *ZIPA* wanakotengeneza Fumba kama atakuweza tutampa mashirikiano makubwa sana litaondoka lile suala la ongezeko ya kodi ya watu wa chini. Tumpe nguvu, tumpe shughuli za kufanya, tumpelekee kule masuala ya umeme, njia, na kila kitu, masuala haya yataondokana. Lakini kila siku ndio itakuwa hivi hivi tutapandisha makodi mpaka wananchi watatukimbia. Maana yake sasa hivi wafanyabiashara wanatukimbia, wananchi sasa nao watakimbia nchini hapa watakwenda kuwekeza kwengine.

Kwa hiyo, ushauri wangu naomba hili suala kuwa tupewe nguvu sehemu ambayo tunaweza tukapata kodi kubwa. Kwa mfano tuweke sheria ambayo itakayoweza, tutakuwa na meno, sasa hivi ya kuita viwanda vikubwa. Mhe. Spika, tukiwa navyo hivyo, tutasema *alhamdulillah* utajiri. Hilo ninalokwambia wazi, tukifanya hivyo Mwenyezi Mungu atatujaalia. Lakini Mhe. Spika, hapa ndio pa kusema kuwa jana nilijaribu kumwambia yule mama yangu pale, lakini hakuweza kunijibu vizuri na hili suala hakunijibu.

Mheshimiwa sasa wewe uwaonee huruma kinamama wawekee benki, hili jamani suala hakuna tatizo. Juzi nilikaa nyumbani tulisikia hili tangazo kuwa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, kafanya kitu kama hicho. Kumbe na yeye

anasikiliza Baraza Mshimba kasema nini ana-*note* kule. Kishaiweka hiyo kwa sababu ndio tulisema hapa sisi mara chungu nzima na wewe Mhe. Waziri, weka mfano mkubwa huo, historia hiyo itakuwa kwako. Hebu wawekee kinamama benki yao na wao tutakuwa tunawahangaisha tu, tuwe tunaitwa maskini kumbe njia ndogo tu. Mhe. Waziri, ninakuamini Kamanda wangu wewe utafanya hicho kitu na Mungu akusaidie.

Lakini Mhe. Spika, jengine niseme suala la hawa wawekezaji. Mhe. Waziri, amesema kuna ugomvi wa wananchi na wawekezaji na nakubaliana nalo hilo. Lakini tumekosea sana na hiyo tuikubali. Kwa sababu wawekezaji wanapotaka kuwapa maeneo karibu na wananchi ilipaswa serikali ianze kuwaelimisha wananchi nini madhumuni ya kufanya jambo hili. Ilipaswa wananchi kuwabembeleza na kuwaondoa pale au kuwatafutia jambo jengine, nyinyi mtapata faida yake. Hili mimi nakubali serikali ikubali kosa hilo wala si vibaya, si dhambi kabisa kukubali kosa, ndio unakuwa mtu mzuri kabisa, ukikubali kukosolewa, basi na wewe unaonekana mtu mzuri sana. Hili suala Mhe. Spika, tumelikosea sana.

Lakini vile vile, Mhe. Spika, mimi naomba sana hii *ZIPA* na wao waweze kuwa karibu sana na wananchi. Kwa sababu kuna matatizo ya mwekezaji na yeye kunyang'anywa eneo na hili nililisema sana mimi juzi kuwa tuwekewe Mahakama. Lakini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kasema kuwa ana mbinu mbadala, kaogopa ile kusema kunikubalia *direct* kama hichi kitu nitafanya.

Lakini katumia njia ambayo ni muafaka akasema kuwa tutawaweka majaji maalum wa kuweza kuzisikiliza kesi zile tu. Sasa itakuwa si kichekesho, si ndio yale yale Mahakama, ni Mahakama kuitaja, lakini kageuza mbinu tu. Lakini nakubaliana nalo pamoja na hilo tulifanyeni, tuwawekee hawa watu kutokana na hali halisi ilivyo. Jamani hili ni suala ambalo lina masikitiko makubwa sana.

Mhe. Spika, hapa niondoke kwa Wizara yangu ya Fedha japo nina mengi na muda wenyewe umenambia ni mdogo leo na kazi tunayo nzito, mimi sina tatizo kubwa. Lakini hili jengine Mhe. Spika, sasa hivi tuna ushindani wa mambo ya kuja watalii nchini kwetu. Tuangalie katika maeneo viza, hebu tujaribu tuangalie kwa jirani anaweka ngapi. Na je, hiyo bei aliyoweka yeye anapata wangapi. Mimi naomba sana hili jamani tusione haya kuangalia majirani jamani, tumo katika mashindano ya kibiashara. Naomba sana Mhe. Waziri, aangalie hayo, ikiwa mwenzetu kaweka dola mbili, sisi tuweke dola moja na nusu sio mbaya kwa sababu sisi tunapokea. Huuzi kitu hapa kama utakula hasara Mheshimiwa wangu, lakini isipokuwa hii wanaona tabu sana.

Mhe. Spika, hii ndio iliyojaa hivyo, lakini kwenda wuuuuuu! haiwezekani. Naomba sana hebu tulifikirie jamani hili tufanye kidogo kidogo tutizame tija yake itakavyokuwa. Mhe. Spika, naomba hilo nimkabidhi Mhe. Waziri, anisikilize naomba aje kunipa jibu kwa fasaha kabisa ili kuweza kufanikisha suala ambalo tulilolikusudia katika mambo yetu haya.

Mhe. Spika, ukurasa wa 7 amesema kuwa anafanya mawasiliano kuona jinsi gani kwa sababu anataka kujua huyu anatupa kweli viwango vizuri au vibaya tuweze kwenda kwengine tunakopata viwango vizuri vya mafuta. Nalo hili ni suala zuri. Namuomba sana Mhe. Waziri, ushauri wake nautilia maanani nakubaliana na yeye asilimia mia kwa mia.

Lakini Mhe. Spika, niingie katika suala la kamati hapa ya utekelezaji masoko. Mhe. Spika, juzi tu katoka kutamba hapa Mhe. Waziri, pamoja na Naibu wake, Katibu wake, Wakurugenzi na Wanasheria wao, mimi nakubaliana nao. Lakini naanza kutoa tahadhari kubwa tumeambiwa karafuu sasa tumeshazipa sheria, lakini eka zinauzwa. Wacha kuwa eka zinauzwa tu, kuna eka watu wanapewa nyingi, mtu anachukua eka 29.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, tufanye marekebisho. Mhe. Wazir, nakushukuru sana hapo naona umeshaanza ku-*note* sawasawa endelea hivyo hivyo. Eka zinauzwa Mhe. Waziri, njoo jimboni kwangu tayari watu wanaziuza eka huku. Wanyang'anywe kwa nini wauze eka? Tena basi ananyang'anywa mtu anakwenda kuuziwa mtu. Mhe. Spika, hilo suala mimi limeniuma sana sikufichi, na sisemi ni utajiri huo Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko anatuletea. Maana yake ni utajiri sasa si mchezo. Kwa sababu leo mtu unaambiwa wewe mkulima unasaidiwa kwa kila hali uupande ule mkarafuu si kitu cha mchezo, kabisa mimi sijapata kuona ulimwengu huu, lazima nimsifu.

Mhe. Spika, mimi namuomba kwa hili tu Mhe. Waziri, ajitahidi kutuletea viwanda, ashirikiane na Wizara ya Fedha wakae, wapange na washauri, waelekezi wapo wa Kiswahili, wawaite tuone jinsi gani ya kuweza kufanikisha. Lakini sheria ile moja bado hawajaifanyia kazi ya chakula, bado tunaumia kwenye chakula. Mmetuletea sheria nzuri sana, lakini bado tunaumia, tusiwaogope wafanyabiashara jamani wanawamaliza watu kuleta vitu ambavyo havifai kuliwa na binadamu. Jamani mpaka lini sheria imezungumzia vizuri, lakini utekelezaji wake sitaki nikutieni dosari, lakini itafika siku nitakutieni dosari kwa sababu hamjajiandaa vizuri. Mmetunga sheria, lakini maandalizi yake hamjaandaa. Kamateni watu bwana hao wanyang'anyeni vyakula vitupeni baharini huko. Itakuwaje kwa kila siku wawe ni watu wale wale tu.

Lakini Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri, katika hichi kiambatanisho cha pili nimeona hapa namba 4 kuwasaidia wazalishaji wadogo wadogo mitaji kukuza na wakiwemo jamaa zangu wa Ulezi Kazi wa Fujoni. Mhe. Waziri, nakupongezeni sana, vikundi hivi mmevipa sifa kubwa mpaka Kenya wanakwenda, mpaka wapi. Mimi nakusifuni sana, tena endelezeni na kuwaongezea tija kuwasaidia. Mhe. Spika, hapa mimi sina tatizo nawaunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Spika, nikimalizia na hii ya misitu. Mhe. Spika, niwapongeze sana kilimo ni uti wa mgongo, lakini kilimo kama hatutashirikiana na Wizara ya Fedha hamna ulilolifanya hata siku moja, utabakia na jina la kilimo tu. Kivipi basi. Mimi nashangaa sana sijui kwa nini. Jamani nataka nikwambieni kitu kimoja nilicho-*experience* ndani ya moyo wangu, mimi mnavyoniona nina watu *special* nakwenda kuchukua mawazo, kama leo hii nikishahutubia, nakwenda kufanya *correction* vipi nimekwenda vizuri au vibaya.

Ndio sioni tabu wengine ninao humu humu ndani na wengine ninao nje. Kwa sababu nataka niweke katika *set* nzuri, nieleze jambo la msingi. Sasa na nyinyi Mawaziri msione tabu, kuna vitu ambavyo vinaingiliana kimawazo, kiutendaji hili lazima tulione. Wizara ya Fedha ni kiungo kwa Wizara nyengine zilizobakia. Lakini sijui niulize hapa kama angalau siku moja mlimwendea Waziri wa Fedha. Iko siku moja angalau mtu kenda hapa, haiwezekani Mhe. Spika, hakuna hicho kitu. Ni kitendawili Mhe. Spika, sasa hivyo sivyo Mawaziri wangu. Nawaombeni sana nendeni kule yule ana fedha, ana mambo mengi, lakini ukingoja leo wewe akupe kwenye bajeti tu ndio utakuja kumsulubisha hapa bure maskini ya Mungu, kumbe yeye kakaa mlango wazi kule Waziri wangu wa Fedha, shemegi yangu.

Sasa na huo ni ushauri wangu wa bure, nawaombeni nikupeni kabisa hautaki mwekezaji kutoka nje wala nini. Nendeni kule mkapange mambo ya *strategy* ya nchi yetu iinuke kwa uchumi. Yule ndio Mwenyekiti wa Uchumi wa Umoja wa Kitaifa, kama kanyang'anywa cheo hicho, basi mmemnyang'anya kwa kumuonea, kama anacho haki yake, nendeni kule tuone jinsi gani ya maendeleo.

Mhe. Spika, mimi nimefurahi sana nataka niulize swali, naomba Mhe. Waziri unijibu. Katika bonde letu kule la Pangeni/Kilombero tulipata wafadhili wa kutuchimbia mitaro kwa kupata kumwagilia maji mipunga yetu. Mhe. Spika, nalo hilo mpaka leo naona kimya, sijui tumefikia wapi. Naomba unisaidie hili suala nililisema sana katika bajeti, lakini sikuliona utekelezaji wake ukoje. Mimi naomba hili Mheshimiwa anisaidie kwa sababu tukifanya hivyo, umaskini Jimbo la Kitope baibai kwa ukulima wa mpunga. Mhe. Spika, njia

nyengine yoyote kwa kusubiri mvua vyanzo vyenyewe vinakatwa miti kila leo. Na nilisema Sheria ya Misitu ifanyiwe marekebisho.

Mimi nimshukuru sana Mkurugenzi wangu wa Misitu kuwa anajitahidi sana, lakini sisi ndio tunakwenda kumharibu kama ni viongozi hilo tuseme wazi. Kwa sababu leo mwananchi anakamatwa, mimi inabidi niende sina njia nataka kura eti pale, kumbe nakwenda kumharibu yeye kwa mujibu wa sheria. Na yeye atanisaidia kwa shingo upande halafu leo mapato yatapatikana wapi. Kwa sababu wewe sheria ukishaweza kukamatwa inabidi unatakiwa ulipe faini na faini ni moja katika mapato ambayo tuliyokusudia kuyapata.

Ninaomba sana Mhe. Spika, hili suala la misitu sheria iwekwe wazi na iwe kali sana ili kuweza kumsaidia Mkurugenzi wangu. Anajitahidi, lakini msitu unateketea, umebakia Kiwengwa tu kwa Unguja hii na Jozani, tukiuachia huo unakwenda na maji.

Mhe. Spika, nishukuru sana wakati huu kiasi tumeanza kulima mapema baadhi ya mambo. Nashukuru sana kwa hilo wamejitahidi watu wa kilimo. Lakini tatizo linakuja watu wanapiga kelele sana dawa za magugu. Wanasema dawa za magugu zinauzwa kidogo halafu baadae utasikia zimeuzwa Kenya, sijui zimeuzwa wapi. Hebu hili tuangalie utaratibu mara hii tugeuze, tuweke utaratibu ambao uliokuwa *strong* na tutaweza kuwa na *security* nzuri kwa wakulima kuweza kupata dawa kwa wakati.

Mhe. Spika, kwa kuendelea ningeomba sana Kilimo kibadilike kwa wakulima, tuache ofisi twende kwenye mabonde yetu tuwa-o*rganize,* hivi vikundi vinavyo-*organize* vizuri, lakini michango yake tuipe fursa njia ya kuweza kwenda benki. Kwa sababu wakipata mikopo benki, ndio mwananchi ataweza kulima. Hilo tusidanganyane hakuna *plan* hiyo, mtasema kila siku hampati. Limeni, limeni, limeni nini wakati hana kitu ndani yake. Namuomba sana Mhe. Waziri, hilo ili kuweza kusaidia katika ukulima, lakini naona serikali haijawa *serious* katika jambo hili. Kwa sababu lazima serikali tuiambie ili waharakishe kuwasaidia wananchi. Huko mbele ya haki Mheshimiwa na umetupa msahafu hapa.

Mhe. Spika, nimalizie sasa kuwa wanajitahidi sana kuweka madarasa ya wakulima. Tumesema humu, lakini hakuna, jimbo langu kulikuwepo madarasa mengi tu, naona sasa hivi yale yame-*disappear* kwa sababu nafikiri mfuko hakuna wa kufanya hivyo. Mhe. Spika, madarasa yale ni mazuri sana, ni ajabu kuwa tunaagiza kitu kizuri halafu baadae kinakuwa tunaki-*delay,* sijui kwa nini. Naomba sana Mhe. Spika, darasa hili bwana linamuokoa mkulima kwa kujua upandaji wa aina gani na sasa hivi nipande nini na sasa hivi niache kupanda nini. Hili tulihamasishe, tusiseme kwenye *paper*,

twendeni *field*, wale walimu wetu hebu waambieni sasa hivi wakupeni ripoti za ukamilifu.

Lakini la mwisho, kuwa agizo namba nne, Wizara ya Fedha kuharakisha kutia saini mkataba wa maelewano wa *MOU*. Naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, wape hawa wamalizie ili tujisikie raha Mheshimiwa. Mimi nakuamini wewe ulivyokuwa mchezaji mzuri hapo, utawamalizia hawa, kiungo mzuri wa ku-*connect* na nini. Mhe. Waziri wangu, shemegi yangu, naomba sana hebu weka hiyo uwasaidie. Nikisema leo hii hata mchana ukija kujibu, sema nimeshamaliza hii kazi, tayari mambo yote wameshamalizia ili na wao wajisikie. Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono ripoti ya Mwenyekiti asilimia mia kwa mia.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndie aliyetuwezesha siku hii ya leo kufika katika Baraza lako tukufu na kuchangia mambo mbali mbali ya taifa letu. Pia na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa kamati pamoja na wenzake wote wa kamati kwa jinsi walivyoeleza, lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Fedha pia na yeye alivyoeleza kinagaunaga ili kuona hali halisi.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati mimi niende moja kwa moja. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, wakae pamoja wapitie uwanja wa ndege kwa jumla, halafu wapitie bandarini pia kwa jumla, waangalie ni matatizo yepi ambayo yanawakwaza wananchi, lakini pia yanaikwaza serikali yetu. Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ninarudia tena, wakae pamoja wakubaliane, wautembelee uwanja wa ndege wote pamoja na bandari kwa jumla, ili waoanishe mapato pamoja na mambo mbali mbali ambayo inaikwaza serikali kwa kukusanya mapato. Hilo moja na mimi nitakwenda moja kwa moja kwenye *point*.

Lakini jengine niseme tu kwamba tulipitisha bajeti hapa Mhe. Spika, lakini bajeti hii mbona kipindi hichi haikufanya kazi ipasavyo. Ninamuomba Mhe. Waziri aje atueleze kwa sababu tulipoingia katika kamati kutembelea wizara husika, nyengine miezi mitatu haijapata shilingi ya kutumia na tumejionea sisi wenyewe, huenda mpaka mafuta wahangaike wakope tunachelewa kuanza kazi. Hilo ninamuomba Mhe. Waziri, alizingatie kwa hichi kipindi kifupi kilichobakia angalau mawizara yaweze kupatiwa makisio yao ya bajeti kama kawaida.

Nije katika kilimo Mhe. Spika. Mhe. Spika, tunasema kwamba Rais alihutubia akasema kwamba mapinduzi ya kilimo lakini mapinduzi yale ya

kilimo yalikuja kama mvua vuu! vuu! ilivyonyamaza yamenyamaza. Naiomba sana serikali kwamba tuelewe kwamba asilimia 70 ya taifa hili la Zanzibar basi ni wakulima. Kuna mambo makubwa tunapotembelea huko kwa sababu hii Wizara ya Uvuvi na Mifugo kidogo inawasiliana na Wizara ya Kilimo. Mhe. Spika, wizara zote takriban hatimiliki ni jambo gumu sana.

Naomba wizara husika ziwasiliane na wizara nyengine ambazo kila wizara inatakiwa hatimiliki ya sehemu ambayo nimepewa. Unaona kwamba unapotembelea Mhe. Spika, basi maeneo mengi ya mawizara yananyofolewa kidogo kidogo. Hata tukiangalia tunaona kwamba wizara husika kama imepewa eneo la kufanyia kazi, eneo lile halipo tena.

Naiomba sana serikali kwa sababu ni sisi wenyewe kwa wenyewe kuna tatizo gani ya kila wizara kupatiwa hatimiliki kwa pale ambapo watu wamepewa na serikali. Naiomba tena kipindi cha bajeti nitakuja kutoa shilingi na mimi, kama tumetoa maagizo ya Kamati kila sehemu ipatiwe hatimiliki na hazipatikani mara unaambiwa kuna hivi na vile, sielewi wakati sisi hapa tupo majirani. Kwa nini hakuwi na *one stop centre* na hili jambo hili tunalizungumza kila siku Mhe. Spika, kiwizara kuwe na *one stop centre* ya kufanyia mambo yetu ya kilimo, ya hatimiliki, ya utalii, ya vitega uchumi. Kwa nini hatufanyi suala hili, kuna ugumu gani? Tunafanya urasimu ambao kwa kweli hauleti tija. Hilo moja.

Lakini jengine Mhe. Spika, niseme tu kwamba naiomba serikali kupitia kwa Waziri wa Fedha tuanzishe Benki ya Kilimo. Benki ya Kilimo Mhe. Spika, inaweza ikasaidia wananchi wetu. Wenzetu Tanzania Bara wanayo Benki ya Kilimo na inasaidia mpaka watu wanakopa matrekta na vitu vyengine. Iwekwe Benki ya Kilimo kushughulikia wakulima tu kwa sababu asilimia 70 ya taifa letu hili la Zanzibar ni wakulima.

Nimuombe Mhe. Waziri na serikali kupitia kwake Mhe. Waziri benki hii itaweza kuwasaidia wakulima wetu kutokana na ile kwamba kwenda benki ukahangaishwa, kwenye vikundi unahangaishwa, kwenye uhamasishaji unahangaishwa, pesa yenyewe ukipewa ni shilingi laki mbili, laki mbili zifanye nini Mhe. Spika. Nimuombe sana akae atafakari na serikali tuhakikishe tuanzishe benki yetu ya kilimo.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda mimi niseme tu hebu Mhe. Waziri, aje anielimishe hii habari ya *ZANTEL*, mbona siku hizi ina matatizo pamoja na huu mkonga, mimi sizungumzii mkonga, wenzangu wameshazungumzia na mimi naona kwamba kuna haja ya kuundwa Kamati Teule kweli kuchunguza huu mkonga uliokuwa unatuletea matatizo, lakini mimi ninasema *ZANTEL* yenyewe hasa nije nipate maelezo ya kina, kuna nini, kulikoni? (*Makofi*).

Mara ukipiga simu saa nyengine unajisikia mwenyewe, maana yake ni tafrani tu, saa nyengine unaambiwa unayemtaka hapatikani, mwenzako anakwambia nimekupigia simu leo sijui mara ngapi simu hunijibu. Hebu kulikoni kuna nini Mhe. Waziri? Tupe matatizo ya *ZANTEL*, kwa sababu *ZANTEL* chimbuko lake ni Zanzibar. Sasa kuna nini na mimi ninaweza kusema wana wizi wa udoho udoho. Siku hizi ukitia shilingi elfu tano, hutumii hata siku moja shilingi elfu tano imekwisha, kuna nini? Kulikoni na sisi wamesajili kwetu sisi hawa. Naomba uje unipe maelezo ya kina kuna nini *ZANTEL* sasa hivi haijulikani Kusi wala Kaskazi? (*Makofi*).

Ninaiomba sana serikali na ninakuomba Mhe. Waziri wa Fedha, sisi ndio waanzilishi wa *ZANTEL*, Baraza hili Mhe. Spika. Ilipoanza tu *ZANTEL*, sisi tulileteawa fomu ndio watu wa mwanzo kununua *line* ya *ZANTEL*. Sasa kwa nini tunafanyiwa hivi Mhe.Spika?

Mimi nitakupa mfano Mhe. Spika, samahani nitachukua muda wako mdogo tu. Hivi karibuni sijui wanatia mule ukitaka kujiunga upate rahisi, elfu mbili na mia nane, elfu tatu na mia ngapi. Nimejiunga hiyo 3800, ninatizama naona pesa zangu zimeliwa dakika. Nikapiga simu wakati wameshasema kwamba ujiunge, maana yake wengine ni ma-*layman* Mhe. Spika, hatuwezi kujua mambo hayo. Nikapiga simu kuwauliza ilikuwaje jamani mbona pesa zangu zimekwisha na mimi mumeniambia nina elfu saba. Naona leo hata haijafika siku ya pili pesa zimekwisha, ilikuwaje. Aah! maana yake mama. Nikawaambia wizi wakubwa nyinyi! Wakaikata simu.

Sasa badala ya kunifahamisha mteja wakanipa maneno mazuri, matamu, wamekata simu. Mhe. Spika, hili Mhe. Waziri pamoja na yote lakini ninataka uje unipe maelezo ya kina ya *ZANTEL*. Si hivyo wakati wa bajeti waziri anayehusika na mambo haya na hayupo sasa hivi, yupo Naibu Waziri haki ya Mungu hapa hapatokalika. Kwa sababu kwa kweli sisi ndio waanzilishi wa *ZANTEL*,sasa ameshafanikiwa, ameshapata faida, sasa anatuletea bughudha ya *ZANTEL*. (*Makofi*).

Baada ya kusema hayo pamoja na yote lakini niseme na mimi ninaunga mkono hoja yote moja kwa moja. Tutoe indhari tu haya baadhi ya mambo ya kwamba kila siku "tuta". Jana nilisema hivyo hivyo matuta haya yatakuwa mengi. Maana matuta haya yakiwa mengi baadae mutatuchokesha kuyapanda haya matuta. (*Makofi*).

Baada ya kusema hayo, niseme ninaunga mkono tena, lakini ninasisitiza *ZANTEL*, tuje tupate ufafanuzi wa kina. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii nikazungumza machache sana ili kuokoa muda katika ripoti hii ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara pamoja na Fedha.

Mhe. Spika, na mimi ninaungana mkono na ripoti ya kamati pamoja na mapendekezo yote ambayo au maagizo yaliyotolewa kwa wizara. Na ninaamini Mhe. Spika, nilipokuwa nikiwasikiliza Mawaziri walipokuwa wakitoa ufafanuzi wa maagizo wa ripoti iliyopita, kwa kweli nimepata faraja kubwa sana kwamba sasa hivi kumbe hizi ripoti zetu zinasaidia sana. (*Makofi*).

Kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri walipokuwa wakijibu walikuwa wanajibu maagizo ya kamati na utekelezaji wake. Kwa kweli wamejitahidi sana katika kutekeleza yale maagizo na ushauri wa kamati. Kwa hivyo naomba Mhe. Spika, Waheshimiwa Waziri waendelee na moyo huu, kwa kweli na sisi tutajitahidi kwamba kila inapowezekana kutafuta zile hoja za msingi kuwapa ili waweze kuwatekelezea wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi ninataka nianze moja kwa moja kwa swahibu wangu Wizara ya Fedha. Mhe. Spika, mimi bado nina kilio changu ambacho Mhe. Waziri katika bajeti iliyopita aliahidi kwamba ndani ya kipindi kifupi ataweza kuyashughulikia masuala ambayo niliyoyaeleza kipindi kirefu.

Kwanza kuna huyu mwekezaji Bwana Magembe ambaye wananchi wa kule Michamvi ambao kwa kweli walikubaliana kwa maandishi kupitia kwa Sheha, baadae ilipokuwa suala halikutekelezwa wakaenda kwa Mkuu wa Wilaya, baadae likaletwa katika kamati yetu, tukamuita yule mwekezaji akakubali.

Kwa kweli mpaka leo utekelezaji wake ule haujatekelezwa na wananchi wanaathirika. Pesa si kidogo karibu milioni kama sikosei zilikuwa ishirini na saba kama sikosei. Sasa kwa kweli kwa wananchi wa kawaida wanyonge eneo lao tayari mwekezaji anaendelea kukusanya fedha, wananchi fedha zao zaidi ya miaka sita sasa hivi. Kwa kweli Mhe. Waziri hivi sasa apunguze shughuli ili awahudumie hawa wananchi waweze kupata hizi fedha zao.

Wananchi wetu tunajua ni wanyonge, wametoa ardhi yao kumpa mwekezaji lakini sasa mwekezaji ameshageuka kwamba yeye ana shughuli nyingi na kuacha wananchi wanahangaika. Kwa hivyo, ninadhani hili Mhe. Spika, kwa sababu hata Kamishna wa *ZIPA* hili suala tulilishughulikia kwa pamoja, analijua. Kwa hivyo, ninaamini na ninategemea kwa kweli tutaweza kupata jawabu ambayo ni nzuri ili kuhakikisha kwamba wananchi wanatendewa haki.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, vile vile, katika eneo hili hili la uwekezaji. Eneo hili juzi Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa hayupo lakini kwa kweli tulilizungumza hasa kwa yule mwekezaji wa *Cristal* ambaye kwa kweli uwekezaji wake sio uwekezaji, umekuwa ni unyanyasaji na udhalilishaji. Mwekezaji huyu ukiacha zile njia alizozifunga, kuwazuia wananchi wasiitumie bahari, wasitumie fukwe lakini bado amekalia eneo la mwananchi mzalendo, amejenga mabanda yake ya hoteli, anaweka wageni, anakusanya fedha ndani ya eneo la mzalendo.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe.Waziri wa Fedha mimi ni rafiki yangu sana, lakini kwa kweli sasa hivi itabidi nitakuja kuzuia fungu la safari za nje ili kwanza afanye kazi za ndani, akishamaliza tutamruhusu aende nje akaendelee kututafutia fedha.

Kwa kweli haiwezekani mwananchi mzalendo, eneo lake linakaliwa na mwekezaji zaidi ya miaka saba, serikali ipo na sisi Wawakilishi tupo, mwananchi anadhalilika. Kwa kweli Mhe. Spika, suala hili siwezi kukubali mwananchi yule akaendelea kudhalilika.

Nilizungumza juzi hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alisema atawaagiza Waziri wa Ardhi na Waziri wa Tawala za Mikoa, lakini wao watakwenda kushughulikia zaidi ya kuzuia njia za watu kwenda baharini, lakini kuna eneo *specific* la uwekezaji, kwa sababu hata huyu mwananchi na yeye ni mwekezaji, vile vile, lakini amezuiliwa eneo lake hawezi kulitumia. Kwa kweli muda umeshakuwa mrefu, hatuwezi tukawavumilia wawekezaji wao ni kuja kukusanya fedha ndani ya ardhi ya nchi yetu, wakawazuia wananchi wetu wasiweze kuendeleza miradi yao. Kwa hivyo, haya Mhe. Spika, ninamuomba sana rafiki yangu, swahibu wangu Mhe. Waziri wa Fedha, ninaamini akiamua kulifanyia kazi, hili suala ndani ya wiki moja linatekelezeka.

Mhe. Spika, nitamuomba sana Mhe. Waziri pamoja na mambo mengi ya nje ambayo tunayomtuma lakini na haya ya ndani vile vile ni muhimu, kwa sababu hawa mwisho wa habari ndio wanaokuja kutupigia kura, tukaingia tena humu, tukavaa suti ili sasa tuweze kuwatumikia wao.

Mhe. Spika, nataka niendeleze jengine katika hawa hawa wawekezaji wa ndani. Mhe. Spika, mimi ninaomba sana Mawaziri wetu hasa Mhe. Waziri wa Fedha, mimi kwa bahati hichi kipindi kifupi nilipokwenda Marekani nimejifunza mambo mengi sana. Na nimejifunza jinsi gani wenzetu *private sectors* ilivyopewa nafasi kubwa sana katika uwekezaji ndani ya Marekani.(*Makofi*).

Mhe. Spika, wenzetu kule ile sekta binafsi kwa kweli serikali imewaandalia utaratibu inawawezesha, imeandaa utaratibu wa mabenki ambao unaweza ukaenda ukakopa fedha wanazozitaka kwa makubaliano maalumu, lakini hapa kwetu Mhe. Spika, bado wawekezaji wetu wa ndani, serikali yetu bado inawaangalia kama ni walanguzi, kama wababaishaji. Na kama kuna matatizo kaeni nao muwarekebishe ili waweze kufuata njia ambazo zilizokuwa sahihi.

Mhe. Spika, hivi sasa tulivyokwenda kule tunategemea kuna *Chamber of Commerce* ya *Seattle* kule Marekani, watakuja kutembelea Zanzibar baada ya ziara ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, wakija hapa watataka waonane na *Chamber of Commerce* ya Zanzibar, waangalie ni maeneo gani wanaweza wakashirikiana.

Leo Mhe. Spika, wawekezaji wetu wana maeneo, tayari wameshayanunua wameshalipa *compensation* ile mpaka *certificate* ya ardhi wameshapatiwa, lakini leo *ZIPA* mpaka leo wanashindwa kutoa kibali. Suala hili aliwahi kulizungumza swahibu wangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kama mwaka mmoja uliopita. Na akamtaka Mhe. Waziri akae na yule mwekezaji mzalendo, waangalie eneo lake na bora nilitaje eneo la Mangapwani ambalo wamekusudia kuweka Chelezo.

Mhe. Spika, kwa kweli eneo lile ni eneo ambalo linatosha kabisa kwa sababu pana kina kirefu cha maji. Mazingira wameshafanya, *certificate* ya mazingira wameshapata lakini mpaka leo kibali cha *ZIPA* hakijatoka.

Mhe. Spika, ukiuliza sababu unaambiwa eneo lile maana yake kuna mahoteli. Mhe. Spika, ndio yale tuliyokuwa tunayazungumza kwamba serikali haijaweka *master plan* ya miji yetu, eneo gani la uwekezaji wa aina gani na eneo gani la uwekezaji wa aina gani, lakini hata hivyo Mhe. Spika, tuangalie kuna baadhi ya uwekezaji sio unaweza ukawekeza eneo lolote. Eneo la Chelezo linahitaji maji ya kutosha na pale yule mwekezaji katika lile eneo lake pamepimwa na pana kina kirefu cha maji, meli ya aina yoyote inaweza kuelea na hao ndio wateja wake.

Sasa leo unaposema kwamba hutaki kumpa kibali cha uwekezaji, umekusudia kufanya nini. Mwananchi yule mzalendo ametumia fedha nyingi, amewalipa wananchi, tayari ameshazungusha ukuta eneo lake, kibali cha kuendeleza mradi wake kwa kweli hawezi kuruhusiwa.

Sasa hii mimi ninaona Mhe. Spika, kwa kweli wawekezaji wetu hatuwasaidii. Mimi naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, hili ninaomba sana kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambayo Idara ya Mazingira ipo chini yangu. Kwa hivyo yule

mwekezaji aliponieleza tu kadhia yake, nikamuuliza je, umeshafanyiwa *EIA*, amenionesha mpaka *certificate* kwamba tayari ameshafanyiwa *EIA* ya mazingira hakuna tatizo lolote.

Mradi ule unaweza ukawekezwa pale lakini leo umekwama Wizara ya Fedha zaidi ya mwaka wa nne. Sasa Mhe. Spika, mimi ninaomba tuwe wakweli sana, tuwe wawazi sana ili wananchi wetu hawa waweze kufaidika.

Hivi sasa Mhe. Spika, katika eneo hilo wamekuja wawekezaji wa aina nyingi. Kuna wawekezaji wamekuja kutoka Oman wameshirikiana na wenzao wa China, kwa sababu Wachina *globally*, wao ndio wanaotawala biashara dunia nzima. Kwa hivyo, tayari wameshakuja wanataka kuwekeza, ukiacha ule mradi wa Chelezo. Kuna na mradi mwengine mkubwa zaidi wanataka kuwekeza katika eneo la pale pale.

Bado mwananchi wetu huyu tunamzuia. Kwa kweli Mhe. Spika, hatuwatendei haki wafanyabiashara wetu wa Zanzibar na hili mimi ninaomba sana na kwa kuwa nimeona, nimeona choyo sana ninapoona wenzetu ya kwamba serikali zao wanawa-*support* wafanyabiashara wa ndani ili kuweza kuwapa *funds* lakini vile vile katika kuwekeza. Kwa kweli hapa kwetu mimi ninasikitika sana.

Taasisi yetu ya *ZIPA* baada ya kwamba hichi kiwe kituo cha kuwahamasisha wawekezaji, kituo hichi kinahangaika kuwatafuta wawekezaji nje lakini kinawaumiza na kuwakandamiza wawekezaji wa ndani. Kwa kweli suala hili mimi siwezi nikakubaliana nalo hata kidogo.

Kwa hivyo, naomba maelezo ya kutosha Mhe.Waziri ili kuhakikisha kwamba huu mradi unaendelea na mwananchi wetu yule, na kwanza pale kuna ajira nyingi sana. Kuna ajira ambazo zitakazotoka pale haipungui watu 150 wataajiriwa katika eneo hilo. Leo tunazuia mwekezaji kama hivyo. Sasa Mhe.Spika, mimi ninafikiri sio jambo zuri sana.

Lakini nikiendelea Mhe. Spika, niliwahi kueleza mara nyingi hapa kwamba Mhe. Waziri, unajua sasa hivi dunia ni utandawazi, tunapokwenda katika mikutano hii ya Mabunge ya *CPA* tunafahamishwa serikali iwe wazi kila kitu inachokifanya. Sasa Mhe.Waziri, mara nyingi nilikuomba kwamba basi ututajie alau ile misamaha ya kodi. Si lazima ututajie watu, maana yake wakati mwengine kuna mambo mengine haya kidogo sisi hatuna tatizo sana, alau kidogo lakini kujua ile misamaha ya kodi imetolewa vipi na inasaidia nini katika kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Spika, misamaha ya kodi sio upotevu wa fedha za umma. Inategemea namna gani munavyojipanga ile misamaha ya kodi iweze kusaidia nchi. Tumekwenda pale Mhe. Spika *Ras Al Khaimah*, tulipokwenda na *Chamber of Commerce*, wao mwekezaji kama mwekezaji unakuja pale, unataka kuwekeza katika eneo la maeneo huru, unaambiwa kwanza ushirikiane na mzalendo wa pale, mzalendo wa pale apate asilimia 52, wewe yako 48. Halafu ardhi unapata ziro kodi, hutozwi kodi kwa muda wa miaka zaidi ya hamsini ni ziro kabisa, lakini ni fursa ambayo wameitoa ili kuhamasisha uwekezaji ndani ya nchi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunapozungumzia misamaha ya kodi, hata ukitaja mabilioni mangapi, sisi wengine hatutafsiri kwamba ule labda ni upotevu wa fedha, lakini misamaha ya kodi mengine inasaidia kuvutia uwekezaji ili wananchi kuweza kupata ajira. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hili usilionee haya kulitaja, kwa kweli tunataka tuone namna gani serikali yetu inavyojipanga katika kuinua kipato cha wananchi.

Mradi wa *e-government*. Mhe. Spika, mradi huu ni mzuri sana tukiweza kufanikiwa, na mimi nilisoma jana ripoti ya wizara inayohusu *e-government*, kwa kweli ni *project* nzuri sana. Ni *project* ambayo *investment* kubwa itawekwa na serikali, lakini baadae tunategemea mapato yale yatarudi kwa njia ya uwekezaji.

Lakini tatizo lake Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, hakufanya taaluma ya mwanzo. Unajua sisi tunaposema semina, watu wanafikiri sisi tunaangalia kile cha mfukoni tu, hakuna, elimu ni muhimu. Mhe.Spika, kama Waheshimiwa wataweza kupata taaluma ya mradi huu wa *e-government* kwa kweli ni mradi ambao utakaobadilisha sana uwazi katika utendaji wa serikali, utaongeza mapato ndani ya serikali lakini vile vile itakuwa ni sehemu ya ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Sasa Mhe. Spika, pengine hata haya ambayo yanayozungumzwa matumizi, manunuzi na kwa sababu mradi ume-*delay* kwa muda mrefu. Sasa mimi nadhani hii ni moja katika inayosababisha Waheshimiwa wengi kuhoji mpaka kusema kwamba kama kuna kufichwafichwa mambo, hebu twende sasa tukajionee sisi wenyewe. Lakini bado pamoja hata Mhe. Spika, utaruhusu Kamati Teule kuundwa lakini bado elimu kwa Waheshimiwa Wajumbe, kujua hasa huu mkonga maana yake nini na una faida gani.

Na hili Mhe.Spika, wenzetu Mauritius katika *e-government* kwa kweli wamefanikiwa vizuri sana. Tulikwenda pale katika Ofisi ya *CAG*, wenzetu wale wamebahatika kwenda maeneo mengi, mimi ninashukuru alau sasa hivi Wizara ya Fedha wamesema huu mkonga *ZRB* pale umeshaungwa. Lakini

ZRB kwa kuwa umeungwa lazima uende sambamba na Ofisi ya *CAG*, kwa sababu wale wanatakiwa *ZRB* anapokusanya mapato, Ofisi ya *CAG* anapata kuona, tunashukuru kwamba na wao wameshafungiwa.

Lakini kitu tunachokiomba Mhe. Spika, suala hili kama wanavyosema wenyewe ni sekta mtambuka. Tunaomba wataalamu wa IT wote washirikiane, wasibakie eneo moja tu. Washirikiane watu wa Ofisi ya *CAG*, Mkurugenzi wa ZAKUKURU, jina lake hatujalizoea vizuri, lakini wenyewe watakuwa wanajijua. Wale wataalamu wao, kwa sababu wale ndio wanao-*monitor* mapato ya serikali lakini vile vile kuangalia uvujaji wa mianya vile vile.

Kwa hivyo, mimi ninaomba sana huu mradi wa *e-government*, kwa kweli sisi tumepata dozi ndogo lakini kuna baadhi ya wenzetu wengi hawajapata hii dozi. Mhe. Spika, ni mradi mzuri sana lakini kwa kweli tunahitaji kupata taaluma kubwa, halafu na sisi tupate kuishauri serikali. Hapa ongezeni hivi, punguzeni hivi ili tuweze kwenda vizuri. Tunategemea mradi huu ukishafanikiwa vizuri, mawasiliano yatakuwa rahisi, hata yale aliyoyazungumza Mhe. Asha Bakari Makame, yataondoka hayo. Mambo unapiga simu unaambiwa yupo nje ya eneo, kumbe yupo jirani yako, eneo lenyewe lipi.

Lakini mimi nafikiri mkonga huu ukiweza kufanikiwa, kwa kweli tutaweza kuingiza mapato mengi sana katika nchi yetu. Tumeona namna gani utakavyoweza kufanya kazi kutumia Kampuni ya *ZANTEL*, ambapo watatumia ile *fiber* yao kwa kupitia mpaka kule upande wa Ras Kiromoni kwendea kule umeme unaoendelea Pemba. Kwa hivyo, huu mradi kwa kweli utaweza kunufaisha sana kurahisisha mawasiliano.

Na sasa hivi Mhe. Spika, teknolojia ipo mikononi. Umelala juu ya kitanda chako unafanya mambo yako yote, unatoa pesa benki, unamrushia mtu, unafanya biashara, upo juu ya kitanda umelala. Mhe. Spika, ndio mambo ya siku hizi yanavyokwenda, na haya yote yanachangiwa zaidi na huu mpango wa *e-government* utaweza kurahisisha hii kazi.

Mhe. Spika, ninajua dakika zangu zimebakia 5. Ninakwenda haraka haraka. Katika suala hili la *special economic zone*. Mhe. Spika, pamoja na kwamba Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alieleza bado kuna changamoto nyingi kuifanya hii Zanzibar tengefu au *special economic zone*, lakini bado Mhe. Spika, mimi ninadhani pamoja na huo mchakato mrefu, lakini bado eneo hili la Zanzibar lina uwezo wa kuweza kutangazwa eneo tengefu. Kwa sababu kama suala la umeme sasa hivi hatuna tatizo la umeme, baada ya ule waya wa *megawatt 100*, mimi ninafikiri kuna umeme mwingi ambao tunaweza kuupata ambao sasa hivi hatuwezi kuutumia.

Kwa hivyo, mimi naomba sana eneo hili Mhe.Spika, kwa sababu eneo hili likiweza kufanya kazi vizuri, litaweza kurahisisha na kuwavutia wawekezaji mbali mbali kuja Zanzibar kuwekeza kwenye sekta ya viwanda.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye Wizara ya Kilimo. Wizara ya Kilimo hapa Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba sana hawa wenzetu wakulima wa mpunga ambao wanaidai serikali zaidi karibu shilingi milioni mia mbili na zaidi. Mhe. Spika, mimi ninadhani kwa kweli hili si jambo sahihi sana. Wakulima wetu hawa walikuwa wanatakiwa wao serikali wawatafutie nyenzo za kuweza kuwasaidia, wawatafutie njia za kuweza kupata mikopo ili kuweza kuendeleza kilimo.

Leo serikali tayari sasa hivi unakaribia mwaka wa pili, wakulima wamelima mbegu, wizara tayari imekwenda imewakopa hawajalipa. Na sasa hivi wamelipa mbegu nyengine wanataka wakawakope. Mhe. Spika, kwa kweli hapa mimi ninaomba sana serikali yetu ifanye kazi ya ziada. Na ninaomba sana Mhe.Waziri hii Wizara ya Kilimo hebu muiangalie kwa jicho linalostahiki, tunasema kwamba pato la taifa karibu asilimia 40 wananchi wanategemea kilimo. Kweli Wizara ya Kilimo tunaiangalia kama kweli uti wa mgongo? Hebu naomba macho yetu yote tuyaangalie katika Wizara ya Kilimo, nikisema hivi munanifahamu.

Mhe. Spika, nikiendelea baada ya marekebisho hayo au baada ya kulipwa wakulima wetu hawa wanaolima mbegu au waliokopwa mbegu ya mpunga kutoka Wizara ya Kilimo, mimi ninaamini, wenzangu wamezungumza kwamba benki ya kilimo. Benki ya Kilimo Mhe. Spika, ni muhimu sana na sio benki ya kilimo tu, hata benki ya maendeleo ya akinamama.

Mhe. Spika, China kule wenzetu kila taasisi ina benki yake. Wakandarasi kuna *contractors Bank*, kuna *agriculture bank*, yaani kule kila taasisi kuna benki yao ipo wazi kabisa kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Sasa hapa Mhe. Spika, nilikuwa nimeiangalia hii taarifa ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambayo walioambiwa wahamasishe, wakulima wa karafuu kununua karafuu zao kupitia benki.

Mhe. Spika, mimi naomba sana hapa inahitajika elimu kubwa sana kwa walimaji wa karafuu. Walimaji wa karafuu sasa hivi Mhe. Spika, wanakopesheka kwa sababu kwanza bei ya karafuu ni nzuri. Sasa tunashukuru karafuu kila mwaka zinazaa pengine mara moja mpaka mara na nusu. Kwa hivyo, hawa kama watasema Mhe. Spika, kama mtu atakuwa anakwenda kuuza *ZSTC*, anachukua pesa zake mkobani. Mhe.Spika, mkulima huyu anakuwa hakopesheki. Wakulima wa karafuu kama tutaweza kuwawekea

structure nzuri, kila mwenye shamba la mikarafuu ana uwezo wa kujenga nyumba ya ghorofa sasa hivi.

Leo Mhe. Spika, wenzetu wa *ZSSF* sasa hivi wameshaanzisha utaratibu. Unataka kujengewa nyumba ya ghorofa, wewe nenda tu. Sasa hawa wakulima wa karafuu, ile *security* yake ni shamba lake la karafuu. Akionekana kwamba mwaka huu kavuna, kapata milioni kumi, mwaka ujao kapata milioni kumi na tano. Ina maana kile kitakuwa ndani ya miaka mitatu minne kitakuwa ni kigezo cha kuweza kumkopesha yule. Leo wakulima wa karafuu wana mashamba makubwa, lakini mtu anakaa katika nyumba ambayo haieleweki. Sasa kama wataweza kuitumia bei tukaweza kuwapa taaluma vizuri, basi Mhe. Spika, katika watu watakaokuwa na maisha mazuri basi ni wakulima wa karafuu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda umemalizika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya, Mhe. Spika, nakushukuru, mengine nayabakisha kwenye bajeti, ahsante.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipatia nafasi asubuhi hii ya leo, kuweza kuchangia machache katika hotuba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spikia, napenda kuwapongeza wanakamati wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwa kutuletea taarifa nzuri. Mimi Mhe. Spika, napenda nichangie kwa upande wa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kuna agizo nambari 11 la wizara ambalo limetakiwa liwasaidie wakulima wa mpunga kwa kuwajengea miundombinu.

Aidha, juhudi za makusudi zifanyike kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Spika, hili ni jambo zuri na kwa upande wa wizara wamesema kuwa wizara tayari imetayarisha na inatekeleza mpango wa muda mrefu wa umwagiliaji maji. Hivi sasa tayari matayarisho ya kilimo cha umwagiliaji wa hekta 2000 umeshaanza. Mhe. Spika, ukiangalia hekta 2000 ni kidogo sana, ukitilia maanani kilimo cha mpunga ni kilimo ambacho wananchi wengi wanakitazamia kiwe ni mkombozi wao.

Vile vile Mhe. Spika, nizungumzie bonde la Koani. Bonde hili Mhe. Spika, lilipata msaada mkubwa kutoka TASAF, na mradi ule ulifikia asilimia kubwa tu ya utekelezaji. Lakini kulikuwa kuna mpango wa kuchimbwa visima viwili, hadi hivi sasa kuna kisima kimoja kimechimbwa na kimoja hakijachimbwa.

Kama wananchi wanategemea kwamba kilimo cha umwagiliaji maji ndio mkombozi wao, bonde lile miundombinu imefanyika kwa maana ya kujenga yale matuta. Nataka kujua baada ya *TASAF* kuondoka, mikakati na mipango yao wizara ya kuliendeleza bonde lile, kwa sababu wananchi bado hawajanufaika na wanaendelea kulima kilimo cha kutegemea mvua. Kwa asilimia kikubwa *TASAF* wameshalitayarisha lile bonde. Je, Wizara ya Kilimo na Maliasili ni hatua gani inayofuata ili kuweza kuwasaidia wananchi wale na kuweza kufanikiwa katika umwagiliaji wa mpunga katika shamba hili.

Mhe. Spika, nikiendelea sisi Wilaya ya Kaskazini B ni wakulima wakubwa wa mpunga, ambao tunategemea sana kwa sasa ilikuwa ni bonde la Kiwanda cha Sukari, na kwa hali hiyo ina maana maeneo ya kulima mpunga hatuna, lakini Mhe. Rais hapa alituhutubia na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa jumla, walisema kuna mbegu ya *NERICA* ambapo tulitegemea kwa sisi hasa watu wa Bumbwini ingetusaidia kulima maeneo ya juu. Lakini hivi sasa hatuoni ule ufanisi wa ile mbegu na kama upo basi Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atuambie, ili kwa sisi ambao tumekosa maeneo ya kulima basi tuweze kuwashajihisha wananchi wetu na tuweze kulima huko minazini na kuweza kufaidika na hicho kilimo cha mpunga.

Mhe. Spika, nikiendelea nizungumze kidogo kuhusiana na Wizara ya Fedha. Mimi niliwahi kuwa Mjumbe wa kamati hii na katika ziara zetu tulifika kisiwani Pemba na tuliliona jengo la Wizara ya Fedha ambalo halikufanikiwa niseme, kwa maana lile jengo halitoweza kutumika.

Kwa hivyo, nataka kufahamu hadi hivi sasa Wizara ya Fedha wamefikia wapi juu ya ujenzi wa ofisi zile. Wakati tulipokuwa kwenye ziara tulipelekwa sehemu moja ya Gombani pale, ni sehemu ambayo inamilikiwa na kiwanja cha mpira cha Gombani, ambacho kipo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Nilitaka kufahamu Wizara ya Fedha pale inapotaka kujenga ofisi katika eneo la kiwanja, walipewa wajenge ama kwa sababu ni eneo la serikali wajenge kama Wizara ya Fedha. Kwa sababu tunavyofahamu ni kwamba maeneo ya michezo yametengwa kwa ajili ya michezo, lakini unapokwenda kujenga jengo la ofisi kwa matumizi mengine, sioni kama kuna mantiki ya yale ambayo yalikusudiwa ya kuwa na eneo la kiwanja na bila shaka kiwanja kinategemea baadae kujitanua kwa kuweka miradi yake ama maofisi au shughuli nyengine za michezo.

Mhe. Spika, mimi naomba niishie hapo, mchango wangu ni mdogo tu. Kwa hivyo, naokoa muda ili na wenzangu waweze kuchangia zaidi. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, nakushukuru sana, umeokoa muda vizuri mno. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadae Mhe. Asha Abdu Haji.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataalla, kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima na leo tukaweza kuendelea na shughuli za kuzungumzia masuala ya wananchi wa Zanzibar, kwa kupitia chombo hiki muhimu sana.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika mjadala wa ripoti hizi za wizara tatu muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu; Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na ripoti ya jumla ya Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, nitakuwa sitendi haki kama sikumpongeza sana Mwenyekiti wa kamati kwa ripoti yake nzuri, iliyopangika, yenye maelezo ya kina na pia kwa uwasilishaji wake mzuri ambapo sio jambo la ajabu kutokana na uzoefu ambao anao Mhe. Spika.

Baada ya kueleza hayo Mhe. Spika, na kwa sababu ya uchache wa muda na kutokana na zile hoja ambazo ningependa kuzichangia ningependa kidogo nieleweke vizuri, naomba nichangie maeneo machache, lakini muda wangu niutumie kueleza kwa kina ili nifahamike.

La kwanza Mhe Spika, nataka niipongeze sana kamati kwa maelezo yake kuhusiana na mradi wa *E-Government*. Kwa kuona uzito wake na mjadala ambao ulizuka katika Baraza hili kwenye kikao cha bajeti, sio mara moja, sio mara mbili wala sio mara tatu, nafikiri katika bajeti za miaka mitatu iliyopita tulikuwa tukizungumza. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kahakikisha katika ripoti yake kuna kurasa tano kuanzia ukurasa wa 181 mpaka 185 alilieleza suala la *E-Government.*

Mhe. Spika, suala la awali kabisa niseme kwamba mimi binafsi naunga mkono hoja yao kwamba panahitajika kuundwa Kamati Teule kuchunguza suala la *E-Government*. Mhe. Spika, naunga mkono pendekezo hili huku nikiwa nina unyonge fulani, kwa sababu najua kwamba kuundwa kwa kamati teule, maana yake ni gharama, lakini nasema suala hili kama lingekuwa linapatiwa majibu ya kutosheleza tokea mwanzo tulipoliibua humu ndani, basi pengine suala hili lingekuwa halina haja leo, lakini bado maelezo hayatoshelezi.

Mhe. Spika, naishukuru kamati kwa sababu katika haya haya ambayo wameyapata pamoja na ufinyu wa muda na kutokuwa na utaalamu wa masuala haya, kuna vitu imevibaini tayari nafikiri ni vizuri serikali ikavizingatia, na sisi Wawakilishi wa wananchi tukavitazama viwe na funzo kwetu.

Suala la kwanza Mhe. Spika, imedhihirika kwamba kuna masuala mengi ambayo hayana majibu. Suala hili nadhani serikali ijifunze kwamba wengi wetu tukija hapa na tukiibua masuala, tunaonekana labda wakali, huwa tumeyafanyia utafiti Mhe. Spika. Ndio maana mimi naweza kusema siku zote ikiwa suala halina matatizo basi mimi wa mwanzo kuliunga mkono, lakini nikigundua kwamba kuna suala lina matatizo basi nitalihoji.

Mhe. Spika, mimi jambo ambalo nimelibaini ni kwamba kwanza nikubaliane na lile ambalo limeelezwa katika ukurasa wa 185, kwenye kifungu nambari 5 kuhusu maoni ya kamati. Naomba nikinukuu kutokana na umuhimu wake.

Kifungu nambari 5;

"Ni vyema kwa viongozi na watendaji wa serikali kuwa waangalifu sana inapotaka kuanzisha miradi mikubwa, kwa vile inaonekana utekelezaji wa miradi mikubwa hapa nchini, huwa ina mashaka na hivyo kuwafanya wananchi ambao ndio serikali inawatumikia, kukosa imani na serikali yao".

Mhe. Spika, mimi nasema kama ningeambiwa niongezee neo, basi ningesema miradi mikubwa na mipya, kwa sababu Mhe. Spika, inawezekana kabisa viongozi wetu walipoamua suala hili, walipewa ushauri mbaya na watendaji ambao pengine wana maslahi yao katika miradi hii. Suala hili naiomba sana serikali ijifunze sasa, kujirejea kila wakati Mhe. Spika, haileti picha nzuri.

Mhe. Spika, hapa tunaambiwa kwamba mradi huu unaonekana kama vile tumekurupuka hatukuwa tayari. Mhe. Hamza Hassan Juma, kaupigia debe sana, mimi sina tatizo na hili wazo kama tungekuwa tayari, lakini Mhe. Spika, huwezi kutanguliza gari kama hujawa na punda. Sasa leo tunaambiwa, kwanza ofisi nyingi za serikali hazina *local area network*.

Jengine ni namna ulivyotekelezwa. Kamati wanathibitisha humu kwamba kuna uharibifu wa mara kwa mara kwa sababu kina kilichotumika kuzikia hiyo *fiber optic* kina matatizo sio cha kutosheleza, na hili nililisema humu ndani ya Baraza Mhe. Spika. Sisi wengine kwenye Kamati ya mawasiliano na ujenzi tulipokwenda katika sekta na tukaambiwa haina matatizo. Kama haina matatizo kwa nini upate matatizo.

Lakini jengine Mhe. Spika, hata nikasema serikali imekurupuka, ni kwa sababu humu kamati imetwambia kwamba uharibifu huu mkubwa umetokea kwa sababu kuna utekelezaji wa miradi mingine kwa mfano wa maji, pengine matengenezo ya barabara yakiingia kati, basi yanavuruga mkonga. Sasa kama kungekuwa kuna uratibu wa pamoja wa serikali katika suala hili basi yasingetokezea haya. Ndio maana nasema kuna vitu vya kujifunza humu ndani.

Mhe. Spika, jengine tumeambiwa humu kwamba lengo lilikuwa ni kuwa na majengo kadhaa ikifika mwisho wa mwezi wa Disemba mengi tu ya serikali, kwamba ndio itakuwa yamekamilika ikifika mwezi wa Disemba 2013. Sasa huu Mhe. Spika, tuko mwezi wa Januari 2014. Kamati inatwambia kwamba ni majengo manne tu ambayo yameunganishwa na mtandao. Tena katika hayo Mhe. Spika, kwa uhakika ni matatu, kwa sababu moja ni *data centre;* ni kile kituo chenyewe ambacho kimekuwa ni makao makuu ya mradi huu, hapa Mazizini.

Sasa Mhe. Spika, mimi napata matatizo hata kwamba serikali imejipanga katika uendeshaji wa huu mradi wenyewe. Kwa sababu huku inaambiwa Idara ya Mawasiliano katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ndio isimamie, lakini upande mwengine suala la *E-Government* yenyewe limepelekwa sasa naambiwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kwa mujibu wa ripoti hii.

Sasa Mhe. Spika, najiuliza kama ni suala la *E-Government* hata kama ingekuwa ni wizara mbali, ningetegemea ingekuwa ni Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma maana ndio inayosimamia ofisi zote za serikali. Sasa hata serikali yenyewe haijajua bado inataka isimamie wapi, lakini kwani ingebakia Wizara ya Mawasiliano hili, na kama ndio idara ya mawasiliano iko pale kwamba masuala ya mawasiliano ndani ya serikali kwa mfumo wa *E-Government* yangeachwa pale, lakini usimamizi wenyewe una wizara zaidi ya mbili Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kama hilo halitoshi, tumeona humu kwamba kulikuwa kukabidhiwe uendeshaji wa mradi huu kibiashara sasa kwa Kampuni ya Zantel. Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wanajua, tukizungumza na Zantel wao wenyewe wana maswali mengi tu ambayo wanaona kwamba hayajajibiwa na serikali katika kukabidhiwa mradi huu.

Kwa hivyo, kwa kifupi Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba inathibitika kwamba tulikurupuka kufanya mradi ambao ulikuwa bado hatujawa tayari, tumeiingizia serikali hasara ya kwenda kukopa dola 20

milioni, ambazo mimi sina hakika kama tija yake tutaiona, au tutaingia kama miradi mingine magharama, kama ule mradi wa *Airport* ule. Tutaingia magharama mengine ya kuja kutumia pesa nyengine za ziada kurekebisha mambo yaliyokuwa hayakuzingatiwa pale mwanzo, huu sio utumizi mzuri wa fedha za serikali Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kila siku nasema mkopo sio msaada; mkopo unaning'inia katika shingo za Wazanzibari, serikali inabidi ilipie deni hilo. Kwa hivyo, inabidi ifanye kazi ya kutoa mapato yake na baadae iwe inalipa deni kwa mujibu wa makubaliano yaliyokuwa yamefikiwa.

Sasa Mhe. Spika, kutokana na hayo niseme kwamba katika hili mimi naridhika kabisa kwamba tuna haja ya kutizama sana kwa kina na kwa undani kabisa, ni yapi yaliyokuwa malengo ya mradi huu, na kweli ulikuwa na lengo la kuisaidia nchi yetu? Watendaji wamefaidika na nini na gharama halisi za msaada huu zilipaswa ziwe ni za kiasi gani. Kwa sababu niliwahi kusema hapa. Mimi niliwahi kukaa na wataalamu ambao walifanya kazi katika upande mwengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Walifanya makisio na kwa kitaalamu kabisa, wakasema mradi huu usingeweza kugharimu zaidi ya dola milioni 7, zimefikaje dola milioni 20. Kwa hivyo, kuna maswali mengi ambayo yanahitaji majibu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika hili mimi naomba kuunga mkono kabisa suala la kuwa kunahitajika Kamati Teule. Tumepitia taratibu zote za kawaida za Baraza kupata majibu, lakini hatuyapati majibu Mhe. Spika. Nilisema hapa juzi tulipokuwa tukijadili, kwamba mimi nilikuwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, tuliandika mpaka barua chini ya Mwenyekiti wetu Mhe. Ali Abdalla Ali, ambaye ni Naibu Spika, mwaka mzima hatukujibiwa. Kamati iliyokuja mara hii iliyokuwa inasimamia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala nayo imesema kwamba imeshindwa kupata majibu.

Juzi iliwasilisha ripoti yake hapa wakasema kwamba imefika pahala iundiwe Kamati Teule, ukatuongoza Mhe. Spika, kwamba tusubiri wizara inayohusika na mradi uliosimamia Wizara ya Fedha, ambayo leo ndio wakati wake tupate majibu, labda baada ya hapo ndio tutaamua. Mimi naomba tuunge mkono pendekezo la Kamati kwamba tuunde kamati teule.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo kama nilivyosema nilikuwa nimechagua masuala machache kwa sababu ya muda ili nieleweke hoja yangu. Naomba niingie suala jengine, sitaki kuzichangia wizara nyengine hizi mbili kwa kina, kwa sababu naona tatizo liko pale pale nililolizungumza juzi kwamba tuna tatizo kuwa wizara nyingi tukienda bajeti zilizoingiziwa ni kwa kiwango kidogo sana.

Jana Mhe. Spika, katika kikao cha jioni Mhe. Waziri wa Fedha, alitoa maelezo. Kwa bahati nimekwenda kuomba mpaka *hansard* nijiridhishe kabisa kwamba nimemfahamu vizuri. Mhe. Spika, mimi naomba bado katika hili Mhe. Waziri wa Fedha, akija atusaidie zaidi.

Mhe. Spika, katika maelezo yake Mhe. Waziri wa Fedha alitwambia kwamba katika bajeti aliyoiwasilisha, alisema kwamba serikali inatarajia kukusanya mapato ya ndani ya bilioni 423. Halafu katika ufafanuzi wake alisema ZRB walikuwa wakusanye bilioni 155.3, TRA wakusanye bilioni 147.6 na nyengine zingetokana na mkopo wa ndani bilioni 25. Fedha ambazo zimebaki mwaka jana wakazileta mwaka huu bilioni 5, *JBC* bilioni 40 na *MDRI* bilioni 2, ukizijumlisha hizo utapata bilioni 427.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha, alitoa maelezo yake kiwango halisi cha ukusanyaji. Lakini hiki bahati nzuri Mhe. Spika, hata kamati wamekieleza. Ukiangalia ripoti hii ya kamati utakuta *ZRB* imefikisha katika miezi mitano ya awali waliokuwa wamefanya tathmini asilimia 101 ya malengo ya makusanyo yake. *TRA* imekusanya asilimia 90 kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba bilioni 1 na nukta kadhaa. Kwa wastani ni kama bilioni 91 kwa upande wa *TRA.*

Sasa Mhe. Waziri wa Fedha alitwambia kwamba mapato ya *ZRB*, takriban yote inakwenda katika mishahara. Mhe. Spika, nilitegemea katika hili nikubaliane naye, lakini najiuliza ikiwa malengo yamefika asilimia 101 kule na kwenye *TRA* kuna asilimia 90, mbona hii asilimia 90 ya *TRA* ambayo ingekwenda kuhudumia hayo matumizi mengine hayaonekani katika mawizara mbali mbali, ikiwa umefika asilimia 90 lakini huku uingizwaji wa fedha nyengine ni asilimia 24, asilimia 23 na asilimia 26 je kuna nini. Kwa hivyo, ningeomba suala hili Mhe. Waziri wa Fedha, akija atuelimishe.

Mhe. Spika, nauliza suala hilo kwa sababu katika maelezo yake aliyoyatoa jana, kasema katika kuhakikisha kwamba wanawabakisha wataalamu ndani, walikadiria kutumia bilioni 76.5 lakini wakatumia bilioni 77.4. Hapa Mhe. Spika, pana ongezeko la milioni 900, tuchukue bilioni moja. Sasa vipi bilioni moja iathiri? Kama hii ndio wanasema imebidi waitoe katika *OC* na *development fund.* Sasa bilioni moja vipi Mhe. Spika, hii iwe ati makusanyo ambayo yamefika asilimia 90 isiakisi katika kuingizwa fedha katika bajeti za wizara mbali mbali. Mhe. Spika, nadhani hilo napaswa kuja kujibiwa.

Mhe. Spika, niseme kwamba yeye mwenyewe Mhe. Waziri wa Fedha kuna changamoto ambayo kaizungumza mwisho wa maelezo yake ya jana, aliposema naomba nimnukuu;

"Tulipoingia mwezi wa Novemba, 2010 tulikuwa tunakusanya *TRA* na *ZRB* kwa pamoja kwa mwezi bilioni 13 na leo tunakusanya kati ya bilioni 27 na 28 kwa mwezi, mapato yetu yameongezeka, lakini na sisi tumepanua matumizi tunafikiria jinsi ya kubana kidogo matumizi ili twende kulingana na hali halisi ya mapato"

Mhe. Spika, naona kidogo unaanza kuelekea kwenye spika yako namaliza sasa hivi. Mhe. naomba anisaidie tu Mhe. Waziri wa Fedha, yeye kwa mtazamo wake kwa sababu ndio tumempa *ex-chequer* aisimamie. Je, haya matumizi yameongezeka wapi Mhe. Spika. Je, ni huku kuunda kwetu kwa taasisi mpya kila siku na ambazo zimeonekana kwamba nyengine hazileti tija kwa sababu haziingiziwi fedha.

Kwa mfano Mhe. Spika, Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe inashindwa kufanya kazi zake. Kamati inaturipotia kwamba hata ghala moja tu ya Unguja kutengeneza imewashinda kwa sababu hawana bajeti. Sasa tumeiunda katika kipindi hiki cha miaka minne hii, lakini kwa nini tunaongeza bajeti ya kwenda kuongeza gharama za utawala na mishahara yao wakati ile tija inayokusudiwa haipatikani.

Hiyo Mhe. Spika, ukienda kuangalia pengine katika Bodi ya Viwango, *ZBS*, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, tumeziunda hizi lakini hiyo tija yake haipatikani kwa sababu hawaingiziwi fedha. Kwa hivyo, tunaongeza gharama ya uendeshaji wa serikali, lakini tija ya kuziunda taasisi hizi haionekani. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe una kasoro ya dakika tano, yaani dakika tano hazitimii kwa muda wako uliobaki.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri wa Fedha, akija atusaidie na pengine asaidie kuna haja ya kushawishi serikali.

Moja ambalo Mhe. Spika, nilikuwa nikisema ni kwamba tuna haja ya kutizama muundo wa serikali yetu, lakini tuna bahati mbaya. Hakuna kitu kibaya kama ndani ya serikali kukawa na viongozi ambao wana-*inferiority complex,* kwamba madamu suala fulani limesemwa huku basi mimi sitekelezi, au madamu ushauri umetolewa na mtu fulani basi mimi siutaki, naonesha tu kwamba mimi nina nguvu fulani. Mhe. Spika, hiyo sio picha nzuri hata kidogo.

Mimi nadhani chombo hiki kazi yake ni kuishauri na kuielekeza serikali, kuna haja ya kuangalia ukubwa wa serikali yetu, mimi naamini sehemu kubwa ya bajeti kama tulikuwa tunapata bilioni 13 mwaka 2010. Leo tunafika bilioni 28 ni zaidi ya mara mbili ya bajeti iliyokuwa inakusanywa. Tujiulize kwa nini wakati ule mambo kwa kiasi fulani yalikuwa yanakwenda na yanaonekana na leo hayaendi, haya matumizi makubwa yanaingia wapi, kama ni ukubwa wa serikali tumsaidie Mhe. Rais kumshauri, ili tuone kwamba kuna haja ya kupunguza ukubwa wa serikali yetu, ili tija iende katika kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha vile vile aje anisaidie suala moja la mwisho. Mhe. Spika, suala hili sikuliona katika ripoti za kamati wala katika ripoti za wizara, kwa sababu wizara wanajibu utekelezaji lakini lilijitokeza.

Suala la fedha za Zanzibar kutoka Mfuko wa Jamhuri ya Muungano zinazotokana na kodi ya *paye*. Mhe. Spika, tuliambiwa kwamba zitalipwa, tukaambiwa kuna madeni hazilipwi, kuna mwaka mmoja mzima nafikiri hazikulipwa. Hivi karibuni katika wiki iliyopita tulisoma katika vyombo vya habari wakati wanalumbana baina ya *TANESCO* na *ZECO* juu ya ulipwaji wa deni lao. *ZECO* wakataja kauli ambayo Mhe. Waziri wa Fedha aliwahi kuitoa humu ndani ya Baraza, kwamba katika vikao vya mashauriano baina ya serikali mbili; Serikali ya Zanzibar iliwaambia zile bilioni 18 mliosema tunawadai nyinyi zilipeni *TANESCO* ili mpunguze deni lenu kwa Zanzibar.

Juzi *TANESCO* wametangaza kwamba wanaidai Zanzibar kwa maana ya *ZECO* bilioni 77, wakati *ZECO* wanasema bilioni 40. Hebu Mhe. Waziri wa Fedha aje atwambie *status* ya zile bilioni 18 ambazo ni za mwaka mmoja tu, kuna miaka mingi hawakutulipa, zile za mwaka ambazo walizokubaliana tuanze kulipana *paye* bilioni 18 kwa nini hazikulipwa mpaka leo?

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nashukuru kwa kunivumilia, nasema naunga mkono ripoti ya Kamati kwa asilimia 100, ahsante sana *(Makofi).*

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuchangia ripoti hii. Kwanza kabisa naipongeza kamati na watendaji wake wa wizara wote kwa ujumla.

Pili, naanza kwa masikitiko makubwa kwa idara hii ya kilimo, idara hii ndio kiini cha Wizara hii ya Kilimo na Maliasili, lakini ina malalamiko makubwa kwa wakulima wa mpunga. Lakini cha kusikitisha wakulima wale wanalima kwa kutegemea pesa zile ziwasaidie kuwasomesha watoto, ziwasaidie kwa matibabu na kukidhi maisha yao, lakini sasa hivi wanalima matokeo yake

mbegu ile inachukuliwa na wizara na kupewa watu wakaendelea na kupanda. Mhe. Spika, cha kusikitisha hawawalipi pesa zile na hatimaye idara inadaiwa milioni 240. Bonde la mpunga la Mtwango peke yake linadai milioni 60, suala hili ni la kusikitisha kwa wakulima wale.

Mhe. Spika, la kusikitisha zaidi tulipokenda kwenye bonde lile tulikuta mbegu tayari inataka kuvunwa, lakini wale watendaji walisema kwamba na ile mbegu pale tunaitaka pia tukopeshwe, hilo ni la kusikitisha zaidi, ambapo deni la nyuma hawajawalipa na zile mbegu pale kwenye mabonde bado wanazitaka.

Mhe. Spika, vile vile, la kusikitisha zaidi ni Wizara ya Fedha. Bajeti hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili ni finyu sana, bajeti ambayo wanapangiwa basi sio ambayo wanapewa. Labda wizara hii ni yatima haina baba, wizara hii kweli haina baba lakini yupo waziri ambaye anakaimu, japokuwa yeye ana wizara, lakini akifika kule na hii wizara aitetee kutokana na bajeti yake ni finyu na bado deni ni kubwa inayodaiwa na wakulima.

Mhe. Spika, kuna kilimo cha umwagiliaji maji, ambapo sisi tumezoea kilimo cha umwagiliaji wa mpunga, kuna kilimo cha umwagiliaji wa migomba, umwagiliaji wa mboga na umwagiliaji wa tungule. Kwa hivyo, ningeiomba wizara katika kilimo cha umwagiliaji migomba ambacho kinahitaji pesa nyingi za kuchimba kisima, kutia umeme na mipira.

Kwa hivyo, ningeiomba Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto iwawezeshe wananchi ili waweze kujishughulisha na kilimo cha migomba, mbali ya kilimo cha mpunga ambacho kinahitaji mabonde. Kilimo cha umwagiliaji migomba kinakuwa hata kwenye tambarare tu.

Mhe. Spika, ningeiomba wizara iwasaidie, kwa sababu kilimo cha migomba ni kilimo ambacho kina tija. Mhe. Spika, tulikwenda Makunduchi ili kuangalia kilimo kile, hekta moja ina migomba 300 na kila mgomba hivi sasa umeshaanza kuzaa, kila mgomba una chana hazipungui 13 au 15, hayo ni mafanikio.

Kwa hivyo, ningeomba Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, iwawezeshe wananchi ili waondokane na tatizo la kilimo, ili wawawezeshe kuwapa uwezo wa kulima kilimo cha umwagiliaji wa tungule, migomba na viazi. Wakiwawezesha basi watajitahidi na wataondokana na umaskini. Naiomba wizara washirikiane na Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto wawaone wananchi hawa, ili waondokane na kilimo

chengine na wajishughulishe na kilimo hiki cha umwagiliaji. Ahsante sana nashukuru.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa. Pia, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi muda niweze kuzungumza machache.

Vile vile, nichukue fursa hii nimshukuru Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii, ambaye amefanya kazi vizuri na kila siku zinaonekana kazi zake zinaendelea kuwa nzuri zaidi, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amzidishie.

Mhe. Spika, kwanza nianze na hii Wizara ya Kilimo na Maliasili. Nianze na huu mpango wa chakula na lishe. Mhe. Spika, wenzangu waliotangulia wamesema na mimi napenda nisisitize, kwa sababu chakula na lishe ni kitu muhimu ambacho kinatufanya sisi tuweze kusimama hapa. Leo uliletwa mswada katika Baraza lako hili tukufu na tukaupokea kwa mikono miwili, tukaujadili na tukaupitisha kwa sababu tuliona ni jambo la maana. Lakini mpaka leo hii inaonekana hakuna utekelezaji wowote juu ya suala hili.

Mhe. na mimi niungane na wenzangu kusisitiza suala hili la lishe ni kitu muhimu sana. Mheshimiwa tuseme Mwenyezi Mungu atuepushie mbali lakini kuingia ukame hapa kwetu hatuna akiba ya chakula hata cha siku moja. Hili ni tatizo na wakulima wanalima na hicho hicho chakula ambacho kidogo tunakipata, lakini bado serikali haijajipanga kuweza kuwahamasisha wakulima wale wawe wanajiekea akiba.

Nimewahi kusema mimi wakati wa mswada, ulimaji wa mahindi wananchi wetu wanalima, lakini hatimae mahindi yale yanaishia kuchomwa tu siku hizi, yanauzwa mabichi na wakati ukila mahindi hata kumi ya kuchoma hutosema kuwa leo mimi sitokula tena nyumbani nimeshiba. Lakini mahindi yale yale yakianikwa yakakaushwa na yakaweza kusagwa ukapatikana unga ukasongewa sembe, basi kama utakula robo utajisikia umekula na umeshiba. Kwa hivyo, Mheshimiwa mimi bado nasisitiza wizara hii ijitahidi kuwahamasisha wakulima wetu na tuwe na tabia jamani ya kujiwekea akiba ya chakula.

Mhe. Spika, jengine kumeonekana kuna uingiliwaji wa vyanzo hivi vya maji ambapo wananchi wanavamia kwa kujenga. Mimi bado niisisitize serikali kwamba tukiweza kudhibiti vyanzo vyetu tukavijengea basi sidhani kama uvamizi unaweza ukatokea. Kwa sababu itakuwa tumeshaweka hadhari mapema, kwa hivyo athari haiwezi kutokea.

Mhe. Spika, jengine ambalo na mimi linanisikitisha ni zile fedha za wakulima. Mhe. Spika, wakulima ni watu wanyonge sana na sisi huwa tunahamasisha ili walime waondokane na unyonge huo. Lakini leo utakuta serikali baada ya mzigo ulionao unajitwisha tena mwengine, kuzichuka fedha zile za wakulima na baadae wasipatiwe yale mahitaji ambayo waliyahitaji! Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naomba sana Wizara inapokusanya fedha kwa wakulima wetu basi iweze kuwapatia mahitaji yao, ambayo yamekusudiwa kama ni mbegu, ulimaji wa trekta au mbolea lakini waweze kupatiwa, tena na wapatiwe kwa wakati.

Mhe. Spika, nije katika Wizara ya Biashara. Mhe. Spika, pia katika wizari hii mimi nichukue fursa ya kumpongeza sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri wake na watendaji wake wote kwa juhudi zao kubwa, kusema kweli wanachapa kazi sana na ushahidi ni juzi ambapo tulipitisha mswada wa sheria mpya ya karafuu, ambao mswada huu umeleta matumaini makubwa sana kwa wakulima wetu wa karafuu.

Mhe. Spika, labda sisitizo langu lije kwa wajasiri amali wadogo wadogo. Niiombe sana Wizara iweze kuwatafutia masoko wajasiri amali wetu kwani wanajitahidi sana lakini biashara hawana pa kuziuza. Tukiwatafutia wajasiri amali masoko wakaweza kufanikiwa kuuza biashara zao, basi ninaamini tutaweza tukapunguza umaskini kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, nije katika Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha mimi niseme vyanzo vya mapato vipo, ingawa vipo kidogo lakini vipo na mapato yapo. Lakini kinachojitokeza ni ule usimamizi mzuri au uzibaji wa mianya ya uvujaji wa fedha hizo. Mhe. Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri, ajitahidi sana kudhibiti mianya ambayo mapato yetu yanaonekana yanavuja kwa wingi. Mhe. Spika, serikali huona kumhamisha mfanyakazi kutoka sehemu moja kwenda nyengine labda ndio dawa ya kuzuia mapato yasivuje, hiyo si dawa. Dawa yanapotokea mtu anapotambulikana kama huyu amesababisha uvujaji wa fedha, basi ni kumchukulia hatua za kisheria ili na walio pembeni yake waweze kujua kama huu si mchezo mzuri na waweze kuachana na tabia hiyo.

Mhe. Spika, mimi nije katika huu mkonga ambao wenzangu wameuzungumzia na mimi nilitaka niiugusie kidogo. Kwa sababu tulizungumza sana hapo nyuma na mimi nilizungumza sana kipindi kilichopita, kwa kusema serikali inapokuwa na miradi yake kama hii basi ni vyema kukawa na mashirikiano. Kwa sababu miradi yote ni miradi mikubwa na miradi ya jamii yote tunapelekea wananchi wetu huduma. Leo kama hatujipangi ikawa tunazitumia tu fedha za serikali, tunatengeneza hii, lakini unakuja mradi mwengine tunaharibu hili. Mhe. Spika, hapo itakuwa hakuna

ufanisi mzuri. Kwa hivyo, mimi niiombe sana serikali tunapokuwa na miradi kama hii, basi zile Wizara ambazo zitahusika ziweze kukaa pamoja na kuona wana mipango mizuri ambayo haitoathiri mradi wa mwenzake.
Mhe. Spika, mimi niseme tu ninaipongeza sana taarifa hii ya kamati na ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Baada ya kusema hayo ninashukuru na ninawatakia kila la heri. Ahsante.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi ninamshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo asubuhi hii katika Baraza lako kwa madhumuni yale yale ya kutekeleza wajibu na majukumu ambayo tumepangiwa na wananchi wetu wa Zanzibar.

Lakini la pili, nichukuwe nafasi ya kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo na Wajumbe wake kwa kutuletea ripoti hii mbele yetu, ili na sisi tutie mawili matatu kama Baraka zetu kuiboresha ripoti. Pamoja na hayo ninawashukuru mawaziri wote waliosoma ripoti za utekelezaji kwa maagizo ya kamati waliopewa katika kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu uanze katika hili buku kubwa la ripoti za Kamati za Kudumu ukurasa wa 160 Idara ya Umwagiliaji Maji. Mhe. Spika, hii inahusiana na masuala mazima ya kilimo. Tumetoa lugha nyingi na matamko mengi kuhusiana na suala zima la kuboresha kilimo. Tumesema kwamba kilimo ni uti wa mgongo, tumesema tuna mapinduzi ya kilimo, na lugha nyingi ambazo zinaboresha neno kilimo. Lakini tukiangalia jinsi ya kilimo chetu kilivyo basi ubora wa matamko haya ambayo tunayatamka hauonekani.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa niende katika bonde la Makombeni na hapa nitanukuu katika maelezo yaliyomo ndani ya kitabu hiki kilichopo mbele yetu. Kamati ilipokea taarifa fupi kuhusu bonde la Makombeni, kuwa bonde hilo liliingizwa katika mradi wa umwagiliaji wa maji ulioendeshwa kwa kushirikiana na serikali ya Japan. Mradi huo ulitakiwa kuanza mwaka 2009 hadi 2010, ambapo hadi sasa jumla ya Tanzania *Shillings* milioni 311,877,550 zimeshatumika katika mradi huo. Hata hivyo kazi ya umwagiliaji maji katika bonde hilo bado haijaanza kutokana na kasoro kadhaa zilizojitokeza.

Mhe. Spika, hili ni tatizo tena tatizo kubwa sana kwamba fedha zilizotumika katika bonde hili shilingi milioni mia tatu tokea 2009 mpaka leo mradi huu umeshindikana kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa kweli Mheshimiwa tungeiomba Wizara ya Kilimo iwe makini sana kusimamia miradi kama hii, ambayo inapoteza fedha nyingi za wavuja jasho wa nchi hii.

Mhe. Spika, kwa kweli tamko la kilimo cha umwagiliaji maji hapa Zanzibar, tumelianza muda mrefu lakini nimuulize Mhe. Waziri hivyo tumefaidika kiasi gani na kilimo cha umwagiliaji maji hapa Zanzibar? Kwa sababu tuna maduka mengi na masoko mengi hapa Zanzibar hatujakuta hata soko moja au duka moja linalouzwa mchele kwa ajili ya mahitaji ya wananchi wa Zanzibar, Mchele unaotokana na kilimo cha umwagiliaji kutoka Zanzibar. Tunakutia mchele unatoka Tanganyika na kwengineko. Je mapinduzi haya ya kilimo mpaka lini tutafikia manufaa yake?

Mhe. Spika, kwa kweli hili linakwenda sambamba na bonde la Mtwango, yameelezewa hapa maelezo mbalimbali ambayo yamerudisha nyuma maendeleo ya kilimo hiki cha umwagiliaji katika mabonde haya. Mhe. Spika, tuna mabonde mengi Zanzibar, mabonde yenye rutba lakini yamekosa miundombinu huku tukitumia mamilioni ya shilingi bila ya kufikia lengo. Mhe. Spika, mimi ninamuomba Mhe. Waziri, aangalie kusijekuwa kuna wajanja wachache ambao wanatumia mbinu kutumia fedha hizi kwa mgongo wa umwagiliaji maji.

Mheshimiwa inasikitisha sana kwamba kila siku tunapiga kelele za umwagiliaji, umwagiliaji, lakini kinachomwagika si maji bali ni fedha za wananchi. Na fedha hizi hazimwagiki tu, zinamwagika ndani ya mikono ya wachache, ndani ya mikono ya wajanja, ndani ya mikono ya wenye mbinu, ndani ya mikono ya watu ambao wanawadhalilisha walio wengi. Mheshimiwa, ninaiomba serikali iwe makini sana juu ya suala zima hili la kunzisha miradi hasa miradi mikubwa kama hii ambayo haifikilii lengo la wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiacha hapo nende katika Ofisi Kuu Pemba. Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 165 maslahi madogo kwa wakuu wa Idara Pemba. Mheshimiwa, nikinukuu katika kitabu hiki kinaeleza hivi, "ilielezwa kuwa wakuu wa Idara kwa Wizara zote hawalipwi stahiki zozote zinazolingana na nyadhifa zao, isipokuwa mshahara wa kawaida tu". Mhe. Spika, hili ni tatizo. Wakuu wa Idara wameteuliwa kwa mujibu wa umuhimu wa kufanya kazi zao. Kwa hivyo, ni vyema serikali, ikawapatia mahitaji na maposho yao na stahiki zao zote, si vyema kuwaweka kama Wakuu wa Idara ya kibandia.

Mhe. Spika, haipendezi hata kidogo watu kupewa majukumu ya kusimamia wafanyakazi halafu maslahi yao yakaonekana si chochote si lolote. Mhe. Spika, haki na wajibu ni watoto pacha, kama ambavyo wanatekeleza wajibu wao basi ni vyema na haki zao wapewe. Kuna usemi unaosema" mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni". Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha sana kwamba masuala haya hayako katika uangalizi wa hali ya juu kwa wakuu wa Idara ambao wanasimamia Idara mbali mbali za serikali.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika Wizara ya Fedha katika suala zima la Kampuni hii ya *ZANTEL*, vituo vya mkonga. Lakini hapa ninazungumzia kuhusiana na habari ya changamoto tu zilizopo. Changamoto nambari 4 inasema Afisa Mdhamini Wizara ya Fedha Pemba, kutoshirikishwa katika miradi inayotekelezwa Pemba ambayo inasimamiwa na Wizara ya Fedha na hivyo kukosa taarifa zinazohusiana na miradi hiyo.

Nikiondoka hapo nataka niunganishe nende katika Ofisi Kuu Pemba, vile vile katika ukurasa wa 187 kwenye changamoto. Changamoto ya 4 inasema ushirikishwaji mdogo wa Ofisi ya Afisa Mdhmini Pemba katika kazi za miradi ya maendeleo ya Wizara zinazofanywa kisiwani Pemba. Mheshimiwa ningemuuliza Waziri wa Fedha Wizara ya Fedha kuna tatizo gani la hawa Maafisa Wadhamini pale Pemba kutokushirikishwa katika masuala ya miradi ya maendeleo, wale ni maafisa ambao wameteuliwa rasmi kusimamia miradi mbali mbali iliyopo pale Pemba. Kwa nini hawashirikishwi katika miradi mbali mbali ya maendeleo na Kamati inakwenda inashindwa kupata jawabu sahihi, lazima jawabu hizo zipatikane mafisa kutoka Unguja.

Mheshimiwa nikiondoka hapo niende katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Spika, nizungumzie kuhusu suala la *ZSTC*. Ninaipongeza Wizara kuongeza fedha kwa ajili ya zao la karafuu, lakini ninasikitika sana kuona kwamba mezani zinazopimiwa zimepitwa na wakati. Ninaishauri Wizara ya Biashara itafute mezani mpya za kisasa ili ziendane na wakati tulionao.

Na pia changamoto nyengine ambayo inawakabili wauzaji wa karafuu ni vipimo. Vipimo vinavyopimwa pale ni kilo moja na nusu kilo, kuna bakaa ya robo kilo, wakia na thumni hizi wakulima wa mazao ya karafuu hawalipwi, ninamuomba Mhe. Waziri aweke mazingira mazuri kwamba kutokana na umuhimu wa karafuu na bei ilivyo, basi robo kilo, na thumni, zifanyiwe thamani zake. Kila mkulima anayekwenda kuuza karafuu basi punje yake ya karafuu iweze kupata malipo. Kwa sababu robo kilo za karafuu zinazouzwa, kwa siku zote pale ni nyingi na nani ambae anafaidika na robo na thumni kilo zile. Kwa hivyo, ninamuomba Mheshimiwa hili aliangalie vizuri na azungumze vyema na watumishi wake, wanaopima karafuu ili robo kilo za karafuu na ziada ya hapo zipatikane kwa wakulima wa karafuu.

Mhe. Spika, vile vile, masikitiko makubwa kuhusiana na bei ya makonyo ya karafuu. Makonyo kwa kweli bei yake ni ndogo. Kilo shilingi mia saba! Kwa kweli ni ndogo sana. Ninamuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina suala hili ili wale wauzaji wa makonyo na wao wajisikie. Kutoka shilingi mia saba angalau mpaka shilingi 1500 au zaidi ya hapo.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa190 kwenye kiwanda cha sukari mahonda. Mhe. Spika, naomba ninukuu, "tarehe 2/01/2014 kamati ilitembelea kiwanda cha sukari pamoja na mashamba ya miwa ya kiwanda hicho Mahonda. Katika ziara hiyo kamati ilijionea jitihada kubwa zilizofanywa na uongozi wa kiwanda hicho". Lakini ninachokusudia hapa kwamba kiwanda kinatarajiwa mwishoni mwa mwezi wa Januari, 2014 kuanza kuzalisha.

Naenda katika changamoto, kutokabidhiwa kwa uongozi wa kiwanda hicho, nyumba 150 za kiwanda hicho ambazo zimekuwa zikikaliwa na wananchi. Hali hii imewafanya wafanyakazi wa kiwanda hicho kukodi katika nyumba nyengine kwa fedha zilizo nyingi. Mhe. Spika, hili ni tatizo. Ikiwa kiwanda kina nyumba 150, wafanyakazi wake wanalazimika kukodi nyumba nyengine na nyumba za Kiwanda zipo. Ninamuomba Mhe. Waziri, suala hili aliangalie kwa umakini mkubwa na tatizo hili litatuke.

Mhe. Spika, kwa haya machache na kuokoa muda ninashukuru kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Spika: Tuna wachangiaji wanne waliobaki na dakika zilizobaki ni kama dakika arubaini. Hivyo, tugawane dakika hizo kwa dakika kumi kumi ili tuweze kumaliza michango, kipindi cha asubuhi na jioni twende kwenye majumuisho moja kwa moja.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kupata nafasi ya kutoa machache kuhusu ripoti hii ya Kamati Fedha, Biashara na Kilimo. Mimi niipongeze tu kamati hii kwa kazi nzuri iliyofanya mpaka kuweza kutengeneza ripoti hii na kuiwasilisha hapa leo. Mhe. Spika, mimi pengine dakika kumi ziwe nyingi. Nianze na Idara ya Kilimo. Mhe. Spika, nchi yetu kila kitu tunakifanya kuwa uti wa mgongo wa taifa, kilimo ni mojawapo, na kilimo kwa sababu wananchi wetu walio wengi ni wakulima na takribani wote ni wakulima wadogo wadogo.

Sasa Idara hii ya Kilimo inawajibu kuwasaidia wakulima kwa kuwapatia pembejeo za kilimo yakiwemo matrekta, mbegu bora ili waweze kuzalisha mpunga. Tukitilia maanani kuwa mpunga kwa maana ya mchele ni chakula kikuu cha wazanzibari. Lakini mchele mwingi tunaokula ni ule ambao unatoka nje ya Zanzibar.

Sasa hii ardhi ndogo tuliyonayo ya kilimo kama ingelikuwa inatumiwa vyema, nadhni ingeweza kuzalisha mchele wa kutosha kwa ajili ya matumizi ya ndani na tukaacha kuagizia mapembe ambayo ni mchele ambao mara nyingi umepitwa na wakati.

Lakini mara nyingi Idara hii ya Kilimo inapeleka matrekta kwa wakati ambo sio na mara nyengine wakulima wanalipa kabla na hatimae wakalimiwa wakati uliokwisha pita. Kwa hivyo, Idara baada ya kuwajengea uwezo wakulima inawarejesha nyuma wakulima katika kilimo chao cha mpunga.

Mhe. Spika, kulingana na hali ya nchi ilivyo hivi sasa, sasa hivi mwezi wa Januari ingelikuwa kwa kule Pemba watu tayari wameanza kusia mpunga. Lakini kutokana na mabadiliko ya hali ya nchi hata dalili ya mvua bado haijakuwepo na bado tunaendelea kutegemea kilimo hiki cha mpunga kwa kutegemea mvua zinazonyesha, hii itatukwaza katika kilimo hiki cha mpunga.

Kwa hivyo, Idara hii ya Kilimo ni lazima itafute mbinu mbadala ya kilimo cha mpunga, mojawapo ni hii tunayoiita ya umwagiliaji maji, nayo Mhe. Spika, hii ina matatizo yake kwa sababu matayarisho ya mabonde kwa ajili ya umwagiliaji yanahitaji fedha nyingi. Fedha ambazo sijui niseme hazipo. Kwa sababu mabonde ya kumwagilia yanahitaji kutengenezwa mambo mbali mbali.

Kwa mfano katika jimbo langu la Mtambile, kuna fedha kadhaa ambazo zimeshatumika. Kisima tayari kimechimbwa, matuta, miundombinu mengine yote imewekwa lakini zaidi ya mwaka wa tatu huu bonde hilo bado kilimo hicho hakijafanyika. Tatizo ni ukosefu wa umeme kwenye kisima. Kwa hivyo, ningeomba Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Ardhi Maji Makaazi na Nishati ili sehemu ile ipate maji ili wakulima waweze kulitumia lile bonde.

Mhe. Spika, kutopatiwa umeme kila pahala ni kuziangamiza mamilioni ya pesa za walipa kodi. Fedha za wahisani wanaosaidia, kwa sababu pale pahala pesa nyingi sana zimetumika na hivi sasa hakuna tija yoyote inayopatikana. Hii itakuwa kama ni ubadhirifu wa pesa.

Mhe. Spika, nije kidogo katika maliasili ikiwemo misitu. Pamoja na kuwa ujenzi wa nyumba kwa kutumia miti pole pole unatoweka, lakini bado ukataji wa miti kwa matumizi ya aina nyengine kwa ajili ya kuni na mengineyo, bado unaendelea. Na nishati mbadala ya kupikia si wengi ambao wanamiliki, sasa kukata miti ni kosa lakini kwa kuwa tunaishi lazima tule na ili tule lazima tupike na ili tupike tunahitaji *fuel* ambapo ama ni kuni, *gas* au umeme.

Wengi sisi watu wa vijijini tunachomiliki ni ama kutumia kuni au mkaa na hayo yote yanatokana na miti. Mti ambao tunasema usikatwe ovyo. Lakini kukata mti kwa kuni si kukata ovyo. Kwa sababu ni miongoni mwa matumizi sahihi, kwani mwanadamu lazima ale. Sasa sisi watu wa vijijini kwa kuwa

hatuli mpaka tutumie kuni kwa kupika, tuelimishwe namna gani tuweze kukata miti bila kuleta athari kubwa sana.

Mhe. Spika, nichangie kidogo kwenye biashara. Biashara kazi yake moja ni kuagiza na kusafirisha, lakini bahati nzuri hii kiwizara hapa wao nadhani hawaagizii, kazi yao wanasafirisha. Na zao kubwa wanalosafirisha ni karafuu, sijui haya yanayoagizwa mengine na taasisi zetu za kibiashara yana viwango kuingia nchini. Hili ni suala la mara kwa mara, kwa sababu nchi hii imegeuka kama ni jaa ya mali chakavu ambazo hazina viwango.

Kadhalika, Mhe. Spika, kuna biashara iliyotawala ya mali chakavu. Mali mbovu kuuzwa hapa, sijui inapelekwa wapi lakini halafu inatengenzwa vyombo kama masufuria na mambo mengineyo na inarudi hapa Zanzibar kwa matumizi. Masufuria ya aina hii mimi nina wasiwasi nayo, kuwa chuma kilichotumika au bati lilotumika tayari ilikuwa limechoka. Baada ya muda mchache yakipata moto masufuria yale yanaanza kutoboka na yanaleta athari. Hofu yangu magonjwa mengi yaliyotukumba ni kutokana na kutumia vyombo vinavyotengenezwa kwa mali chakavu. Sijui Wizara hii ina mpango gani wa kufanya utafiti kuona kuwa wananchi wetu hawaathiriki na hayo.

Mhe. Spika, kwa kuwa umenambia bado dakika mbili nafikiri zimemalizika, naunga mkono ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Ahsante sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo iliyo chini ya Mwenyekiti Mhe. Salmin Awadh Salmin ambae ni mwenyekiti mahiri wa kamati hii.

Kwanza nichukue fursa kumpongeza yeye na kamati yake. Hii ni kamati iliyo na wataalamu wengi.

Jengine ni kuiunga mkono ripoti yao kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, kwanza nataka ninukuu maneno kidogo hapa ya Idara ya Kilimo, yanayosema kwamba, "Idara ya Kilimo ndio kiini cha Wizara ya Kilimo na Maliasili ambayo imebeba dhima kubwa ya kuwasaidia wakulima waliopo hapa nchini wakiwemo wakulima wa mpunga kwa kuwapatia huduma mbali mbali zikiwemo utayarishaji wa mashamba na kuwapatia pembejeo, mbegu na mbolea".

Mhe. Spika, ukiachia maneno hayo tuje kwenye maoni ya maagizo ya kamati katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Maoni nambari mbili yamesema, "Kamati katika kutatua tatizo la uhaba wa wafanyakazi, wizara pamoja na

wizara inayohusika na ajira, inapaswa kutilia mkazo suala la uajiri wa wafanyakazi waliojaza nafasi za wafanyakazi waliostaafu na waliofikia kabla ya kushughulikiwa ajira mpya".
Mhe. Spika, na mimi nilikuwa ni mjumbe wa kamati hii, kwa hivyo tatizo hili nakumbuka tulikwenda tukaelezwa na watu wa wizara kuwa kuna tatizo la wafanyakazi ambao hufikia pahali wanastaafu lakini wa kushika nafasi zile hawapo. Na hasa ukizingatia wale pengine ndio wataalamu waliomo katika idara mbali mbali za Wizara hii ya Kilimo na Maliasili.

Sasa Mhe. Spika, hili ni tatizo, lakini wao wenyewe walisema kuwa wanapeleka maombi yao, lakini hufikia pahala maombi yale yanachukua muda mrefu hayapati majibu. Sasa kama Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio iliyobeba dhima kubwa katika kuwasaidia wakulima waliopo, kama wafanyakazi wanafika pahali kustaafu na wengine wakawa hawaajiriwi na pengine wale wanaostaafu ni wataalamu, hiyo dhima kubwa ya kuwasaidia hao wakulima itapatikana? Kwa hiyo Mhe. Spika, hili ni tatizo, katika wizara ambayo inashughulikia mambo ya uajiri.

Lakini pia la kushangaza ni kuwa katika mawizara au katika idara mbali mbali kuna wafanyakazi ambao kuna daftari wanajulikana muda wao wa kustaafu, sasa inakuwaje leo mpaka anafika muda mtu yule astaafu na pengine ni mtu wa taaluma muhimu akaondoka pale asiingie mwengine, pakabakia pengo lisilopungua pengine mwaka mzima. Mhe. Spika, hili ni tatizo na idara ya ajira itambue kuwa ina jukumu la kupeleka wafanyakazi pale, wanapostaafu wafanyakazi wa pale bila ya kuwachelewesha.

Mhe. Spika, jengine nije kwenye changamoto. Uhaba na uchakavu wa vitendea kazi vikiwemo matrekta na vifaa vyengine. Mheshimiwa, hapa katika kitengo hiki cha matrekta kipindi tulichokwenda kuona idara ile, kulikuwa kuna fundi mmoja tu, fundi wenyewe alikuwa ameshakuwa mzee tena hajiwezi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anambie idara hii sasa hivi ishapata watu wengine wa ziada, ili atakapoondoka huyu kushika nafasi hio?

Kwa sababu Mhe. Spika, tatizo watoto tunao waliojifunza mambo mbali mbali, lakini inafikia pahali mtu mmoja aliyepo pale anayetengeneza matrekta ndiye yupo peke yake, kitu ambacho hakiwezekani, kwa sababu ni kazi ya siku zote ile. Matrekta yenyewe yanayochukuliwa pengine hata hayana ubora. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, akija anieleze hapa kuwa tayari kushakuwa na watu wengine pale au ndio yule yule tuliyemkuta tangu kipindi kile?

Jengine Mhe. Spika, kuna bonde la Makombeni hapa ambalo serikali kwa ujumla imepoteza pesa nyingi kwa kushughulikia bonde lile. Lakini wenyewe

kumbe walikuwa hawako tayari kushughulikiwa katika bonde lile kwa suala zima la umwagiliaji maji. Kuna mabonde ambayo watu wana hamu wapatiwe kile chanzo na wenyewe watie nguvukazi yao, kutengenezewa mabonde yao katika njia ya umwagiliaji maji, ambacho ndio kilimo tunachokitegemea sasa hivi. Lakini leo pesa hizi zimepotezwa katika bonde hili hatimae bonde halijulikani mwaka gani litamalizika.

Kwa hivyo, mimi ningewaomba wizara kwanza kabla ya kuingia kwenye bonde wawashauri wakulima kama wako tayari waendelee na shughuli zile, kama hawako tayari mabonde mengine yako Mhe. Spika, ambayo watu wanategemea wapatiwe miundombinu ya umwagiliaji maji na kuendelea na shughuli zao.

Mhe. Spika, jengine nije katika Taasisi ya Utafiti na Kilimo. Taasisi inakabiliwa na ukosefu wa fedha za maendeleo. Mhe. Spika, hii ya utafiti ambayo ndio sekta muhimu, hicho kilimo kama hakina utafiti nadhani hakitofanikiwa na ni juzi tu, tulikuja hapa tukapitisha mswada wa Ugunduzi wa Mbegu. Kitu ambacho leo sekta hii inaambiwa ina uhaba wa fedha. Kwa hiyo, Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha, Wizara ya Kilimo na Maliasili aiangalie kwa jicho la huruma na aone kuwa wizara hii ndio wizara ambayo Wazanzibari wengi wamejiajiri.

Lakini jengine ni masuala ya uwekezaji. Kamati imeshauri mambo yafuatayo; Kamati imependekeza kukamilishwa miundombinu katika maeneo yanayokusudiwa kuwavutia wawekezaji kwa lengo la kuwa na kichocheo cha uwekezaji.

Mhe. Spika, kuna maeneo haya ya maeneo huru, lakini siku zote tunapokuja hili suala la kutayarishwa kwa *master plan* ya eneo la Fumba si ya leo tena. Sasa nimuombe Mhe. Waziri akija anambie hii *master plan* ya eneo la Fumba imefikia hatua gani. Kwa sababu na sisi wengine tunayo maeneo yetu, tunataka tutayarishiwe miundombinu hii ambayo wawekezaji watakuja.

La mwisho Mhe. Spika, kuna maagizo ya jumla hapa katika Sekta ya Kilimo. Katika utekelezaji, Wizara ya Kilimo na Maliasili imekubaliana na maelezo ya kamati ya hifadhi ya chakula kupewa kipaumbele. Hivyo, bajeti hii tayari fedha zimetengwa kwa ajili ya kukarabati maghala katika kuhifadhi hicho chakula. Bajeti hii Mhe. Spika, mimi sijajua ni bajeti ipi, kwa sababu hili nalo si tatizo la leo, siku zote tulipokuwa tukienda Wizara ya Kilimo kunakarabatiwa maghala haya wala hatujui hatma yake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, akija atwambie haya maghala yanayokarabatiwa yamefikia wapi.

Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia ripoti hizi za kamati.
Lakini kabla ya hapo Mhe. Spika, nimpongeze Mwenyekiti wa kamati hii kwa uwasilishaji wake mzuri na kwa umakini.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mchango mkubwa, kwa sababu nilidhani labda iko nafasi jioni nitaipata ili niweze kuja kuchangia vizuri.

Lakini hata hivyo, Mhe. Spika, niende katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Spika, ni vyema kuliangalia vizuri suala la malipo kwa wafanyakazi wa *over time* na yale malipo ya likizo. Kwani hii ndio nguvu kazi kwa watendaji wetu. Mhe. Spika, kutokuwalipa kwa wakati ni kupunguza utendaji katika kazi na ukizingatia hasa hali hii ya maisha kwa watu wetu.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Kilimo, na mimi miungane na kamati kwa ujumla kuwa wizara hii ndio inayobeba mzigo mkubwa. Kwa hivyo, hakuna budi idara hii kuangaliwa ipasavyo,.

Mhe. Spika, nikiendelea pia niseme kwamba namuomba Mhe. Waziri anaehusika na Wizara ya Fedha ajitahidi kuliangalia suala hili la ucheleweshwaji wa fedha katika idara hii. Kwani kutopata fedha mapema ndiko kunakosababisha utendaji mbovu wa kazi.

Mhe. Spika, nije katika suala la Matrekta kwa wakulima. Mwaka jana wakulima wengi walishindwa kulima kwa wakati, kutokana na ucheleweshwaji wa matrekta vijijini na pia kukukosa uburugaji kwa wakulima wetu kwa sababu ya matrekta. Lakini pia uhaba wa vitendea kazi nalo ni tatizo kubwa ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa. Kwa hivyo, naiomba wizara inayohusika ilishughulikie suala hili.

Mhe. Spika, pia wizara iangalie suala la kuwapatia mbegu wakulima kama vile mbolea pamoja na kuwapatia elimu ili waache kulima kwa mazoea. Lakini vile vile, Mhe. Spika, nikija katika Bonde la Makombeni ni vyema bonde hili kuwapatia elimu ya kilimo cha umwagiliaji, wananchi hao ili na wao waweze kunufaika na kilimo cha kisasa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba suala hili aliangalie kwa umakini Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nije katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Wizara hii ndio wanayobeba dhima kwa wageni wanaoingia katika nchi yetu. Kwa

hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aangalie sana wageni wanaoingia kufuata sheria za nchi yetu, na si kufanya kama wanavyotaka wao hapa nchini.

Mhe. Spika, pia niipongeze Wizara hii ya Biashara kwa kusimamia vyema suala la magendo ya karafuu. Kwani pia limepunguza kwa kiasi kikubwa usafirishaji wa magendo ya karafuu. Lakini vile vile nimuombe Mhe. Waziri, hili asiangalie kwa mijini tu, lakini ulinzi zaidi uwekwe vijijini na hata katika sehemu za bandari zilizoko vijijini. Huku ndiko hasa kunakofanywa magendo ya karafuu. Namuomba Mhe. Waziri, hili aliangalie kwa kina.

Mhe. Spika, pia serikali ihamasishe upandaji wa mikarafuu, kwa sababu sasa hivi mikarafuu mingi inatoweka hatujui sababu ni nini, licha ya kukatwa. Kwa hivyo, pia namuomba Mhe. Waziri ahamasishe upandaji wa mikarafuu ili tuweze kupata mikarafuu iliyo bora. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe: Spika: Mhe. Abdalla Moh'd Ali na wewe nakupa dakika kumi.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Spika, mimi naona hizo dakika kumi kwa leo zitakuwa nyingi. Kwa sababu nilijiandaa kwa kujua kwamba fursa sitoipata ya kutosha, isipokuwa nitakuwa na masuala machache tu.

Mhe. Spika, tumepokea ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambayo kwa kipindi cha miaka miwili na nusu na mimi nimeifanyia kazi.

Mhe. Spika, ripoti hii ilitoa maagizo na kwa ujumla maagizo hayo yamejibiwa na wizara husika. Isipokuwa kidogo tu nilikuwa nina mashaka na baadhi ya maelekezo ambayo wizara wameyatoa.

Mhe. Spika, ni agizo ambalo lilielekea Wizara ya Fedha, wanasema kwamba kulikuwa na agizo la mapato hasa *Airport*, yaani udhibiti wa mapato ya *Visa* uwanja wa ndege. Kamati iliagiza hatua za haraka zichukuliwe ili kudhibiti upotevu wa mapato hayo kwa kuweka mfumo wa malipo ambao hautaruhusu ulipaji wa fedha mkononi.

Mhe. Waziri katika kutoa ufafanuzi kuhusu suala hili, alijibu kwamba Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wameiandikia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar juu ya suala hili na kuiruhusu Benki ya *CRDB* kuweka mashine za kukusanyia mapato yatokanayo na *Visa* katika Uwanja wa ndege wa *Abeid Amani Karume, International Airport*. Hata hivyo, uongozi wa mamlaka ya viwanja vya ndege bado haujatoa ruhusa ya kuanza kwa uwekaji wa mashine hizo.

Mhe. Spika, mimi nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri, suala moja dogo tu. Hii sijui itakuwa ndio jawabu ya mwisho kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Mamlaka ya Uwanja wa Ndege haijatoa ruhusa. Mimi ninavyojua tuna serikali moja tu hapa, na ndio inayosimamia mamlaka zote hizi zilizopo katika nchi hii. Sasa sijui Mhe. Waziri atakuwa anatwambia nini, hii itakuwa ndio jawabu yake ya mwisho kwamba mamlaka haijatoa ruhusa au kutakuwa na jawabu nyengine kuhusu suala hili.Suala jengine ni kwamba ninavyojua sisi tuna *local bank* na Benki yetu hapa tunataka ikue zaidi na ifaidike. Benki hiyo ni *PBZ.* Sasa nilitaka maelezo kidogo kutoka kwa Mhe. Waziri. Kulikuwa na sifa fulani iliyovutia hata tukaipatia *CRDB tender* hii ya kuweka hizo mashine za kukusanyia mapato.

Mhe. Spika, niende tena kidogo katika Wizara ya Kilimo na Maliasili. Wizara ya Kilimo nayo katika kujibu hoja zake ilipewa agizo nambari 14, agizo hili linasema kwamba:

Kituo hatua	"Kwa kuwa wafadhili yaani Wakorea wamesita kumaliza ujenzi wa cha Usarifu wa Mazao Kizimbani ni vyema kwa serikali kuchukua ya kumaliza ujenzi huo"

Sasa imani yangu ni kwamba kulikuwa kuna wafadhili waliokubali kuliendeleza jengo hili mpaka kumalizika kwake. Lakini kwa taarifa hii itakuwa jengo hili limesita kwa sababu moja au nyingine ambazo mimi sizifahamu. Nina imani kwamba Wajumbe wengine wa Baraza hili hawalifahamu. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri akatufahamisha ni sababu zipi zilizotokea hata ikasababisha wafadhili hawa kuondoka katika ufadhili wao wa kulimaliza jengo hili.

Lakini jengine niende kwenye Shirika la Bima. Unajua vipando vimeongezeka kwa wingi na Shirika la Bima wanasifia kwamba wamekwenda mpaka asilimia mia moja na kuongezeka. Lakini hivi sasa kuna malalamiko makubwa ya ongezeko la bima hasa *ordinary,* bima zile za kina sisi wadogo wadogo.

Mhe. Spika, ningetaka kujua je, ni kwa sababu zipi zilizopelekea hata bima mara hii ikapanda asilimia zaidi ya mia moja? Labda wakati wa upandishaji wa bei, wanaishirikisha na idara husika ya ukusanyaji wa mapato au wanapanga wao wenyewe pake yao? Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe: Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni. Bahati nzuri leo sina maombi ya kumpenyeza mtu yoyote kwenye orodha ya wachangiaji. Kwa hivyo, tunakomea hapa. Niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa na jioni tutakwenda kwenye majumuisho moja kwa

moja. Basi tusitishe shughuli zetu na niakhirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6: 50 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe.Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili limehusu sekta mbali mbali na mawaziri husika wa sekta hizo wapo ningeomba waendelee na shughuli hiyo na mimi nichangie pale tu itakapofika zamu ya Wizara ya Kilimo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwa kuwapongeza na kuwashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa michango ambayo wametupa mimi na watendaji wangu Wizara ya Fedha. Kwa kweli, imeweza kutusaidia sana na itaendelea kutusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nithubutu kusema mbele ya Baraza lako tukufu kwamba michango ilikuwa ni mingi wengine walipata nafasi ya kuchangia na wengine walipata nafasi ya kunitumia kwa maandishi. Nataka niahidi kwamba mimi na watendaji wangu tumeichukuwa michango yote na tutaifanyia kazi kadiri ya uwezo tulionao. Namuomba sana Mwenyezi Mungu atujaalie kutupa uhai na uzima wa afya ili tuweze kutekeleza vyema majukumu yetu kwa faida ya nchi yetu na wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuokoa muda michango ilikuwa ni mingi na mimi nimeijumuisha kwa pamoja.

La kwanza ambalo lililozungumzwa na Wajumbe karibu wengi lilikuwa ni suala la shughuli za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Suala la shughuli za Bima na Suala la shughuli za *ZIPA*. Kwa maana kwamba wananchi wengi hawana taaluma za shughuli za hivi vitengo vitatu, na Wajumbe wengi waliomba kwamba ni vyema vitengo hivi vikatoa taaluma vikawaelezea wananchi wetu shughuli wanazozifanya na faida zake ili wananchi wetu wengi waweze kujiunga na shughuli zao. Hilo tumelipokea Mhe. Mwenyekiti, na tutalifanyia kazi ili wananchi waweze kutufahamu tunafanya nini.

Lakini vile vile, Wajumbe wameeleza kwamba sambamba na kutoa elimu katika Sekta ya Bima kuna ushindani mkubwa sana na ni kweli kuna vyombo vingi sana vinatoa bima kama chombo chetu cha bima. Kwa hivyo, imetakiwa

bima ijiandae ili kuweza kukabiliana na ushindani. Tumelipokea na ndio maana mwenzako anapokukaribia wewe unaongeza mbio za kwenda zaidi. Sisi bima tunaongeza *product* nyengine mpya ili wanachama wetu waweze kuvutika na bima yetu.
Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo limezungumzwa na Wajumbe wako wengi ni suala la kuiongezea mtaji Benki ya Watu wa Zanzibar. Ni kweli sio kwamba mtaji walionao ni mdogo. Nataka niiweke sawa hii. Tunapaswa kuiongezea mtaji kama serikali ili waweze kufanya biashara nzuri zaidi. Kwa sababu mtaji unapokuwa mkubwa na biashara unaifanya vizuri zaidi.

Hili tumelipokea na nadhani Mhe. Mwenyekiti, nataka niliarifu Baraza lako tukufu kwamba tumeshakaa kama vikao vitatu vinne kuanzia uongozi wa *PBZ* pamoja na Bodi ya *PBZ* kulizungumzia suala hili. Kinachotukwanza katika muda huu hali yetu ya fedha kidogo ni ndogo, lakini tumewaahidi hali itakapokuwa nzuri tutawaongeza mtaji ili waweze kufanya biashara vizuri zaidi.

Suala jengine ambalo limezungumziwa ni suala zima la kuziba mianya ya uvujaji wa mapato kwa upande wa *ZRB*. Hatua tumezichukuwa nimeeleza katika taarifa yangu niliyosoma asubuhi kwamba hatua tumeanza kuzichukuwa na tutazidi kuzichukuwa zaidi.

Lakini nataka nieleze katika eneo hili Waheshimiwa Wajumbe binaadamu ana akili sana, wewe ukitumia mbinu hii na yeye anatumia mbinu ile. Kwa hivyo, hili litakuwa ni zoezi la kila siku na sisi tutapambana nalo na tutakwenda nalo mpaka watu wote watakuwa wanaheshimu sheria na taratibu za nchi. Tumeelezwa vile vile tupambane na magendo ya mafuta. Sasa hivi tunakwenda kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama, tunajitahidi. Tumekamata mafuta mengi na tukikamata mafuta hayo sisi tunayauza na pesa ni zetu.

Tunatoa zawadi sasa hivi kwa mtu yoyote ataetoa taarifa kwamba kuna chombo fulani au kuna mtu fulani anafanya magendo ya mafuta. Kwa hivyo, hiyo ni motisha ili kuweza kupata taarifa.

Kuna suala lilielezwa hapa kwamba *TRA* hawakuweza kufikia lengo kwa sababu mwanzo tulitoa misamaha ya 80% ili ishirini ilipwe na baadae *TRA* wakapelekewa misamaha ya asilimia 85% na 15 ndio ilipwe. Ni kweli misamahaa ya 20% ilibakia pale pale. Lakini tulichokiona baadae kwamba tayari wale wawekezaji wanalipa asilimia 5% *ZIPA*.

Kwa hivyo, tukaona tukiiacha ile ya *ZIPA* 5% na 20% itakuwa ni 25%. Kwa hiyo, tukaona twende nao kidogo kidogo kwa sababu walikuwa wanalipa 5%.

Kwa hivyo, sasa wanataka kuiongeza ifike 20%. Kwa hiyo, 5% iende *ZIPA* na 15% iende *TRA*. Ki ukweli kwamba mapato yale yote yamekuja serikalini asilimia ile 20% yote imekuja serikalini, lakini 15% imekwenda *TRA* na 5% imekwenda *ZIPA*. Kwa hivyo, hicho ndicho kilichotokea.
Mhe. Mwenyekiti, limekuja wazo kwamba kina mama kufunguliwa benki yao. Bahati nzuri Mhe. Waziri, anaeshughulika na mambo haya hayupo sasa hivi. Lakini nataka niseme tu kwamba tumeanza sio kwamba tumekaa kimya. Lakini tuna *check list* ambayo lazima tuikamilishe kabla hatujaifungua hiyo benki.

1. *Check list* ya kwanza lazima tuangalie nani na nani watakaoweza kuchangia ile bilioni kumi na sita.

2. Tunaangalia shughuli hizi tutaziendesha katika majengo gani, kama tunavyofahamu masuala ya benki yako mjini. Benki hasa ukitaka ifanye kazi lazima makao makuu yake yaweko mjini.Kwa hivyo, tunaangalia wapi tutapata majengo ndani ya mji wetu ili kuwezesha kuendesha shughuli za benki ya wanawake.

3. Tunaangalia wataalamu watakaoendesha hii shughuli ya benki, ukimleta mpya *from school* hawezi. Lazima uwalete hawa wakuukuu kwanza waanze kufanyakazi halafu na wale wapya wanaingia wanakwenda nao sambamba.

Kwa hivyo, tuna *check list* tunayojaribu kuiangalia na hatimae tukifikia muafaka kuifungua ni mara moja tu wala haitochukuwa zaidi ya miezi mitatu. Lakini kukamilisha hizi taratibu ndio inaweza ikachukuwa muda kidogo.

Kwa hivyo, nakuombeni Waheshimiwa kwamba bado tunaendelea na hasa kile kigezo cha bilioni kumi na sita. Mwanzo wakati Waziri wa Uwezeshaji alikuwa Mhe. Haroun Ali Suleiman, tulikuwa tunataka tuzichukuwe na *SACCOS* tuziingize. Sasa tunataka kuendelea na mazungumzo yale yale kwamba mbali na wanawake na *SACCOS* iweze kuingia tuliwahi kulipendekeza jina. Kwa hivyo, jina hilo halijapata mushkeli. Kwa hivyo, maani kwamba jina hili litaendelea kuwepo ili kuzi *include* zile *SACCOS*.

Kulikuwa na wazo kwamba mimi na Mhe. Wazir, mwenzangu wa Miundombinu tupite Bandarini na Uwanja wa Ndege kuangalia matatizo yetu yanayowakwaza wananchi na serikali kwa ujumla.

Nataka nithubutu kusema kwamba Waziri wa Miundombinu alieondoka tuliifanya kazi hiyo mimi na yeye. Tulipita Bandarini, tukapita *Air Port* tukarudia tena. Waziri huyu alokuja sasa hivi sijafanya kazi hiyo na yeye.

Lakini nimerudia tena peke yangu, juzi tu nilipita *Air Port* peke yangu kuangalia kuna kazi tumeambiwa tuzifanye, nikawa naziangalia.

Kwa hivyo, hili wazo tunalifanya na tumegundua kuwa kuna matatizo, matatizo mengine yanaambatana na ubinaadamu, matatizo mengine yanaambatana na jengo lenyewe kwa upande wa *Air Port*. Lakini yote haya tunayafanyia kazi.

Kulikuwa na suala jengine ambalo tumeulizwa mgawanyo wa fedha, hili nitaliweka mwisho. Suala jengine lilikuwa sambamba na benki ya wanawake lilikuwa suala ya kuanzisha benki ya Kilimo. Mimi nataka niseme tu. Ukitaka kuanzisha Benki ya Wanawake na wakati huo huo ukaanzisha na ya Kilimo, kwa hali yetu ya kifedha hatutaweza. Lazima tuanzishe moja halafu moja tuwaombe *PBZ* wafungue dirisha.

Hili mimi nimelipokea kwa malengo ya kuzungumza na wenzetu wa Benki ya Watu wa Zanzibar waangalie uwezekano wa kufungua dirisha kuanza na dirisha. Kama wenzetu Tanzania Bara walivyofanya walianza na dirisha hawakuanza na Benki ya Kilimo .

Kwa hivyo, na sisi tuanze kuzungumzia kuanzisha dirisha la kilimo ili liweze kutoa nafasi kwa wakulima na kuweza kukopa. Kulikuwa na suala ambalo swahibu yangu pale aliliuliza sana na najua ananiuliza kila akiniona suala la muekezaji huyu wa *Cristal Hotel*, aliekalia eneo la mwananchi mzalendo. Hili suala hatujaliwacha Mhe. Hamza Hassan Juma. Mimi na Mhe. Waziri, mwenye dhamana ya Ardhi tumekaa. Tatizo liliopo hapa hii ardhi ina *double location*.

Sasa tukifika hapo hiyo kazi inakuwa si ya Waziri tena wa Fedha. Tumelizungumza na tayari tumeshawaandikia wenzetu *ZIPA* mimi na Mhe. Waziri wa Ardhi, ili *ZIPA* watuletee maelezo ya kina halafu tufanye kikao cha pamoja kati ya Fedha, Ardhi na *ZIPA*, tuone tufanye maamuzi gani. Uamuzi wowote utakaofanyika unaweza usilete furaha kwa pande zote. Kwa sababu ya hiyo *double location*. Kwa hivyo, nakuona sana Mhe. Hamza Hassan Juma, vuta subira kidogo taarifa hii ije kutoka *ZIPA*. Na tumeshakubaliana na Waziri wa Ardhi kuweka kikao cha pamoja.

Muekezaji Magembe huyu tumemtafuta sana tukaambiwa yuko nje ya nchi. Sasa tumeambiwa yuko kwao Shinyanga, tumeomba tuletewe yule ambaye anaendesha shughuli zake pale tuweze kulikamilisha hili suala la madai. Na yeye tumsikilize upande wake. Kwa hivyo, nalo si kama tumelikalia tunalifanyia kazi.

Niliulizwa vile vile, kutoa misamaha. Labda nikupe tu takwimu ya haraka haraka, kuanzia mwezi wa Julai mpaka mwezi wa Novemba, Disemba misamaha iliyotoka ni bilioni nane. Katika hizo bilioni nane za msamaha zaidi ya bilioni moja ni misamaha ya mradi wetu wa serikali wa *Air Port*.

Nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe mwende pale mkatizame mradi wa kiwanda cha Maziwa. Kwa kweli ule mradi umeleta mashine nzito sana na misamaha yake ya kodi ilikuwa zaidi ya bilioni mbili. Na pale kuna ajira zitapatikana kwa vijana wetu zaidi ya mia moja. Kwa hivyo, hii misamaha tunayoita si kwamba inatoka tu mingi ina faida na nchi yetu.

Ukiachilia mbali ile misamaha ambayo kwa mujibu wa *status* yake mtu anaruhusiwa kupewa msamaha wa kodi ya gari. Nayo vile vile, inasaidia ili ile gari anapata kutumia kumuwezesha katika shughuli za kitaifa.

Kwa hivyo, hilo ndilo ambalo hadi sasa tunajaribu sana kadiri wa uwezo wetu. Tumeanza kuizungumzia sheria yetu ya *ZIPA* sasa hivi ina marekebisho makubwa sana. Kuna misingi ambayo hatuoni sababu nyengine ya kutoa *exemption* kwa mfano tunapozungumza *exemption during for construction* hatuoni sababu tena kutoa *exemption*. Kwa hivyo, tunajaribu sana kuipunguza hii misamaha.

Kuna suala jengine liliulizwa kwamba 90% za fedha za *TRA* wameweza kukusanya na makadirio yao waliokusanya ni 90%. Nikaulizwa nafikiri na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mbona mgawano hatuuoni ukafikia 90%. Hapa Mwenyekiti, nataka Wajumbe wako wanisikilize kidogo kwa sababu kutakuwa kuna hesabu ili twende sambamba na namba.

Nilisema bilioni mia moja na hamsini na tano ndizo zinazokusanywa na *TRA* na *ZRB* kwa mwaka. Kwa hivyo, nikasema yale mapato yote ya *ZRB* yanakwenda kwenye mishahara. Tunachobakiwa nacho sasa ni mapato ya *TRA*. Sasa tuangalie *TRA. TRA* wanakusanya bilioni mia moja na arubaini na saba kwa mwaka. Miezi sita ya mwanzo *TRA* amekusanya bilioni sitini na tano nukta tatu. Sijui kama mnaziandika hizo *data* hiki tulichogawana kidogo kidogo ambapo mlipokwenda Waheshimiwa Wajumbe mkaona kila wizara inapiga kelele kwamba pesa sijatiliwa. Hichi kidogo kidogo tulichogawana kwa miezi sita ni bilioni sitini na tatu.

Kwa hivyo, kama kuna bakaa hapa ni bilioni mbili. Bilioni mbili mshahara haukuchukuwa bilioni sabiini na tano kwa miezi sita umechukuwa bilioni sabiini na saba hali ndio hiyo.Huwezi ukasema kwamba *TRA* wanakusanya 90% na *reflection* ile ionekane ndani ya taasisi zetu. Taasisi zetu mahitaji yao kidogo ni makubwa ukilinganisha na makusanyo ya *TRA* peke yao. Kwa

hivyo, sisi katika *OC* tumetumia 63 bilioni na *TRA* katupa 65 bilioni hiyo ndio hali.
Lakini hapa wala tusivunjike moyo Waheshimiwa Wajumbe ukitizama hizi takwim zinasema matumizi yetu ya kawaida ni asilimia 98% ya makadirio ya miezi sita na 46% ya makadirio ya mwaka. Kwa hivyo, hatuko mbali *expenditure* yetu ambayo tumeipanga kwa miezi sita ilikuwa ni 50% na tumetumia 46% kwenye *recurrent.* Tatizo kubwa ambalo tumeligundua ni kwenye *development*.

Kwenye *development* katika kipindi cha miezi sita baada ya kupata 50%, tumepata 19% *development* ndio ambayo ina matatizo. Kwa hivyo, hata kufanya kwetu mahesabu katika kutafuta pesa na kuongeza. Tunapaswa kuongeza katika miradi yetu ya maendeleo. Kiujumla *expenditure* yote ya maendeleo na *recurrent* kwa miezi sita ni 97% , kwa mwaka tuko kwenye 41%. Kwa hivyo, hata ukizitizama hizi hesabu bado tuko katika *position* sio mbaya.

Lakini Waheshimiwa Wajumbe mmepata ile semina ya *PBB.* Sasa hivi nimeenda katika taasisi kuangalia utendaji wa kazi msiulize pesa tu zilizoingia haitakusaidieni. *The outcome* ilichopatikana na nataka nikupeni *tip* nyengine, Waheshimiwa Wajumbe msitafute *vote* ya jumla mnakwenda mnauliza *recurrent* mmepeta kiasi gani hampati kitu. Niende fungu kwa fungu kama mlivyotupitishia hapa mtapata na mtajua ukweli.

Lakini la mwisho katika eneo hili Waheshimiwa Wajumbe Waziri wa Fedha na Wizara ya Fedha hawawagaii wizara mafungu kwa mafungu. Mimi ninawapa c*eiling* yao tu wizara zote, *ceiling* yako ya *OC* shilingi 400 milioni hizo hapo yeye ndie anayekwenda kugawa, akiona kama kuna kitu ni *priority* anapaswa kukiwekea pesa pale na ndio siku zote nataka nikwambieni umeme hauwekewi pesa. Taasisi zote hawaweki pesa za umeme isipokuwa wale ambao wana mita, Taasisi za Serikali hawaweki kwa sababu wanaona si muhimu, madhali serikali haukatwi.

Taasisi za serikali tunadaiwa na *ZECO* zaidi ya shilingi 12 bilioni, wanajijua wenyewe mawaziri wizara zao zinazodaiwa. Nimepiga kelele kila siku nawaambia *ZECO* wawekeeni mita tuache vituo vya maji na afya sehemu za hospitali na Vituo vya Afya, lakini mote nimepiga kelele wawekewe mita, wakiwekewa mita wataweka fungu la umeme.

Kwa hivyo, mnapokwenda kuangalia msiangalie kwamba fedha hazijapatikana tu, angalieni na vile vifungu tulivyovipitisha hapa. Tumepitisha vifungu vya umeme hapa shilingi kadhaa na sisi tunatumia umeme kila siku, kwa nini hatuweki fungu la umeme, tuwaulizeni watendaji,

mkija mkiwauliza mawaziri hapa mtawasulubu *for nothing*, lakini kwenye kamati ndio mnatakiwa muwaulize watendaji hasa tena muwaulize kweli kweli.

Vile vile, nilisema kwamba mapato yameongezeka, lakini na matumizi yetu yamekua. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kaniuliza bahati mbaya hayupo, alitaka kujua matumizi yepi yaliyoongezeka. Labda nimfahamishe kidogo kwa faida ya Wajumbe wako Mhe. Mwenyekiti.

Idadi ya wananchi wa Zanzibar inakua kwa asilimia 2.8 kila mwaka, tuna maana gani? Tuna maana kwamba kila mwaka kuna watu elfu arobaini na kidogo wanaongezeka hapa Zanzibar, huwezi ukawaacha watu hao usiwape matumizi, huwezi ukawaacha wasiongeze kunywa maji, huwezi ukawaacha watu wasiende hospitali kupata huduma za afya. Kwa hivyo, matumizi yetu yanaongezeka. Kuna hii wanayoita *age cohort*, ukizaa huku kule wengine wanaingia katika *age* nyengine.

Jana alikuwa na miaka sita, alikuwa yuko nyumbani na mama, leo ana miaka saba umpeleke skuli tunaongezeka, tunatanuka sio sababu ya kutanuka maidara, maidara yakitanuka na kama tunaajiri zaidi pale ndio tutaongeza *expenditure*. Lakini maidara yakitanuka kama tunafanya *alteration* kuchukua watendaji huku ukawapeleka huku, wakaitumikia ile idara, *expenditure* itakayoongezeka ni ndogo mno, ni ile ya *administration* tu. Kwa sababu watendaji ni wale wale umewapeleka kule na mishahara yao ndio ile ile.

Kwa hivyo, tunapotanuka huduma zetu, tunatanuka kwa sababu tunakua na hii sio sisi tu ndugu zangu, ni dunia nzima, *unless* kwa zile nchi ambazo zina *negative growth*. Lakini sisi tuna *positive growth*, lazima kila mwaka 40 na kidogo tutaongezeka, 40 na kidogo tutaongezeka, elfu hiyo tunaongezeka, nisije nikaulizwa wengine wamekufa *no*. Hii ni *growth rate* ambayo ina-*consider Immigration* na inayo-*consider death*, hii ni *net growth rate*, imesha-*take into consideration* vifo, imesha-*take into consideration immigration*, ni *net* kila mwaka wanaongezeka.

Kwa hivyo, mahitaji yetu yataongezeka tu na wala tusiogope mahitaji yakiongezeka, ndio pale niliposema kwamba, lazima tutumie kwa uangalifu. Leo unakwenda maofisini ikifika saa tisa na nusu ukitembea unaweza ukakuta mataa yanawaka tu, mafeni yanakwenda tu, hakuna watu wa kuyazima yale au kuzima zile taa. Lazima tutumie kwa uangalifu ili tupunguze haya matumizi ninayozungumza.

Mhe. Mwenyekiti, hata majumbani mwetu unaweza ukakuta bomba linavuja hatuna habari maji yanatoka tu, yanatoka tu, wewe huna mita, lakini kule

kuna *production* ambayo inakwenda ni *wastage*. Kwa hivyo, hayo ni matumizi yetu Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, hayupo lakini nimeweza kumsaidia.

Vile vile, alitaka kujua *status* yetu ya shilingi 18 bilioni zile za *PAYE*. Sisi tumemuandikia toka mwaka jana huyu aliyekuwa Waziri wa Fedha Bara marehemu, baada ya kudaiwa shilingi 38 bilioni *ZECO*, anadaiwa na *TANESCO*, tukasema *ZECO* anadaiwa na *TANESCO* fedha hizo na *ZECO* anaidai SMZ shilingi 12 bilioni, tukasema sisi shilingi 18 bilioni tunazowadai pesa zetu za *PAYE* wachukue wawalipe *TANESCO*, tunajua tumeshawaandikia na kwa bahati nzuri mwenyekiti wa kikao kile akasema fuateni taratibu tumefuata taratibu za kuwaandikia.

Bahati nzuri yule mwenzetu tena baada ya muda akaanza kuumwa masikini, marehemu ameondoka. Tumekubaliana ofisini kwamba tunampa muda kidogo kama siku mbili tatu wiki moja waziri mpya atulie ofisini tukumbushie barua hii. Kwa sababu bado *TANESCO* wanawadai *ZECO*, lakini sisi pesa hizo tumezipeleka kupunguza deni letu la umeme.

Miradi mikubwa na mipya ni vyema wizara husika wakae pamoja. Mimi nakubaliana na nyinyi Waheshimiwa moja kwa moja. Miradi mikubwa lazima tukae pamoja ili tuweze kuitekeleza kwa pamoja. Na hili nadhani *sector ministry* kwa huu utaratibu ambao ninauona sasa hivi ndivyo wanavyolifanya. Sijui huko nyuma walikuwa wakifanyaje, lakini kwa sasa naona tunakwenda vizuri tu na mimi mwenyewe huwa nashirikishwa kwa baadhi ya miradi mikubwa na tunakuwa tunafanya mazungumzo.

Hata jana tulikuwa tuna kikao cha mradi mmoja mkubwa, sote tuliohusika tulikuwa tunajadiliana. Kwa hivyo, hili nalikubali moja kwa moja na tutalisisitiza. Na kwa sasa Tume ya Mipango haiko tena chini ya Wizara ya Fedha ambaye ndie msimamizi wa Miradi ya Maendeleo. Tume ya Mipango iko chini ya Ikulu na Waziri mwenye dhamana yupo anatusikia na tutashirikiana nae. Yeye sasa ndie atakayekuwa anatoa barua kumualika nani anayehusika kwenye mradi fulani.

Kwa nini Maafisa Wadhamini Pemba hawashirikishwi katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa Pemba. Hili ni tatizo sugu hata mimi sijui kwa nini. Naelewa kwamba *development budget* mwenye dhamana ya moja kwa moja ni Katibu Mkuu. Lakini haina maana kwamba ukimshirikisha Afisa Mdhamini Pemba atachukua madaraka yako.

Nimelipokea na nitamuomba sana Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini Waziri husika wa Miradi ya Maendeleo awaandikie Makatibu Wakuu kupitia Tume

yake kwamba wawashirikishe na Maafisa Wadhamini katika miradi inayotekelezwa Pemba. Hata vikao wajue kipi kinachoendelea. Kwa hivyo, hili tumelipokea ndugu zanguni na tutalifanyia kazi kwa pamoja.

Master plan ya Fumba imefikia wapi? Serikali tayari imeshatoa shilingi milioni 150, eneo limeshapimwa, *design* ya *master plan* iko tayari, sasa hivi tunakwenda katika ile *detail design, alignment* ya barabara zote ziko tayari. Na leo mchana nilikuwa na wawekezaji nao vile vile nililiuza lile eneo ili waweze kutusaidia.Tukibahatika kwa sababu pale panahitajiwa fedha nyingi sana, ujenzi wa barabara, kupeleka maji, kupeleka umeme, halafu na kujenga *industrial sheds,* tunaendelea kulifanyia kazi.

Nyumba na mashamba kwa ajili ya Kiwanda cha Sukari. Ni kweli kulikuwa kuna hekta kama 2,700 wananchi wanazo na kulikuwa kuna nyumba kama 150 zinakaliwa na wananchi. Tayari tumeshaongea na Mkoa, kuna Kamati Maalum, mimi, Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Naikumbuka hiyo Kamati tumeambiwa kwa pamoja tulisimamie. Kulikuwa kuna matatizo mengi, nashukuru na nawashukuru sana wananchi wa maeneo yale. Kulikuwa kuna magari yanapita pale ya michanga wanaharibu zile barabara, wanaharibu miwa, na ule moto ulikuwa unaonekana kama ni dalili za watu wanaovuta sigara na magari yanakuwa yanatupa tu. Sasa hivi nashukuru sana magari yale hayapiti tena.

Lakini na haya mengine tumeanza ku-*list* nyumba zile anayekaa. Kulikuwa kuna mikataba wamepewa kutumia eneo lile yaani kulima mpaka hapo yatakapotakiwa. Hiyo, mikataba tayari tumeshaiona kwa wale ambao waliopewa, tukawapa nafasi wamalize kuvuna mazao yao ili warejeshe katika kiwanda ile ardhi pamoja na hizo nyumba. Kwa hivyo, tunakwenda nalo hili na nakuombeni Waheshimiwa kila tutakapopata zile nyumba tutawakabidhi kiwanda, kila tutakapopata eneo la ardhi tutakabidhi kiwanda.

Niliulizwa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege haijatoa ruhusa. Hii itakuwa jibu la mwisho? Si la mwisho. Lakini katika *good governance* lazima uweze kuomba *authority* ya pale. Sisi tumetekeleza wajibu wetu tumeiomba Mamlaka moja kwa moja baadae tukagundua kwamba tulifanya makosa tukaiomba Wizara. Wizara nao wakawaandikia Mamlaka kuweka zile mashine za *POS*. Bado Mamlaka haijajibu, tumekubaliana na Waziri husika kwamba tuwakumbushe tena kwa sababu hili jambo ni la taifa, si la kwangu mimi Waziri wa Fedha wala si la Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Na sambamba na hili tukaulizwa tena kwa nini tumewapa *CRDB* badala ya kuwapa *PBZ.* Sisi sote ni wateja wa *PBZ,* mimi mmoja nina akaunti pale *PBZ.* Lakini utakubaliana na mimi kwamba *PBZ* hawana *visa* wala hawana *master card.* Na wale wageni wanapokuja nje kule wanakuja na *visa* na *master card.* Ndio kwa maana tumekubaliana katika *interim time (time* ya mpito) wasimamie *CRDB* kuweka mashine na kufanya zile kazi, baadae *PBZ* watakapokuwa tayari waje waisimamie ile *system* wao. Lakini akaunti ile pesa zikiingia tunaziona moja kwa moja, tunaziweka mtandao wa kuweza kuona mpaka *PBZ* kwenye akaunti yetu wataziona ni kiasi gani kilichoingia leo kwa ajili ya *visa.*

Lakini bahati mbaya bado hatujapata jibu, na mimi kama Waziri mwenye dhamana ya kodi, lakini sina dhamana ya kuingia kila nyumba ya mtu na kukusanya kodi. Bado tumesema tukumbushe ili wenzetu waone umuhimu wake.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niipongeze sana Kamati. Mwaka jana wakati tulipokuwa tunalielezea suala la *E-Government* uamuzi uliotolewa na kukubalika na kikao hiki ni kwamba Kamati ya Sekta iende, basi ikaufanyie kazi huu mradi.

Kwa sababu hoja ile mliileta Wizara ya Fedha, Kamati ya Sekta ni Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo nilivyofahamu mimi. Kwa hivyo, Kamati imekuja imeuliza, imepata taarifa, imeona ilichoona. Ripoti yao ya Kamati imewasilishwa na Mwenyekiti wangu Salmin Awadh Salmin, anasema muda ulikuwa mdogo. Kwa hivyo, anaomba Kamati Maalum sikumsikia akiomba Kamati Teule.

Anaomba Kamati Maalum ili ikafanye kazi kwa ajili ya mradi huu. Kwa utaratibu wako Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo nalo, unda Kamati Maalum kwa utaratibu utakaouona wewe unafaa, waende wakautazame mradi. Na katika dondoo ambazo Mwenyekiti wa Kamati yangu amezileta nadhani atanisaidia sana. Huu mradi wa *E-Government* historia yake imeanza mwaka 2004. Watu wengine wanafikiria kwamba mradi huu umeanza jana na leo tu, haukuanza jana na leo umeanza mwaka 2004, ile *concept,* ile *analysis* yake. Na *document* ya mwanzo ya mwaka 2004 bahati nzuri imetiwa saini na ndugu yangu Raphael ambaye leo ni Katibu Mkuu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Huu mradi ni mzuri, lakini kwa sababu ya upya wake hatujauelewa wengi wetu. Mhe. Hamza Hassan Juma, amesema vizuri sana, lakini mimi naamini baada ya miaka minne mitano ijayo tutakuja sote hapa kusema kwamba huu

mradi umetusaidia. Hayo matatizo aliyoyasema Mhe. Asha Bakari Makame, yataondoka.

Leo unataka *internet*, mimi huwasikia vijana pale "iko *slow*, iko *slow"* itaondoka, itapunguza hata gharama za wale watumiaji wa *internet.* Itatupunguzia sisi mawasiliano yetu ya ndani - ndani ya serikali. Leo nikitaka kumpigia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lazima nipitie kwenye *TTCL* au kwenye *Zantel*, pesa inakwenda. Lakini nikimaliza mkongo huo zile alizozitaja Mhe. Haji Omar Kheir *unit* 87, tutataka mwaka kesho nusu yake watakuwa wameshaunganisha ndani, tutaona gharama zitapungua hatutalipa chochote sisi mawasiliano yetu ya ndani.

Kwa hivyo, upya wa huu mradi mimi nakubaliana na Mhe. Hamza Hassan Jum, ndio ninalogomba. Lakini vile vile, nakubaliana na Wajumbe wengi kwamba itolewe taaluma juu ya huu mradi *E-Government.* Na mradi huu ukipata ile ripoti ambayo imetiwa saini na Ndugu Raphael ile ni *concept report.* Kuna *chart* pale inaeleza jinsi itakavyounganisha taasisi nyingi.

Leo kuna watu wa vitambulisho wako peke yao wananing'inia, leo kuna watu wa ardhi kule wananing'inia wako peke yao, kuna watu hawa wanaoandikisha vifo na vizazi wataning'inia nao peke yao. Sasa ukitizama ile *chart* inawaunganisha kwenye huu Mkongo wa Taifa. Sasa mimi nasema tu kwamba taaluma inahitajika juu ya mkongo huu. Na Mhe. Mwenyekiti, kama Mwenyekiti wangu alivyoomba ni matatizo, utaratibu utaupanga wewe, hadudirejea wape wewe, *time* ya kuanza kazi utapanga wewe Mwenyekiti ukishirikiana na Mhe. Spika. Mimi nawakaribisha na watatusaidia sana.

Na Mwenyekiti katika ripoti yake alisema kwamba watu wanakata ile mikongo licha ya kwamba kuna kile kibao cha kuonesha pana Mkongo wa Taifa. Sasa hiyo ni makusudi tu si kwamba mtu hajui. Tutaelimishana na tutasaidiana kuelimishana.

Nataka kumalizia Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema kwamba nawashukuru Wajumbe wote kwa mashirikiano waliyonipa na michango yenu tutaifanyia kazi. Sikuweza kuijibu yote kutokana na wakati, lakini tutaifanyia kazi, yale ambayo yanayohusu moja kwa moja Wizarani kwangu tutayafanyia kazi, na yale yanayohusu kushirikiana na wenzangu kama vile nilivyosema Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tutayafanyia kazi Ikulu, tutafanya kazi kwa mashirikiano. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kunipa fursa ya kutoa utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, tunamshukuru sana kwa maelezo yake marefu ambayo kwa kweli yametusaidia sana. Sasa nilikuwa na mambo machache kidogo nilikuwa nataka atusaidie kwa sababu yeye hasa ndio mwenye mkoba wa fedha na uchumi wa nchi tumemkabidhi yeye.

Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa kwanza suala alilokurejeshea wewe Mwenyekiti, suala la kuunda hiyo Kamati Maalum ya kwenda kwenye Mkongo wa Taifa. Mhe. Mwenyekiti, bado una jukumu ambalo yeye kama Mhe. Waziri, ulijaribu kumshauri na nashukuru kwamba alikiri, lakini hakutoa maelezo ya kutosha. Suala la mkongo huu kwa kweli kama unapata ile *document*, au kama unapata taarifa zake, au ukipata zile nchi ambazo wanatumia huu mkongo kwa kweli faida yake ni kubwa sana.

Lakini bado Wajumbe wengi humu hawajui. Sasa hiyo Kamati Maalum itakwenda watakuwa bado watu wachache watapata hiyo taarifa. Na hata ripoti itakayotoka hapa, bado itakuwa haijaweza kuwasaidia sana Waheshimiwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana ile taaluma ya Waheshimiwa kwa ajili ya hii *E-Government* bado nafikiri ni kitu muhimu sana.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo ambalo katika uwekezaji wa Hoteli ya *Crystal*. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kusema kwamba hatuwaamini watendaji wetu katika taasisi zetu za serikali, tunawaamini sana, lakini bado hawawasaidii sana Mawaziri wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri, katika suala hili la mwekezaji huyu wa Hoteli ya *Crystal* tumeshalizungumza muda mrefu tokea kabla ya bajeti mpaka wakati wa bajeti na sasa hivi bado Mhe. Waziri, anasema tumpe muda. Mhe. Mwenyekiti, suala hili la mwekezaji huyu mpaka huyo Mkurugenzi wa Ardhi, sisi tulikwenda nae na amekiri kwamba yule mwekezaji amekalia eneo la mwekezaji mzalendo.

Na tukamuuliza mpaka *beckon* zake zile akakiri kwamba amejenga ndani ya eneo la huyo mwekezaji mzalendo. Sasa Mheshimiwa hapa tena kuna kitu gani. Au ndio yale aliyosema yule jamaa kwamba hii serikali ameiweka mkononi. Mhe. Mwenyekiti, kauli ya jamaa yule Mwalimu Nyerere katika *speech* yake moja aliwahi kusema.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe toa *concern* yako upate maelezo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: *Concern* yangu Mhe. Waziri, naomba hili mara tu tukimaliza kikao tukae mimi na yeye na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na wale Wakurugenzi wake wa Ardhi pamoja na watu wa *ZIPA* ambao tulikuwa nao katika *spot* warejee maneno waliyoyaeleza pale katika eneo, ili mwekezaji huyu mzalendo apate haki yake. Sisi hatuna tatizo na mwekezaji wa *Crystal*, tatizo letu kulikalia eneo la mzalendo anazalisha mali.

Na leo asubuhi kwenye Mawio eti anajidai anataka kuwasomesha watu wa Paje. Wewe unakalia eneo la mzalendo unamdhulumu halafu unasema unataka kuwasomesha watu wa Paje, miaka yote ulikuwepo wapi. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, hapa ilikuwa huu ubabaishaji wa hawa wawekezaji kwa kweli sasa tunataka tuondokane nao, tunataka Mawaziri wetu wawajibike moja kwa moja.

Sasa la mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuna hoja hii muhimu sana ya mwekezaji wa chelezo kule naona Mhe. Waziri, aliisahau hakuitolea maelezo na hii hoja muhimu sana tena ya msingi. Kwa sababu huu ni mradi mkubwa ambao utaweza kutoa ajira ya zaidi ya vijana 200 Wazanzibari na kuna meli nyingi za kigeni zitakuja kufanyiwa matengenezo hapa Zanzibar. Na hili pia Mhe. Waziri, naona alilisahau.

Lakini mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, sisi ndio tunaopitisha bajeti hapa, na asilimia tunapokwenda katika ziara watendaji wake ndio waliotwambia, sio watendaji wa Wizara yake, watendaji wa Wizara mbali mbali wao ndio waliotwambia tumepata asilimia 25 ya *OC*, wengine asilimia 30. Sasa hii *program* ya *PBB* Mhe. Mwenyekiti, hii ni *program* mpya.

Ndio yale tunayosema hawa Waheshimiwa tunapobadilisha *program* za kuendesha nchi lazima wapewe dozi ya kutosha. Leo wametwambia hata kama umeikuta shilingi moja tu imetiwa katika bajeti angalia *outcome.* Sasa kama tulikuwa tunategemea katika *OC* pale iingizwe tuseme asilimia 80 au asilimia 100, kama imeingizwa asilimia 25 kweli *outcome* itatoka itakuwa nzuri. Hii *PBB* mimi nafikiri tueleweshwe vizuri ili tuweze kujua. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, itakuwa wenzetu wataalamu wa uchumi wa Wizara ya Fedha wanatubadilishia *program* ili kutuchanganya kwa sababu sisi hatujui *program*.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, ili tusije tukafanya tatizo itakuwa kama sisi hatujafahamu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi na Makatibu Wakuu wa Mawizara na Wakurugenzi wao watakuwa hawajafahamu. Wao ndio wanaolalamika *OC* imetiwa asilimia ndogo. Sasa haya mengine ya maelezo ya hizo *program* za taaluma tutafanya baadae,

lakini haya mengine ambayo Mhe. Waziri, tumemwambia tunataka ayafanyie kazi, kwa kweli mimi naomba sana Mhe. Waziri. Na mimi namjua Mhe. Waziri, katika utendaji kwa kweli ni hodari sana, lakini tatizo lake ana shughuli nyingi. Kwa hiyo, apunguze shughuli tufanye kazi ya wananchi.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma, nimemfahamu vizuri sana. Na haya yote ambayo alikuwa anayazungumza ukiachilia mbali chelezo, yote aliyoyasema ndio lengo letu. Taaluma kwa Waheshimiwa kuhusu habari ya *E-Government* hiyo ni muhimu sana. Ni lazima tupate taaluma ya kutosha na tutaandaa na vijana wetu waje watoe taaluma ya kutosha kuhusu habari ya *E-Government* ili tuweze kuifahamu vizuri sana. Na hapo tutaandaa angalau kitu, basi kama hiki ili kila mmoja baadae aweze kusoma. Baada ya pale kwenye mkutano tu aweze kusoma akiwa *free* mwenyewe.

Lakini la pili, amezungumzia kuhusu habari ya mwekezaji. Nimesema pale mwanzo kwamba tatizo kubwa lililopo pale ni la ardhi. Tumekaa na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, tumemuandikia *ZIPA* atupe kwa maelezo. Hata Serikali inafanya kazi kwa maandiko, atupe kwa maandiko. Kutokana na maandiko atakayotupa yeye ndio yale sasa tutaanza kum-*question.* Tumeshakubaliana mambo mengi mimi na Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, lakini bado hayaja-*materialize.* Yeye mwenyewe Mhe. Hamza Hassan Juma, kasema kwamba hata Mkurugenzi wa Ardhi kakiri kwamba tatizo ni la ardhi. Sasa sisi tunataka kulipatia ufumbuzi ambao utakaoleta busara. Mimi namwambia atupe muda ili tulikamilishe hili suala.

Amezungumzia *program* ya *PBB.* Tumetoa semina nadhani hapa kwa Waheshimiwa Wawakilishi, lakini bado inaonekana ile semina haitoshi. *This time* kwenye bajeti ya mwaka huu tunakuja na kitabu ambacho mtaona tunapozungumzia *PBB,* ni nini hasa ile idara inatakiwa kufanya. Na hicho kitabu mkikisoma kitakusaidieni sana kuweza kufahamu hasa *PBB.*

Tutafanya semina nyengine kwa kutoa na mifano. Tutachukua *line item* moja halafu tutatoa na mifano ili kila mmoja aweze kufahamu. Mimi *last week* nilikuwa na watendaji wangu Kitengo cha Bajeti tumekaa tumelizungumzia sana hili na nimeona umuhimu wake. Kwa kweli hata *system* ndio hiyo aliyosema Mhe. Hamza Hassan Juma. Ni kweli lazima tubadilike. Hata *system* ya ku-*audit* tunataka tuibadilishe. *Auditors* nao kwenda tu wakatizama pesa zilizoingia na risiti tu haisaidii. Risiti zinapatikana bila ya matatizo yoyote kwenye maduka yetu.

Tunataka tutazame na *outcome* vile vile. Kwa hivyo, hata ile *audit* yenyewe *procedure* zao tunataka tuzibadilishe. Kwa hivyo, haya nadhani yanahitaji

muda ili baadae twende pamoja, ili tuweze kuyafahamu sote. Yatachukua muda kidogo, lakini naamini kwamba tutafika pahala tutayafahamu.

Mwekezaji wa chelezo. Mhe. Hamza Hassan Juma, hili suala tumeshaliongea kipindi kirefu sana na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Hapa tulipofika leo Mhe. Mshimba Mbarouk ni shahidi, tumefika hapa baada ya kufanya kazi mimi na yeye. Tatizo bado hawajapata *certificate.* Lazima tupate maelezo kwa nini. Maelezo tuliyopata hayajatutosheleza. Unajua Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya wakati huwa hatusemi, lakini tunabeba ndani ya matumbo, tunayajua mambo mengi hapa. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anasema nae ana yake huyo. Nakuomba sana Mheshimiwa ustahamili kidogo tupate sababu za msingi kwa nini hawajapewa *certificate* mpaka leo. Tutalifanyia kazi na tutampa taarifa.

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa kumsaidia Waziri wangu na ni kweli hili suala tumelifanyia kazi mpaka tukafikia pahala hapa lilipo. Lakini tuseme ukweli kuna barua ambayo imeonesha wazi na tumeambiwa barua hiyo na naomba iletwe hapa. Barua hiyo tumeambiwa kuwa limezuiliwa lile suala, haikutoka pale *ZIPA* imetoka kwengine, imeletwa pale barua. Kwa nini sasa kuna kitu hicho.

Tunaomba sana *ZIPA,* tayari wametoa barua ya kuukubali ule mradi, lakini kuna mabwana wakubwa wameenda kutoa barua kusema hii ni amri kutoka kwenye Baraza la Mapinduzi. Mimi mwekezaji mzalendo bwana tunaomba Mhe. Waziri, kalifikisha pahala pazuri na kwenye bajeti mara ile alisema alitaja katika miradi ambayo imeshatokea ya wazalendo akautaja na huo. *ZIPA* kafanya kazi katoa barua, lakini kapigwa *stop.* Kwa sababu gani, yule mtu anatakiwa apeleke mradi Bara Bagamoyo kakataa kasema hapana hapa hapa Zanzibar nitanufaisha. Tutafute kuambizana ukweli jamani tusifichane. Kuna mtu anataka pale apewe kwa mradi aina hiyo. Kama nilivyokwambieni msinichokoz, lakini nitasema ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana namshukuru sana Mhe. Waziri, amekubali amekiri *inshaallah* Mungu amjaalie tuendelee na utaratibu ule, barua ile itafutwe iweze kuletwa hapa tuone ule ukweli tutacheka sisi wenyewe Wajumbe. Mimi siku zote nasema nitakuwa mkweli.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, amesikia na atalichukua hilo kwa ajili ya utekelezaji zaidi.

MUONGOZO

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka muongozo kwenye ile kauli ambayo ameitoa Mhe. Waziri wa Fedha, pale juu ya kuundwa kwa Kamati Maalum. Nilikuwa nataka kujua ule utaratibu. Maana yake ninachokumbuka mimi kwenye kanuni zetu tuna Kamati Teule pale kwenye kifungu cha 120. Sasa sijui Kamati Maalum itapitia katika upande upi. Nilikuwa naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nimekufahamu Mhe. Mjumbe, muongozo wangu nitatoa, wacha tuendelee na Wizara nyengine, halafu kabla hatujamaliza suala hili nitalitolea muongozo. Ahsante.

Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii tena kuchangia na kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuhusu maagizo na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe kwa kuichangia vizuri. Nataka niwahakikishie kuwa michango yao, maelekezo na ushauri wao waliotupa tumeupokea na tutayafanyia kazi kadri ya uwezo utakavyoturuhusu kwa lengo la kuleta mafanikio ya Wizara na wananchi wote kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa michango na maelekezo. Tunaahidi kwamba Wizara itayafanyia kazi maelekezo na ushauri walioutoa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwataje kwa majina wachangiaji waliogusa Wizara hii. Nao ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mbwana Mohammed Hamad, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Mwenyekiti, na wengine wawili walichangia kwa maandishi. Nao ni Mhe. Fatma Mbarouk Said na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa majadiliano Wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu michango yao ililenga zaidi katika mambo matatu. Moja, upatikanaji wa pembejeo na uimarishaji wa kilimo cha mpunga. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nikitoa hoja za awali kuhusu upatikanaji wa pembejeo na

matrekta ni kwamba kuanzia msimu wa mwaka 2012, tatizo hilo limetatuliwa na kwa pembejeo zote zimesambazwa kwa wakati, kabla ya kuanza kutumika, tayari zilikuwa ghalani na zinasubiri wakulima. Utaratibu huu unatarajiwa kuwa endelevu kwa kila msimu ili kufanikisha kilimo cha mpunga.

Kwa upande wa matrekta kwa msimu huu wa kilimo yalianza kuingia mabondeni tarehe 22/07/2013. Hata hivyo, wakulima walianza kujitokeza tarehe 08/08/2013, lakini wakulima wengine walilalamika kuwa matrekta yamepelekwa mapema.

Deni la wakulima wanaoidai serikali malipo ya uuzaji wa ndege. Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru Wajumbe wote walioliona suala hili na hasa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Wizara ya Kilimo na Maliasili imeanza kuchukua hatua za ukamilishaji wa malipo ya fedha hizo za wakulima ambapo kwa kuanzia wiki ijayo wakulima wa bonde la Mtwango watalipwa shilingi milioni 55.

Aidha, juhudi hizi za kuwalipa wakulima wengine waliobakia watalipwa kadri ya fedha zitakapopatikana kutoka serikalini.

Kuhusu kukamilika miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji Makombeni. Mhe. Mwenyekiti, kazi nyengine iliyobakia ni uwekaji sawa wa bonde la Makombeni kwa mujibu wa mkataba wa mradi huu. Kazi hiyo inafanywa na wanajamii. Aidha, Wizara itaendelea kuwashajiisha wananchi na kutoa elimu ili kazi hiyo ikamilike.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na maoni hayo, pia yamejitokeza mengine kama yafuatayo:

Hoja ya Mhe. Bikame Yussuf Hamad na Mhe. Panya Ali Abdall, ambayo ni hoja ya uwezeshaji wa hifadhi ya chakula. Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na hoja ya kwamba suala la uanzishwaji wa hifadhi wa chakula nchini umechukua muda mrefu sana na halijakidhi matarajio ya wananchi. Changamoto kubwa inayokabili Wizara ya Kilimo na Maliasili katika utekelezaji wa suala hili ni upatikanaji mdogo wa fedha za utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, uanzishwaji wa hifadhi ya chakula unahitaji fedha nyingi. Jumla ya dola za Kimarekani milioni ishirini zinahitajika kwa ajili ya ukarabati wa maghala, ununuzi wa vifaa vya muhimu, mafunzo kwa watendaji na ununuzi kwa hizo bidhaa zenyewe; yaani mchele na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na gharama hizi kubwa na uingizwaji mdogo wa fedha ni dhahiri kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili itashindwa

kulitekeleza suala hili kwa kutegemea bajeti ya kawaida. Hivyo, Wizara ya Kilimo na Maliasili hivi sasa inakamilisha waraka wa kuupeleka serikali ili kuishauri iombe mkopo au uandaliwe utaratibu maalumu wa kupatikana fedha ili tuweze kutekeleza suala hili kwa ufanisi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ameulizia dawa ya magugu kwamba haitoshelezi. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli dawa ya magugu haitoshelezi kwa wakulima wote wa mpunga. Hii imetokana na kiwango kinachoagizwa kuwa ni kidogo na hakiwezi kuongezwa, kwa sababu dawa hizi ni sumu na endapo zitatumika wingi zitaleta athari.

Mhe. Mwenyekiti, tusisahau kwamba dawa hizi tunazitumia kwenye ardhi, na kwenye ardhi ndiko tunakopata maji yetu ya kunywa. Sasa tukizitia kwa wingi kama wanavyotaka wakulima, kila mtu aboboshe ardhi, dawa itakwenda kwenye maji na ni athari kwa afya zetu.

Wizara ya Kilimo na Maliasili inawaomba wakulima wote watumie kiwango hicho wanachopata na sehemu inayobakia wapalilie kwa kutumia njia mbadala.

Mhe. Mohamed Ali ukataji wa miti ovyo. Mhe. Mwenyekiti, suala la ukataji wa miti bado unaendelea ili wananchi wajipatia nishati ya kuni, gesi na umeme na
nishati nyengine mbadala zina gharama kubwa na wananchi hawazimudu. Aidha, ukataji wa miti ni kosa, tuelimishe maana bora ya kukata miti bila ya kuathiri mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli zaidi ya asilimia 95 ya wananchi wa Zanzibar wanatumia kuni kama ni chanzo cha nishati ya kupikia, yaani kuni au makaa. Matumizi ya gesi na umeme ni kwa asilimia ndogo sana kutokana na gharama kubwa. Hivyo ni dhahiri kwamba kwa muda mrefu bado wananchi wataendelea kutumia kuni kuliko nishati nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea kutekeleza na kutoa miongozo ifuatayo ili kuwa na matumizi endelevu ya maliasili hizo:-

a) Kwa Shehia zenye misitu mikubwa tumetenga maeneo ya matumizi kwa ajili ya kuni na maeneo ya uhifadhi.

b) Tumeanzisha matumizi ya majiko sanifu yenye kutumia nishati ndogo.

c) Kuendelea na utaratibu wa upandaji wa miti kwa vikundi na watu binafsi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya kuni.

d) Ukataji wa miti wowote ni lazima upate kibali maalumu ambacho idhini yake imeanza na ruhusa itoke kwa Sheha wa Shehia husika kabla ya ruhusa kutolewa na maafisa wa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

e) Tunawanasihi na kuwaomba wananchi wote wafuate utaratibu wa sheria ya misitu katika uvunaji wa maliasili.

Mhe. Panya Ali Abdalla, anasema kwamba serikali isiwakope wakulima na iwapatie mahitaji yao. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili imejipanga kuwapatia wakulima mahitaji yao ya pembejeo na huduma za matrekta. Hata hivyo, uchelewaji wa huduma kutolewa kwa wakulima unatokana na hali ya hewa hasa kwa hivi sasa mabonde mengi makavu, na matrekta hayawezi kulima, wakulima wanatakiwa wawe wastahamilivu.

Maana hata ukilazimisha kupeleka trekta katika bonde ambalo ni kavu sana, kitakachotokea ni majembe kukatika na itakuwa ni hasara zaidi. Mabadiliko ya hali ya hewa ndio yanayoathiri sana kilimo hasa cha mpunga. Mvua zikiwa nyingi matatizo, jua likiwa kali ni matatizo.

Mhe. Asha Haji na Mhe. Hamza Hassan Juma, wakulima na mkataba walipwe fedha za kuuza mbegu. Nilizungumza mwanzo. Kuhusiana na suala hili Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na utayarishaji wa malipo kwa wakulima ambao wamezalisha mpunga wa mbegu na mara tutakapokuwa tayari wakulima hao watapatiwa malipo yao. Tumesema kwamba mwezi huu tunaanza na Mtwango.

Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha fedha hizo zinapatikana. Aidha, Wizara inawaomba wakulima kuwa wavumilivu katika kipindi hiki kigumu.

Mhe. Asha Bakari Makame, anazungumzia juu ya mapinduzi ya kilimo. Mhe. Mwenyekiti, mapinduzi ya kilimo hayakuvia na wizara inahakikisha kwamba yanakuwa endelevu na ndio maana imeandaa mkakati maalumu unaoitwa mageuzi ya kilimo.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad anazungumzia uchache wa mafundi wa matrekta na zana chakavu. Mhe. Mwenyekiti, wizara imechukua hatua za kupeleka vijana masomoni, na tunatarajia nafasi za wastaafu zitajazwa.

Mhe. Mohamed Ali na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwamba idara iwapatie wakulima pembejeo na matrekta kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, wizara inakubaliana na ushauri huo wa kuwapatia kwa wakati wakulima pembejeo na zana nyengine za kilimo. Wizara inauchukua ushauri huo na itaufanyia kazi.

Aidha kuhusiana na suala la ukamilishaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji, wizara kupitia Idara ya Umwagiliaji Maji inaendelea na utekelezaji wa mpango mkuu wa kilimo cha umwagiliaji maji ambapo kati ya hekta elfu nane mia tano na ishirini na moja, hivi karibuni kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo wa Korea itajengwa miundombinu ya umwagiliaji maji jumla ya hekta 2105 katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba.

Mhe. Mlinde Mbarouk, anaulizia juu ya ufanisi wa mbegu ya *NERICA*. Mhe. Mwenyekiti, mbegu ya Nerica ipo na inaendelea kuzalishwa kwa ajili ya mbegu isipokuwa baadhi ya wakulima hawazipendi kwa sababu zao hasa kwa ladha yake.

Hivyo, Wizara ya Kilimo na Maliasili ipo tayari kumpatia Mhe. Mwakilishi pamoja na watu wengine ambao watataka kuipanda mbegu hiyo. Wizara itawaagiza wataalamu wake kufanya matayarisho ili mbegu hiyo ipatikane kwa wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, watu wetu wamezoea mbegu zao za asili zenye kunukia ambazo wanazipenda sana hata kuliko mbegu za sasa hivi. Mhe. Mwanajuma Mdachi alisema kuongeza kasi ya upandaji wa mikarafuu. Kwa kuelewa kwamba karafuu ni uti wa mgongo wa Zanzibar, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeweka mikakati ya hali ya juu kuhakikisha kwamba Zanzibar inaendelea kung'ara katika kuongeza uzalishaji wa karafuu.

Katika kipindi cha miaka mitatu mfufulizo Wizara ya Kilimo na Maliasili imeweza kuvuka malengo ya uoteshaji wa miche ya karafuu. Aidha, miche hiyo inafuatiliwa, na kwa hivi sasa tumeweza kuotesha miche milioni moja kila mwaka. Vile vile, elimu inaendelea kutolea kuhusu uoteshwaji wa mikarafuu na mchango wa watu binafsi ni mkubwa sana, lakini tuelewe kwamba mkarafuu ni mti harara unahitaji utaalamu maalumu katika kuupanda mpaka uote, vyenginevyo jua kali hili linaloendelea matatizo yanaendelea miche inaweza ikapotea.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kutia moyo kwamba wananchi tayari wamehamasika katika kuotesha mikarafuu. Miche hiyo ya serikali na watu binafsi inatolewa bila ya malipo kwa wakulima.

Mhe. Makame Mshimba amezungumzia sheria ya msitu ifanyiwe marekebisho ili iweze kukidhi hoja ya matumizi endelevu ya maliasili. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba sheria ya misitu ya hivi sasa haikidhi haja ya kuleta matumizi endelevu ya misitu.

Sheria hiyo tayari imeshapatiwa mapitio na kuainishwa mapungufu yaliopo. Aidha Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na mshauri elekezi wameanza kazi ya matayarisho ya sheria hiyo. Kazi hiyo ilisitishwa kwa lengo la kusubiri matokeo ya utafiti wa sensa ya miti. Kazi ya sensa ya miti imekamilika na matokeo ya sensa hiyo itatoa mchango mkubwa katika kukamilisha sheria ya misitu kwa uhakika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid ameulizia upelekaji wa umeme katika bonde la Machigini kwenye Shehia ya Mtambile. Mhe. Mwenyekiti, upelekaji wa umeme katika bonde la Machigini linahitaji shilingi milioni sitini ambapo Shirika la Umeme wanahitaji wapatiwe nusu ya gharama hizo na Wizara ya Kilimo na Maliasili iweze kutoa shilingi milioni kumi. Wizara ya Kilimo na Maliasili imeweza kutoa shilingi milioni kumi, fedha zilizobakia bado hazijapatikana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amezungumzia hatua zilizofikiwa katika mradi wa umwagiliaji katika bonde la Kilombero hekta mia mbili na thalathini. Mhe. Mwenyekiti, bonde la Kilombero ni moja kati ya mabonde yanayotegemewa kutayarishwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji kupitia mradi wa *Exim Bank* ya Korea. Kinachosubiriwa hivi sasa ni ruhusa ya matumizi yaani *no objection* kutoka *Exim Bank* Korea ili kuendelea na hatua nyengine ya kuanza kwa mradi.

Mhe. Asha Abdu Haji, amezungumzia uanzishwaji wa kilimo cha umwagiliaji maji Wami Gomba. Mhe.Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili tayari imeshaanza juhudi za makusudi kushajihisha wakulima kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maji kwa mazao mengine ikiwemo migomba. Katika kufanikisha suala hili mradi wa ASSP tayari umetayarisha andiko la mradi wa kilimo cha matunda na mboga mboga ikiwemo na migomba.

Mhe. Mwenyekiti, tayari baadhi ya wakulima wameshaanza kilimo cha migomba kwa njia ya umwagiliaji maji kwa matone.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma juu ya uchimbaji wa kisima cha pili katika bonde la Koani. Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana na hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba uchimbaji wa kisima cha pili ni muhimu ili kuweza kulihudumia eneo lote la hekta ishirini kwa umwagiliaji. Wizara ya Kilimo na Maliasili

tayari imeliingiza suala hili kwa washirika wa maendeleo kupitia mradi wa *GAFSIP*.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kurejea tena kuwashukuru Waheshimiwa wote waliochangia katika wizara hii na maelezo yao pamoja na kuwa nimeyajibu, lakini kinachotakiwa sio kujibu ni kwenda kuyafanyia kazi na kuona kwamba yanatekelezeka kwa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya (Kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, naomba kutoa majumuisho ya taarifa ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii tena ya kufanya majumuisho ya michango ya Wajumbe kuhusu taarifa ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, pia namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Thuwayba Edington Kissasi kwa mashirikiano yake makubwa hasa kwa kunisaidia kunieleza mambo mengi yanayohusu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kufanya kazi hii ionekane rahisi kwangu mimi.

Tunamshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mhe.Salmin Awadh Salmin pamoja na Wajumbe wa kamati yake kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuisimamia shughuli za wizara yangu na hatimaye kutoa taarifa ambayo imekuwa nzuri na iliyokuwa na matatizo machache. Hata michango ya Wajumbe inaonekana kwa wizara yetu si mingi kiasi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niwatambue Wajumbe wote waliochangia ambao ni wachache pia, kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Panya Ali Abdalla
4. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid
6. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati wote hawa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu na hasa Wajumbe wote waliochangia taarifa ya wizara ambao pia wamechangia kwa wazi, ufasaha na umahiri kweli.

Napenda kuwahakikishia kwamba michango na maelezo na ushauri wao tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya wizara na kuendelea kufanya vizuri kama vile munavyotuelewa wizara yetu inavyojitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya maelezo yanahitajika hasa yaliyoelezwa na Mwenyekiti wa kamati yakiwemo suala la wajasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa yake Mhe. Mwenyekiti amezungumzia umuhimu wa kuendelea kuwasaidia wajasiriamali kwa karibu zaidi huku akitilia mkazo suala la mitaji na kuweka mkakati maalumu juu ya kutafuta soko kwa bidhaa za wajasiriamali wetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala kweli ni muhimu na tunahakikishia kuwa pamoja na kwamba wajasiriamali wetu tunakwenda nao vizuri sana katika masuala yote hayo, lakini tutazidisha nguvu zetu katika kuwasaidia zaidi ili kuwaongezea ufanisi.

La pili ilikuwa ni suala la viwanda. Mhe, Mwenyekiti, hapa Mwenyekiti wa kamati amesisitiza juu ya umuhimu wa kuikamilisha mapema sera ya viwanda na akaitaka serikali kuipa msukumo maalumu sekta ya viwanda, kwani ni kweli sekta hii itachangia sana katika kunyanyua uchumi wa nchi yetu na kupunguza suala la matatizo ya ajira kwa vijana wetu na kupunguza umaskini.

Aidha ni kweli kwa sasa wizara ina upungufu wa wataalamu lakini tayari tumekwishawasiliana mahitaji yetu ya wataalamu katika Ofisi ya Tume ya Utumishi Serikalini na tunaamini yamo katika kufanyiwa kazi.

Kuhusu majengo yaliopo Saateni. Mhe. Mwenyekiti, wizara bado hatujarudishiwa majengo hayo na JKU ambao ndio tuliokuwa tumewaazima wakati wizara ilipokuwa hayatumii, lakini tunaendelea kuwasiliana nao na mara tu tukikabidhiwa, basi ukarabati utaanza mara moja ili azma yetu ya kuyafanya majengo hayo kuwa ni *incubator*, yaani kama kiotea mayai cha wajasiriamali na wafanyakazi wa viwanda vidogo vidogo iweze kuanza kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Kiwanda cha Sukari. Ni kweli ipo haja ya kiwanda hicho kupewa ulinzi kutokana na hujuma zinazofanywa na baadhi ya wananchi katika mashamba na kurejeshewa nyumba zao. Wizara imesikia

hoja hiyo na itashirikiana na Wizara ya Fedha kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha katika maelezo yake hapo mapema.

Suala la *ZBS*, yaani *Zanzibar Bureau of Standard.* Kwa kweli imepiga hatua kubwa shughuli zake na mengi yameshafanyika ikiwa ni pamoja na matengenezo ya ofisi hapo Saateni, na kwa kweli wanaendelea vizuri ingawa kama pesa zipo wakiongezewa basi mambo yatakuwa mazuri zaidi. Hivyo tunashukuru sana kwa Mwenyekiti kutusaidia katika kulisemea suala hili la kuingiziwa fedha.

Aidha suala la uhaba wa wataalamu, tayari nalo tumeshalifikisha katika Tume ya Utumishi Serikalini.

Kuhusu *ZSTC*. Mhe. Mwenyekiti, Shirika la *ZSTC* ameshauri mambo yafuatayo:-

1. Katika vituo vinavyonunuliwa karafuu, wakulima wasidhulumiwe walipwe kwa karafuu zao zote kama hazipimiki ni kidogo sana basi warejeshewe wenyewe. Mhe.Mwenyekiti, hili tunakubaliana nalo na tutalishughulikia ipasavyo.

2. Wizara kushirikiana na vikosi katika uzuiaji wa magendo; ni suala jema na ndio tunavyofanya.

3. Duka la *ZSTC* lisiuzwe ila liboreshwe na kwa kushirikiana na Ofisi ya SMZ iliopo Dar es Salaam basi *ZSTC* walinunue jengo hili. Suala hili tumekuwa tukilifanyia kazi kwa muda mrefu sasa na ndio lengo la wizara kubaki na jengo hilo kwani ni raslimali nzuri kwa siku zijazo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya Mwenyekiti, kulikuwa na maelezo vile vile kutoka kwa Wajumbe ambayo ni moja kuuzwa kwa eka.

Mhe. Mwenyekiti, imependekezwa kwamba baadhi ya wananchi wanauza eka walizopatiwa na serikali, hivyo kuna haja ya kulifuatilia suala hili.

Wizara imelipokea pendekezo hilo na itashirikiana na Wizara husika hasa ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Utekelezaji wa sheria ya viwango.

Mhe. Mwenyekiti, imependekezwa kwamba kuna bidhaa nyingi chakavu na mbovu zinazoingia nchini. Hivyo, kuna haja ya kuharakisha utekelezaji wa

sheria ya viwango Zanzibar. Wizara inaendelea na utayarishaji wa Kanuni na viwango mbali mbali vya bidhaa zikiwemo bidhaa chakavu na mbovu. Utekelezaji wa kanuni hizo utaweza kudhibiti ipasavyo matumizi ya bidhaa mbovu na chakavu.

Kuhusu utekelezaji wa eneo tengefu la kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe walipendekeza kuna haja ya kuharakisha utekelezaji wa eneo tengefu la kiuchumi kwa vile baadhi ya miundombinu muhimu kama umeme yameshapatikana. Utekelezaji wa mkakati huu unahitaji umakini mkubwa hasa baada ya kuwakaribisha wawekezaji wakubwa. Hivyo, wizara inaendelea na taratibu za kuandaa sera, sheria na mpango wa utekelezaji wa mkakati huo ili kuhakikisha suala hilo linatekelezwa kwa ufanisi na tusije tukakwama kati kati ya njia baada ya mambo kufanyiwa haraka.

Ukosefu wa soko kwa wajasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba suala hili tayari limeshatolewa ufafanuzi wakati mwengine, lakini nisisitize tu kwamba wizara inaendelea kutafuta masoko kwa bidhaa za wajasiriamali na kwa sasa wizara huwa inawapeleka kila inapokuwa na fedha katika maonesho na matamasha ya kibiashara.
Aidha, wizara itaendelea kuwafuatilia wajasiriamali na kuorodhesha bidhaa zao kwa ajili ya kuwatafutia masoko. Kwa taarifa ya Wajumbe wajasiriamali wameshawahi kupelekwa mpaka Korea ya Kusini, Rwanda, Nairobi na kila zinapopatikana fedha huwa wanasaidiwa kwenda katika maeneo ya maonesho.

Kilichogundulikana tu kwamba taarifa za wajasiriamali hawa na wanapopata *orders* zinazotoka huko walikokwenda, mara chache huwa wanaweza kuzitimiza. Na mimi nina mfano mzuri, kuna wakati fulani ulikuja mkutano mkubwa hapa wa mambo ya utawala na wakaambiwa watengeneze mikoba ya ukili ile. Ile mikoba ya ukili mahitaji yalikuwa makubwa kuliko uwezo wa wale wajasiriamali. Ikawa wale Wajumbe wa mkutano wanaitaka mikoba, mikoba haipo. Kwa hivyo, vitu vyengine wala si tatizo soko, tatizo ni uwezo wa wale wajasiriamali kutimiza mahitaji.

Uchakavu wa mezani na kupima karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wamependekeza kuwa kuna haja ya kununua mezani mpya kwa ajili ya kupimia karafuu. Wizara imeanza kulifanyia kazi pendekezo hilo na tayari imeshanunua mezani mpya za kisasa ambazo zina

uwezo wa kupima ujazo mdogo kama robo kilo. Wizara itaendelea kununua kwa ajili ya kuziweka katika vituo vyote ili kuondosha malalamiko ya wakulima wa karafuu katika ujazo mdogo.

Bei ya makonyo ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa kwamba kuna haja ya kupandisha bei ya makonyo kwani iliopo sasa ni ndogo. Hili si wazo baya, bei ya makonyo iliopo sasa ni shilingi 700 kwa kilo ndio inayoendea na soko la dunia. Wizara itaweza kuongeza bei hiyo ikiwa bei ya mafuta itapanda katika soko la dunia, yaani mafuta ya karafuu, sio mafuta ya petroli.

Magendo ya Karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wameeleza kuwa kuna haja ya kuongeza ulinzi katika kuzuia magendo ya karafuu hasa katika bandari ndogo ndogo. Wizara imepokea mapendekezo hayo na itaimarisha ulinzi kupitia kikosi kazi. Juzi Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alichukua muda mkubwa hapa kueleza jinsi ya mafanikio ya kikosi kile kilivyoweza kuzuia magendo. Lakini kwa kupitia njia hii wananchi wanahitaji kushirikiana na wizara kwani tutakuwa hatulindi tu karafuu kupelekwa Mombasa lakini vile vile tunalinda raslimali zetu ambazo ndio msingi wa fedha za kigeni.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Wajumbe wake wote wa kamati pamoja na Waheshimiwa wote wa Baraza lako hili tukufu kwa michango yao na usikivu wao wakati wote nilipokuwa ninawasilisha ufafanuzi wa masuala mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niwashukuru wataalamu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambao wamekuwa pamoja na mimi na kuonekana vile vile kama ninaweza kuwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko hata kama sipo huko. Ninashukuru sana. Ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa kabla sijamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuna maombi ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi na niwapongeze

Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wajumbe kwa maelezo mazuri waliyotoa, ninaamini tutafikia maamuzi mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nimeomba hivi kutoa ufafanuzi kabla ya Mwenyekiti kuja ili maelezo yetu Mwenyekiti naye aweze kuyapokea.

Kubwa ilikuwa ni suala la Kamati Maalum. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mtando alitaka ajue hii kamati maalum hii ikoje au iko vipi.

Tunachoshauri kama serikali Kamati Maalumu hii iwe ni kamati ile ile ya kisekta iweze kufanya kazi maalumu kwa muda maalumu, kwa sababu tatizo kubwa lilijitokeza wakati ikifanya kazi zake haikuwa na muda wa kutosha kutokana na kazi nyengine nyingi. Ili kuepusha na shughuli nyengine za Kibaraza, basi serikali inapendekeza kamati hii ipewe muda maalumu, wakati maalumu ikafanye shughuli hii maalumu ili ilimalize tatizo hili ambalo limekuwa likizungumzwa na Wajumbe.

Na kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha kwamba yeye yupo kupokea kamati hiyo, kufanya nayo kazi na kwa sababu ni sehemu ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliopo.

Tunafanya hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kamati hiyo imeshaanza kazi, imeshapata uelewa kidogo wa jambo hili na kama unavyojua, tuna Bunge la Katiba lipo mbele yetu, kwa hivyo muda wenyewe ni mdogo sana ulio mbele yetu. Kwa hivyo tunapendekeza suala hili liende kwa utaratibu huu kwa nia njema kabisa ya kulipatia ufumbuzi. Hiyo hasa ndio ilikuwa lengo kubwa la kuomba kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba nitoe ufafanuzi mwengine kwa sababu wakati Mhe. Hamza Hassan Juma hapa alielezea kwamba kuna mwekezaji wa *Cristal* anayesema kwamba serikali ameiweka mkononi.

Sijui ana mkono mkubwa kiasi gani wa kutuweka mkononi serikali hii. Serikali hii haiwezi kuwekwa mkononi na mtu yeyote, na tukipata ushahidi wa maneno yake haya, sisi tunaweza tukamchukulia hatua za kisheria, hayana msingi kwa msingi hii na hana uwezo wa kuweka mkononi serikali hii, na tukipata ushahidi tutachukua hatua kali dhidi yake. Kwa hivyo, haya maneno maneno ya kuidhalilisha serikali tusingependa kuyasikia. (*Makofi*).

Vile vile, ningependa nitoe ufafanuzi kuhusu maelezo aliyotoa Mhe. Ismail Jussa Ladhu juzi hapa aliposema kwamba serikali hii ni *acting government*. Hii si *acting government*. Hii ni serikali, ni halali iliyochaguliwa na wananchi

na ipo hapa kwa mujibu wa Katiba za nchi na inakwenda kihalali kabisa. Si *acting* kabisa.

Kwa hivyo, ningependa nieleweke kwamba inafanya kazi kwa mujibu wa Katiba na Sheria na Mawaziri kukaimu ni utaratibu wa kawaida wa kiserikali. Kwa hivyo, anapokaimu waziri anafanya kazi za waziri muhusika.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufanya majumuisho juu ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe.

Lakini pili niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri; Mhe. Waziri wa Fedha Mhe.Omar Yussuf Mzee, Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe.Ramadhan Abdalla Shaaban, Kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Juma Duni Haji, kwa kutoa maelezo na majumuisho mbali mbali kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati na ahadi katika mwaka 2012/2013 kwa wizara zao pamoja na hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wajumbe wameweza kuzitoa.

Pia, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi kwa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, naamini Waheshimiwa Wajumbe mtakuwa mmeridhika na ufafanuzi ambao umetolewa na Waheshimiwa Mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuweza kutoa michango yao mbali mbali, inayohusiana na ripoti ya Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, ripoti ya mwaka 2013/2014 nawashukuru na ninawapongeza Wajumbe wote.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri ripoti yetu imepata kuchangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 14. Wajumbe 12 wamechangia kwa kusema na Wajumbe wawili wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kama muda zaidi ungeweza kupatikana basi Wajumbe wengi zaidi wangeweza kuchangia ripoti yetu hii, kwani wizara zetu hizi tatu ni wizara zinazogusa moyo wa nchi, ni wizara za uchumi ambapo uchumi ndio kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe waliochangia ripoti yetu hii kama hivi ifuatavyo;

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Asha Bakari Makame
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Asha Abdu Haji
7. Mhe. Panya Ali Abdalla
8. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
9. Mhe. Mohammed Haji Khalid
10. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
12. Mhe. Abdalla Moh'd Ali

Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa; na
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said

Mhe. Mwenyekiti, karibu Wajumbe wote waliochangia ripoti yetu wameanza kwa kuipongeza kamati kwa kazi nzuri tuliyoifanya. Mimi Mwenyekiti wa kamati hii kwa niaba ya Wajumbe wote wa kamati nazipokea pongezi hizo, na tunawashukuru sana kwa kutupongeza na kwa kweli wametupa moyo sana.

Mhe. Mwenyekiti, michango ya Waheshimiwa Wajumbe ilikuwa ni mingi sana na mingi tayari imeshapatiwa ufafanuzi kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri husika, lakini pamoja na ufafanuzi uliotolewa Mhe. Mwenyekiti, lakini ningependa kuizungumzia baadhi ya michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe walio wengi.

Mhe. Mwenyekiti, mchango mmoja ulihusu kuingiziwa fedha za kufanyia kazi katika wizara mbali mbali na shughuli za maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii tayari Mhe. Waziri wa Fedha ameshaitolea maelezo mengi sana na ni maelezo ya kitaalamu na ya takwimu. Sasa sijui kama takwimu zile zimefahamika, kwa sababu kama unavyojua ni takwimu za kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, kinachoonekana alizungumzia mambo mawili makubwa, kwamba katika hali hii matumizi haya ambayo Waheshimiwa Wajumbe walipopita katika wizara mbali mbali, walikuta kwamba fedha zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo na fedha zile za kawaida haziridhishi kiasilimia. Lakini Mhe. Waziri hapa anasema hatuko vibaya, na kwa sababu asilimia 46

ya fedha za *recurrent* ndio zilizotolewa, isipokuwa kwenye fedha za maendeleo ni asilimia 19 hapa ndipo penye tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe sio wataalamu sana wa mambo ya mahesabu, lakini tunachofahamu ni moja kwa moja na uhalisia wa mambo yenyewe. Tunafahamu kwamba bajeti ya serikali tunayopitisha hapa inakuwa na maeneo mawili makubwa. Eneo la kwanza ni eneo la matumizi ya kawaida ambalo nalo huwa linagawika katika maeneo mawili; mishahara na fedha za kufanyia kazi. Sasa kwa upande wa fedha za mishahara hapa hatuna matatizo, fedha zote zinapatikana kwa asilimia 100, lakini tatizo liko katika fedha za kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mawizara mengi tunakuta kwamba zile fedha za kufanyia kazi ambazo zimepangwa, hizo hizo chache zilizokuwa zimepangwa katika bajeti, basi haziendani na ule muda ambao upo.

Kwa mfano utakuta utekelezaji wa bajeti upo karibu miezi sita, kuanzia Julai hadi Disemba, lakini fedha zilizotolewa katika kipindi hicho cha miezi sita kwa ajili ya fedha za kufanyia kazi basi utakuta iko kwenye asilimia 20, 21 au 26. Sasa ni dhahiri fedha zile za kufanyia kazi hazijapatikana ipasavyo, na jambo hili kwa kweli huwa linadhorotesha shughuli za utendaji wa kazi.

Mhe. Waziri, hapa alitoa mbinu za Waheshimiwa Wajumbe wanapokwenda kwenye mawizara basi waangalie ule mtiririko mzima. Mimi kwenye kamati yangu ndivyo ninavyofanya na wale watendaji huwa ninawalazimisha watoe ule mchanganuo maalumu juu ya zile fedha jinsi zilivyoingizwa na katika kasma mbali mbali. Lakini utakuta kasma nyingi zinakuwa hazina kitu, ni zile kasma ambazo ni muhimu ndio utazikuta zimeingiziwa asilimia, kama kasma zile za safari hivi na mambo mengine. Lakini katika maeneo makubwa yanakuwa fedha zile hazipo. Hiki ndicho kilio cha Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, unapozungumzia asilimia 46 *recurrent*, utakuta fedha nyingi zimekwenda kwenye mishahara, lakini zile za kufanyia kazi hazipo na hata jana Mhe. Ismail Jussa alisema kwamba inaonekana sehemu kubwa ya fedha zinatumika kwa mishahara, lakini hao wenyewe wanaolipwa hiyo mishahara fedha zile za kufanyia kazi wanakuwa hawana.

Kwa hivyo, utakuta shughuli nyingi za mawizara na taasisi zinakuwa haziendi kama vile zilivyopangwa. Kwa hivyo, hicho ndio kilio kikubwa cha Waheshimiwa Wajumbe katika mawizara.

Vile vile, fedha za maendeleo katika sehemu ya pili. Utakuta fedha za maendeleo nazo ziko katika maeneo mawili. Kuna fedha zinazoahidiwa na

wahisani na fedha zinazotolewa na serikali. Fedha hizi zinazoahidiwa na wahisani hatusemi kwa sababu ni kitu cha kugaiwa, huwezi ukakilazimisha, utakachopewa ndicho utakachopokea. Lakini fedha za miradi ya maendeleo zinazotolewa na serikali hapa ndio tatizo, ambapo ni fedha chache sana zinazotolewa katika miradi yetu sisi wenyewe ya maendeleo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hili ndio tatizo letu, na kwa sababu sisi tunataka tuone moja kwa moja, lakini ukitupa asilimia tutakuwa hatukuelewi, isipokuwa tunataka tuone kile kinachotolewa moja kwa moja. Kwa hivyo, hili ndio suala la juu ya uingizwaji wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ni kuhusu suala la mradi huu wa *E-Government* na ile miradi mipya ambayo inaanzishwa na serikali. Hoja hii ilijadiliwa sana na kubwa wasi wasi wa Waheshimiwa Wajumbe ni juu ya gharama za huu mradi. Inaonekana gharama za huu mradi ni kubwa kulingana na mradi wenyewe na namna ya utekelezwaji wenyewe wa huu mradi. Hapa ndio kidogo pamekuwa na mashaka. Sasa ufafanuzi umetolewa, naamini Waheshimiwa Wajumbe wameridhika na kama hiyo kamati maalum itakuwepo kama ilivyopangwa basi itapata nafasi sasa ya kuingia zaidi kuona na hizo gharama nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi wakati fulani niliwahi kuuliza juu ya thamani ya huu mradi nilipokuwa kwenye Wizara ya Fedha, niliwahi kumuuliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Hivi unahisi fedha hizi zilizotolewa zinalingana na gharama za mradi wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, Katibu Mkuu yule aliniambia kwamba sisi sote hatuelewi kwa sababu mradi huu ni mpya haujawahi kufanyika. Kwa hivyo, hatuwezi kuoanisha kati ya gharama zilizotolewa na thamani ya mradi wenyewe. Sasa kwa kweli hilo ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa kubwa zaidi ni juu ya miradi inayoanzishwa hii mipya. Kumekuwa na matatizo mengi juu ya miradi hii tunayoanzisha, inaanzishwa lakini hatimaye inafika pahala inakwama na inakuwa na matatizo. Kwa hivyo, ni maeneo ambayo ni ya kuangalia sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mifano ya miradi kama huu mradi wa Uwanja wa Ndege *Terminal II* ulikuwa na matatizo na miradi mingine mingi. Kwa hivyo, eneo hili linahitaji kufanyiwa kazi vya kutosha ili tuone kwamba miradi hii mipya tuliyoianzisha basi haina mashaka katika utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo limezungumzwa sana ni masuala ya uwekezaji na wawekezaji. Miradi inayosimamiwa na *ZIPA*, *master plan* ya Fumba na juu ya umuhimu wa maeneo huru ya uchumi. Suala hili Mhe.

Waziri amelitolea ufafanuzi na alitueleza kwamba tayari *master plan* ya Fumba iko katika kukamilika, kwa hivyo hakuna matatizo.

Eneo hili ni muhimu sana Mhe. Waziri. Masuala ya uwekezaji ni masuala muhimu na kuna haja ya kusimamia kwa karibu sana Mamlaka hii ya *ZIPA*, kwa sababu kuna mambo kidogo hayasimamiwi vizuri. Kuna malalamiko mengi juu ya wawekezaji hasa katika maeneo haya ya *ZIPA*. Kwa hivyo, eneo hili linahitaji kuangaliwa kwa makini, na kwa sababu ni eneo ambalo linaweza likakuza sana uchumi wetu katika maeneo haya ya uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kuhusu fedha za mbegu za mpunga zilizokopwa kwa wakulima. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili alilitolea ufafanuzi hapa na akasema kwamba wiki ijayo wanategemea kuanza kulipa milioni 55 kati ya milioni 240, kwa sababu wizara inadaiwa milioni 240, lakini wanaanza kulipa milioni 55 kuanzia wiki ijayo. Lakini hii wiki ijayo wiki ijayo hii, kwa sababu nakumbuka wiki iliyopita niliwahi kukutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, nikamuuliza haya pesa za watu umeshalipa, akaniambia sasa hivi ndio tuko kwenye maandalizi wiki hii tunaanza kulipa na leo Mhe. Waziri anasema wiki ijayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema pesa hizi zilipwe, kwa sababu pesa hizi ni za wanyonge, wale wakulima ni wanyonge, wanahangaika mabondeni, halafu tumekwenda tumewakopa tumechukua mbegu zao, sasa mbegu zile wanahitaji wapate fedha ambazo ni kwa ajili ya kuwakimu maisha pamoja na watoto wao. Sasa kama serikali imezizuia fedha zile nadhani watakuwa hawatuelewi. Kwa sababu badala ya sisi kuwasaidia wakulima, halafu sisi ndio tunawakopa.

Kwa kweli jambo hili halipendezi na nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na uhaba wa fedha, lakini jambo hili lichukuliwe kwa umuhimu mkubwa, ili hawa wakulima walipwe fedha zao wasitusemeseme. Midomo midomo, wanalalamika sana na ni haki yao, kwa sababu kulima ni kazi na kila mmoja anajua ugumu wa kilimo.

Lakini nimwambie Mhe. Waziri, sijui kama yupo, upo? Mhe. Waziri wiki ijayo uliahidi kwenda kuzilipa hizi fedha, wiki ijayo maana yake ni kuanzia Jumatatu tarehe 03/01/2014. Mhe. Waziri, ninachokuomba wakati wa ulipaji wa fedha hizi katika wiki hiyo, basi unishirikishe na mimi. Katibu Mkuu anipigie simu na aniambie sasa nakwenda kulipa tushirikiane twende kule kwa wakulima Kibokwa twende tukalipe, ndio nitakapohakikisha kwamba fedha hizi zimelipwa. Kuanzia tarehe 03/01/2014 Jumatatu unishirikishe na mimi Mwenyekiti wa Kamati ili tufuatane na watendaji twende kule tunapodai, hapo ndio nitahakikisha kwamba pesa hizi zimelipwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la matayarisho ya kilimo cha mpunga ikiwa ni pamoja na pembejeo za kilimo kutolewa mapema. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, ametoa ufafanuzi juu ya eneo hili, lakini bado hapa pana matatizo. Suala la pembejeo na mbolea halina matatizo makubwa, lakini suala la matayarisho ya maeneo ya kilimo ni tatizo, kwa sababu kwanza wao wanavyodai kwamba Wizara ya Fedha inachelewa kuwaingizia fedha, pamoja na kwamba msimu wa kilimo unafahamika. Kwa sababu ni lazima tukiri kwamba kilimo kinakwenda kwa misimu, sasa kama fedha zitachelewa kuingizwa katika maeneo haya, basi kwa vyovyote vile matayarisho ya kilimo cha mpunga yatachelewa, na kwa sababu msimu unakuwa hautusubiri.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha nikuombe sana kwamba wakati wa matayarisho ya kilimo cha mpunga. Wizara ya Kilimo na Maliasili ipewe umuhimu wa kupewa hizi fedha ili waanze matayarisho mapema. Matayarisho mapema ni pamoja na kuwapa fedha kwa ajili ya kuyafanyia matengenezo matrekta, kwa sababu matrekta yale kabla ya kwenda mabondeni ni lazima yafanyiwe *service*. Matrekta yote yanakusanywa yanapelekwa pale matrekta yanafanyiwa *service* mapema tayari kwa ajili ya kwenda mabondeni. Matayarisho yake hayaji wakati ule ule wa kilimo, matayarisho yake yanatayarishwa mapema kwa kufanyiwa *service* na kila kitu, halafu pale msimu unapoanza sasa ndio yanaanza kwenda mabondeni.

Kwa hivyo, fedha kwa ajili ya matayarisho ya kilimo cha mpunga yanahitajika mapema, vyenginevyo kila wakati tutakuwa tunachelewa na msimu hautusubiri, na tukichelewa kutayarisha kilimo chetu mapema maana yake tutakosa yale manufaa ya kilimo, kwa sababu mpunga utachelewa.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo halikutajwa ni umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji maji na serikali kutoa kipaumbele kwa taasisi ya utafiti. Kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walizungumzia jambo hili. Suala hili Mhe. Waziri amelitolea ufafanuzi wa kilimo cha umwagiliaji maji, ambapo tayari kuna miradi mbali mbali ya *KOICA* ambayo itashughulikia suala hili la umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, fedha kwa ajili ya utafiti. Taasisi ya utafiti bado hatujaipa kipaumbele na kilimo bila ya utafiti basi hakuna kilimo. Mpaka juzi kamati yangu inakwenda katika taasisi hii, kati ya fedha walizopangiwa kama milioni 140 hivi, basi hawajaingiziwa hata senti moja miezi sita, kwa ajili ya kufanyia utafiti na mambo mengine. Kwa kweli ni matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ni kuhusu Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe nalo limezungumziwa sana juu ya utekelezaji na malengo ya kuanzishwa kwa Idara hii. Waheshimiwa Wajumbe wamesema kwamba

tumepitisha sheria, lakini bado inaonekana hakuna utekelezaji wowote, sheria ipo na idara ipo. Kubwa sisi tulikuwa tunahitaji tuanze, idara ipo, lakini tuanze angalau ghala moja la akiba ya chakula na ndio lengo hasa la kuanzisha idara hii.

Katika bajeti hii kumepangwa pale kufanyiwa matengenezo ghala moja kwa ajili ya kuanza kuweka akiba ya chakula, lakini kinachoonekana hadi sasa bado hawajaingiziwa hata shilingi ili kuanza kufanya ukarabati. Kwa hivyo, tuiombe sana Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba watu hawa wanapatiwa hizi fedha ili angalau waanze kufanya ukarabati ghala moja.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mjumbe hapa alisema kama kutatokea majanga yoyote hapa Zanzibar basi hali itakuwa ni ngumu Mwenyezi Mungu atuepushe, lakini hatuna akiba hata kidogo. Wenzetu Bara kidogo wameshaanza kuweka akiba, lakini sisi Zanzibar hatuna akiba yoyote, hatuwezi ku-*survive* hata kwa mieizi miwili. Kwa hivyo, hili ni jambo la hatari, bado Mwenyezi Mungu anatupenda, lakini tujihadhari kabla ya athari haijatokezea.

Siku tuliyokwenda China Mhe. Waziri unakumbuka kwamba Wachina pamoja na kwamba ni nchi inayoendelea, wana akiba ya chakula cha miaka 100 sio mchezo, asilime Mchina hata mmoja asishike jembe miaka 100 watakula wanatwambia, wana chakula cha akiba cha miaka 100 na tuangalie *population* yao ilivyo, miaka 100 asilime mtu hata mmoja basi watakula China. Sasa sisi *population* yetu tuliyokuwanayo ndio hii lakini hata gunia moja la kuweka akiba hatuna. Kwa hivyo, tujitahidini katika eneo hili ili tuone angalau tunapata eneo kwa ajili ya kuweka hifadhi ya chakula, na litakapotokezea janga basi angalau tuweze kuwa na akiba.

Eneo jengine ni suala la miaka mia…

Aaa! miaka 10 samahani sio miaka 100, akiba ya miaka 10, nimeongeza ziro moja mbele. Mhe. Mwenyekiti, wana chakula cha akiba cha miaka 10. Alishtuka eeh!

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Sukari Mhe. Waziri amelitolea ufafanuzi, lakini jambo hili limeshazungumzwa sana tokea awamu ile ya sita juu ya nyumba hizi za kiwanda ambazo wenzetu wawekezaji wale wa kiwanda wamekuwa wakilalamika. Kwa hivyo, nadhani sasa wakati umefika serikali ichukue hatua juu ya jambo hili, haipendezi kila mwaka tunazungumzia jambo hilo kwa hilo. Hatua zichukuliwe wale wanakaa katika zile nyumba hawahusiki, walipewa kwa muda wakati ule walikuwa wanadai fedha zao wanakidai kiwanda, lakini sasa fedha wameshalipwa kila kitu.

Kwa hivyo, nyumba zile zichukuliwe wapewe muda wahame ili wakabidhiwe wenyewe watu wa kiwanda na hata mkataba wao unasema hivyo, mkataba wao umejumuisha pamoja na hizi nyumba. Sasa inakuwa haipendezi, kila wakati tunapokwenda tunapokea malalamiko tunahitaji nyumba, kwa sababu wanalazimika kukodi nyumba nyengine wakati nyumba za kiwanda zipo. Suala hili Mhe. Waziri nadhani linahitaji kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo limezungumziwa ni kuhusu Wakuu wa Idara, wale wanaowasaidia Maafisa Wadhamini Kisiwani Pemba. Waziri anayehusika na Utumishi hayupo, lakini nadhani kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha hawa wana umuhimu wa kuangaliwa sana, kwa sababu pale kuna Afisa Mdhamini ambaye ana Wakuu wa Idara ambao wanamsaidia shughuli zake. Jiografia ya Pemba kama tunavyoiona, Afisa Mdhamini peke yake pale hawezi akafanya kitu.

Katika kila idara kuna Mkuu wa Idara, umwagiliaji maji, misitu na kila sekta, lakini cha kusikitisha ni kwamba wakuu wa idara ni vyeo tu, hakuna hata ile posho wanayopewa ya kuonesha kwamba mimi ni Mkuu wa Idara, ambayo inakuwa na tofauti na wale anaowaongoza, wanapata mishahara yao ile ile. Kwa bahati akitokea mtu ambaye ana elimu kidogo katika wale anaowaongoza basi anampita hata mshahara.

Kwa hivyo, watu hawa nao wanahitaji kuangaliwa, malalamiko yao ni sahihi na wako sawa. Ni lazima wapate posho inayolingana na wadhifa wao wanaoufanyia kazi, sio vyema tukawa tunawatumia na huku tukitegemea kwamba watafanya kazi vizuri. Kwa hivyo, wadhifa tunaowapa kama ni Wakuu wa Idara wa kumsaidia Afisa Mdhamini basi na posho yao iwepo, tena sio posho ya mchezo iwe inalingana na wadhifa ambao wanapewa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu kuongeza mtaji wa *PBZ*. Mhe. Waziri suala hili amelitolea ufafanuzi, na hoja ni kwamba benki hizi sasa hivi zinakwenda na wakati, teknolojia inakuwa na tuko kwenye mashindano makubwa. Lakini serikali haijaongeza mtaji pamoja na kwamba wanao mtaji, lakini unahitaji kuongezeka, kwa sababu ukitaka kupata pesa ni lazima utumie pesa.

Hawa wanachoomba zaidi sio lazima kwamba serikali iongeze pale pesa, wanachoomba ni kwamba zile kodi ambazo wanapeleka serikalini, wana kodi wanapeleka unajua Mhe. Waziri wa Fedha wanazolipa, basi angalau kodi zile zikisamehewa tu kama kwa miaka mitatu hivi, badala ya kuzipeleka serikalini wakaongeza ikawa kama ndio mtaji wake serikali basi pia zitawasaidia. Kwa hivyo, serikali badala ya kuchukua zile kodi, serikali iseme basi kwa miaka mitatu tunawaachia hizi kodi, basi zitawasaidia.

Mhe. Waziri hapa utakumbuka kwamba ulipokuwa ukijibu swali kuhusu Benki ya *CRDB* kupewa kazi pale, ulisema kwamba *PBZ* hawana *Visa card* wala *Master Card*, hii inatokana na kwamba uwezo wao sasa umekuwa mdogo. Kwa hivyo, tunahitaji tuwawezeshe ili sasa na wao vitu kama hivi waweze kuwa navyo, waweze kutoa huduma za *Visa Card* na *Master Card*. Haya wanayakosa kutokana na uwezo wao mdogo.

Kwa hivyo, wao wanachohitaji ni kwamba angalau zile fedha ambazo zinalipwa serikalini, yaani zile kodi wanazolipa serikalini basi tuwaachie tunaweza kuwapa muda kama miaka miwili wanakusanya na huku wenyewe mnaweka kumbukumbu. Kwa hivyo, utakuwa ni mtaji wa serikali kuiongezea *PBZ*, badala ya kuwa sasa kila wakati wanalipa serikalini, pamoja na kwamba nako tunazihitaji, lakini tukiiwezesha hii *PBZ* inaweza ikafanya kazi vizuri zaidi na baada ya hiyo miaka mitatu tunayoizungumza, basi tutakuja kupata zaidi ya hicho ambacho tunakipokea sasa hivi, kwa sababu watazalisha zaidi, watatoa mikopo zaidi.

Sasa hivi hata wale wanaohitaji mikopo mikubwa wanashindwa kuwakopesha kutokana na mtaji waliokuwa nao. Kwa hivyo, tuwawezeshe ili waweze kufanya shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo mafua yamenishika.

La mwisho ni kuhusu suala la Uwanja wa Ndege, ambapo Mhe. Waziri alilielezea vizuri na akayaeleza matatizo yake. Mimi ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hawa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wana matatizo, ni lazima tukiri kwamba pale pana matatizo. Kwa sababu kuna wakati fulani kamati yangu ilikwenda kwa ajili ya kupata kijieneo, ili *PBZ* wafungue kijitawi kidogo cha kupokelea zile pesa za *Visa*, baada ya kuona zile pesa zinapokewa *cash* mikononi, tukasema basi angalau *PBZ* waweze kufungua kijitawi pale na wale wageni wawe wanalipa pesa pale za *Visa*. Juu ya hivyo wakafanya ukaidi, wakasema sijui hatuna nafasi, wakatoa hoja nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, leo tayari barua zimeshakwenda kwa ajili ya kupatiwa nafasi pale, lakini mpaka leo hawajajibu. Hili ni suala muhimu sana ambalo tulikuwa tukililalamikia kwa muda mrefu, kwamba fedha zinazotolewa kwa ajili ya *Visa* zinavuja, lakini wenzetu wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege inaonekana hawataki kutusaidia. Mhe. Waziri kasema hapa kwamba yeye kama Waziri wa Fedha hawezi akaingilia Mamlaka, lakini sisi kama Baraza la Wawakilishi tunayo mamlaka, kwa sababu sisi ndio tunayoisimamia serikali na kazi ya kusimamia ndio hiyo.

Sehemu hii tuliiona kuwa ina matatizo na tulikushauri na umeshakubali, umeshaandaa miundombinu ili kuona kwamba pesa zile sasa zinakusanywa kwa utaratibu huu. Lakini kama mamlaka haitaki kutoa mashirikiano katika hili sisi hatuwezi tukaliachia tu hili. Kwa sababu hizi ni fedha za umma, hii mamlaka sio ya mtu. Kama kuna mtu anajifikiria kwamba ile mamlaka ni mali yake anajidanganya si kweli. Na pamekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu uwanja wa ndege, aliwahi hata kuzuia huyu kutaka kukosesha pesa wakati *precision air* ilipokuwa ikidaiwa fedha na akaruhusu kwamba ndege iendelee kuruka.

Kwa hivyo, kuna *record* nyingi ambazo si nzuri katika mamlaka hii. Nadhani kuna baadhi ya viongozi wanajihisi kwamba ile mamlaka ni yao, lakini ile ni mamlaka ya umma na inahitaji kutoa mashirikiano ya pamoja ili kuona serikali nayo inafanya shughuli zake pale.

Mwaka jana Mhe. Spika, alipitisha bajeti ya Mhe. Waziri wa Miundombinu aliipitisha hapa, lakini tunamuomba sana bajeti ijayo Mwenyezi Mungu akitujaalia kama tutafika Mhe. Spika, atuachie. Kwa sababu pale napo sisi ndipo penye mamlaka yetu atuachie kabisa Mhe. Spika, na hizi salamu Mwenyekiti mpelekee, atuachie Wizara ya Miundombinu kwa sababu tunataka kufanya dawa na Mhe. Rais atufahamu sana katika hili.

Lengo letu ni kuona kwamba shughuli zetu hizi zinakwenda. Sio mtu mmoja ana malalamiko chungunzima kila pahala analalamikiwa halafu sisi tukae tu hapa. Kwa hivyo Mwenyekiti tumuombe sana Mhe. Waziri ushirikiane na Waziri wa Mawasiliano, hayupo, tuhakikishe kwamba kabla ya bajeti hiyo ufumbuizi juu ya jambo hili limeshapatiwa. Tunahitaji kuweka mitambo pale kwa ajili ya kukusanya kodi za wananchi na fedha hizi ndizo hizo tunazozilalamikia. Tukizungumzia fedha haziingizwi. Fedha sijui hazipatiwi *ten percent* ndio hizi. Hizi ndizo fedha za kufanyia kazi. Sasa kama kuna mtu anajijali yeye tu nafsi yake, hajali wenzake anakwamisha kwa makusudi, hili hatuwezi kumvumilia.

Mhe. Waziri amesema hapa ikiwa mtambo ule utafungwa, basi uwezekano wa kuongezeka mapato zaidi inawezekana kabisa jambo hilo.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru tena Mhe. Waziri, na niwashukuru waheshimiwa wajumbe na ripoti hizi. Mhe. Mwenyekiti, ni dira ambayo waheshimiwa mawaziri wanatakiwa waifanyie kazi. Kwa sababu zitasaidia katika kuleta ufanisi katika shughuli zetu. Ripoti hizi sio maana yake zikae tu zisifanyiwe kazi. Ripoti hizi zitakapofanyiwa kazi basi hata yale malalamiko ya waheshimiwa yatapungua katika baadhi ya maeneo. Inakuwa haipendezi kwamba kila mwaka ripoti zinakuja, zinazungumzia jambo hilo

kwa hilo lakini ufumbuzi wake haupatikani. Mimi ninaamini kama ripoti hizi za kamati zitafanyiwa kazi ipasavyo, basi tutakuwa hatuna matatizo makubwa katika maeneo yale.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti niwashukuru na naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla ya kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe kwanza ningeomba wale wajumbe ambao wako nje warudi ndani sasa kwa ajili ya kupitisha hii ripoti. Lakini baada ya hapo ningependa kuchukua fursa hii kutoa ufafanuzi juu ya hoja ambayo Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alikuwa ameulizia.

Waheshimiwa Wajumbe, chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi kinaongozwa kwa mujibu wa sheria na kanuni ambazo tumejiwekea. Mhe. Mjumbe ambae alikuja kuleta hoja yake hapa aliomba iundwe kamati maalum. Kwa mujibu wa Kanuni yetu hii ambayo imetolewa, toleo la mwaka 2007, toleo mwaka 2012 baada ya marekebisho hakuna kipengele kinachozungumzia suala la kamati maalum.

Kwa msingi huo basi kutokana na hoja ya Mhe. Mjumbe aliyokuwa amewasilisha hapa juu ya kwamba wao kama Kamati ya Fedha na Uchumi walikwenda kufanya kazi ile, lakini maoni yake ya ziada yalikuwa juu ya kuzidishiwa muda ili kazi ile iweze kufanyika kwa ufanisi zaidi, kitu ambacho kilikosekana kwa wakati ule.

Kwa muongozo wa kiti hiki naonelea ni vyema basi kazi hii ambayo wenzetu walikuwa wameianza tuwarejeshee wao Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ili wakaendeleze kazi hii, kwa kuongezewa muda maalum na kazi maalum na kwa maeneo maalum na hadidu rejea ambazo zitahusiana na utaratibu wa kukamilisha kazi hiyo zitawasilishwa na Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe mkubaliane na maelekezo haya ambayo nimeyatoa, ili tuweze kupitisha ripoti hii na baadae tuendelee na taratibu nyengine ambazo tumejiwekea.

Sasa niwahoji wanaokubaliana na ripoti hii pamoja na maelekezo ambayo nimeyatoa wanyooshe mikono yao. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2012/2013

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako naomba kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufuatia na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Mifugo, Utalii na Habari ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Julai, 2012 hadi Juni, 2013.

Mhe. Mwenyekiti, natoa shukurani za dhati kwako wewe binafsi na kwa Kamati ya Mifugo, Utalii na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wake na watendaji wa Wizara katika kusaidia utendaji bora kwa ajili ya kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi.

Mhe, Mwenyekiti, ninashukuru pia kamati kwa kutoa maagizo yaliyolenga kuifanya Wizara itekeleze majukumu yake yote kwa ufanisi. Ninathibitisha kwamba Wizara imeyatekeleza maagizo yote ya kamati. Mhe. Mwenyekiti, naomba nisome ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa wizara yangu kuanzia mwezi wa Julai, 2012 hadi Juni 2013.

Agizo la kwanza, wizara iendelee kukumbushia kwa Wizara ya Ardhi Makaazi Maji na Nishati kuhusu maeneo yake yaliyoombewa hakimiliki ikiwemo eneo la karantini la Nziwengi Pemba, ambalo limeshapimwa na kuombewa hatimiliki na pesa zimeshalipwa kwa wizara husika. Katika hatua ya utekelezaji Wizara inafuatilia upatikanaji wa hatimiliki Ofisi ya Ardhi na Upimaji Pemba. Ofisi hiyo imeshapitisha taratibu zote za kupatikana hatimiliki ya Nziwengi. Tumeelezwa kwamba karibuni kutakabidhiwa hatimiliki kwa Taasisi za Serikali ikiwemo na Nziwengi. Wizara imekwishapata hatimiliki ya Dunga, hatimiliki A.I Mtoni na Kisakasaka bado hazijapatikana lakini zimeshalipiwa, upimaji na maombi yameshawasilishwa.

Agizo la pili, Mhe. Mwenyekiti, wizara ifuatilie kwa makini hati zinazohusu eneo lake la Mtoni kuweka mikakati itakayozuia uvamizi zaidi katika eneo hilo. Katika hatua ya utekelezaji, Wizara imekwishapima mashamba yake yote kwa kupitia bajeti ya mwaka 2013/2014 imeomba fedha za kutengenezea nyaraka muhimu za kupatiwa hatimiliki likiwemo na eneo la upatikanaji upandishaji ng'ombe kwa sindano liliopo Mtoni. Eneo la A.I Mtoni limekwisha jengewa uzio wa matofali.

Mhe. Mwenyekiti agizo la tatu, wizara ifanye uhakiki kuyatambua maeneo yake yote ili kuepukana na hatari ya uvamizi ya kupotea kwa maeneo ya

wizara. Katika hatua ya utekelezaji, kazi hii imekwisha kutekelezwa na wasimamizi wa maeneo yote wametakiwa kuyalinda maeneo ya serikali, maeneo yamekwishapimwa na mipaka yake inajulikana.

Agizo la nne, Mhe. Mwenyekiti, elimu ya kutosha kuhusu sheria ya utumishi wa umma inapaswa kutolewa kwa wafanyakazi ili kuifahamu vyema sheria hiyo. Katika hatua ya utekelezaji, kazi hii imeshaanza na inaendelea na jumla ya wafanyakazi mia wameshapatiwa semina kuhusu sheria hiyo. Kwa wafanyakazi wapya watapatiwa elimu ya sheria hiyo huko Tunguu katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Wizara imepanga kuwapatia mafunzo ya sheria ya umma ya utumishi wafanyakazi wake wapya.

Agizo la tano, Wizara itilie umuhimu suala la kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo tafiti za kugundua iwapo gesi nyengine zinazotoka wakati wa kutengenezwa *bio gas* zina madhara yoyote kwa binaadamu na mifugo. Katika hatua ya utekelezaji wizara inatilia umuhimu kufanyika tafiti mbali mbali ili kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi.

Katika mwaka 2012/2013 wizara imefanya utafiti shirikishi wa ufugaji kuku wa uzalishaji, wenye lengo la kuongeza uzalishaji, ukuaji, ustahmilivu wa maradhi na ulezi. Kuku wa aina 3 za makabila ya kigeni yaani *Australop, Rhod Island Red na White legon* na kuku wa kienyeji aina ya kishingo wameshachunguzwa. Utafiti huu bado unaendelea na matokeo ya mwanzo yanaonesha kuku chotara waliotokana na utafiti huu wana uwezo wa kutaga wastani wa mayai 180 kwa mwaka badala ya wastani wa mayai 65 kwa mwaka na kuku wetu wa asili.

Jumla ya majogoo bora 180 yameshasambazwa kwa wafugaji Unguja na Pemba. Jumla ya kuku majike 1,080 na majogoo ya kisasa 120 yamesambazwa kwa wafugaji katika shehia za Mbuyutende, Bandamaji, Kikobweni, Kibeni, Mjimbini na Ukutini. Ikiwa ni awamu ya mwanzo katika kueneza kuku kwa lengo la kupata kuku chotara wenye uzalishaji mzuri ikiwa ni mpango wa kuwasaidia wananchi kujitoa katika hali ya umaskini.

Katika uzalishaji wa *bio gas* wizara haijaona aina ya *gas* yoyote inayozalisha ambayo inaweza kuathiri wanaadamu au mifugo yao. Wizara imeanza kushirikiana na Taasisi za Kimataifa ili tufanye tafiti kwa pamoja na kuanzishwa kwa vituo vipya vya utafiti hapa Zanzibar. Makubaliano ya kuendeleza shughuli za utafiti hivi karibuni tumetegemea kuwasili kwa ujumbe kutoka *State Oceanic Administration* (*SOA*) ya Uchina kwa kupanga mipango na kuendeleza ushirikiano katika sekta ya uvuvi.
Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein, alipotembelea Uchina aliweka saini ya ushirikiano huo.

Aidha wizara inashirikiana na Taasisi ya *IMS* na kufanya utafiti mbali mbali hasa zinazohusiana na zao la mwani. Wizara kwa kushirikiana na Korea ya Kusini imefanya utafiti wa maeneo ya ufugaji samaki.

Agizo la sita, Mhe. Mwenyekiti wizara ihakikishe kwamba inatumia vizuri fursa za kushiriki katika mikutano mbali mbali ikiwemo mikutano ya kikanda. Katika hatua ya utekelezaji Mhe. Mwenyekiti, wizara imeshiriki katika mikutano mbali mbali ikiwemo *European Union* huko Dar-es-Salaam, ambako kumepelekea kupatikana kwa mradi wa *Smartfish* na *Small Island Project*. Pia, tumeshiriki vikao vya *World* Bank na kupatikana mradi wa *South West Indian Ocean Fisheries* (*Swiofish*).

Aidha, tumeshiriki mkutano wa mashirikiano huko Dar-es-Salaam na kufanikisha mashirikiano ya pamoja kwa kuendeleza shughuli za mazao ya baharini. Tunashiriki, vile vile, katika vikao vya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki vinavyohusu kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Hata hivyo, ushiriki wa baadhi ya mikutano hushindikana kutokana na uhaba wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti agizo la saba, Wizara pamoja na kuwasaidia wafugaji kitaalumu, akiwemo mfugaji wa ng'ombe wa maziwa wa Machui. Iangalie uwezekano na kuwasaidia kifedha wazalishaji ili iwape moyo wa kuendelea kufanya shughuli hizo muhimu za ufugaji. Katika hatua ya utekelezaji, wizara inaendelea kuwasaidia wafugaji kwa hali na mali na kuwapatia taaluma katika nyanja mbali mbali za uzalishaji.

Mfugaji wa Machui anapatiwa huduma ya upandishaji wa ng'ombe pale inapohitajika sambamba na kuwapatia mafunzo kwa vitendo kupitia kijana aliyemteua na mfanyakazi mwenyewe. Mfugaji mwenyewe wa kuku wa Kandwi amepatiwa pikipiki kwa kurahisisha shughuli zake. Wavuvi wamekwisha patiwa misaada mikubwa hasa kupitia mradi wa *MACEMP* na kasma ya Mhe. Waziri.

Agizo la nane, wizara ifanye juhudi maalum za kuwaendeleza wafugaji waliopiga hatua kwa kuwapatia ziara za kimafunzo nje ya nchi ili wapate fursa ya kujifunza zaidi kwa wenzao kwa ajili ya kuleta mafanikio zaidi kwa pamoja na wafugaji wengine hapa nchini. Hatua ya utekelezaji wa kipindi cha mwaka 2012/2013, Idara haikupanga kupeleka wafugaji nje ya nchi kwa ajili ya ziara ya kimasomo.

Hata hivyo, kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hivi sasa Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma, vijana 40 kutoka shehia ya Kikobweni na Kibeni Wilaya ya Kaskazini 'A', walipatiwa fursa ya kufanya ziara ya kimasomo ndani ya nchi kwa kuwatembelea wafugaji

wenzao. Miongoni mwao ni Bwana Ame Khamis Ame wa Kandwi na Bwana Muadhin Suleiman wa Uroa.

Aidha, katika mwaka 2013/2014 wafugaji 10 kutoka Pemba watakuja Unguja na wafugaji wa Unguja watakwenda Pemba kwa ajili ya ziara za kimasomo. Aidha, wazalishaji wa mazao ya baharini 18 wamepatiwa fursa ya kwenda China kujifunza mbinu bora za uzalishajiu.

Agizo la tisa, Mhe. Mwenyekiti utaratibu mzuri zaidi unapaswa kuandaliwa na Wizara utasaidia uangizaji na upatikanaji wa chanjo za mifugo zenye ubora na zinazokidhi viwango vinavyokubalika kitaalam, ili kuwaepusha wafugaji kutumia chanjo zilizo chini ya kiwango ambazo huleta madhara kwa mifugo yao.

Katika hatua ya utekelezaji Wizara itashirikiana na waagizaji wa chanjo za mifugo na kusisitiza waagize chanjo zitakazoweza kudumu kwa muda mrefu, bila ya kuharibika na ambazo zina uwezo wa kulinda mifugo yetu kutokana na maradhi yanayosabishwa na aina ya vimelea vya maradhi vilivyokuwepo nchini. Chanjo zinachunguzwa mashambani na kuthibitishwa ubora wao. Aidha, maofisa waliopo vijijini wanapatiwa ushauri, nao wanawaelekeza wazalishaji njia bora za kuzitumia chanjo hizo.

Agizo la mwisho la kumi, Wizara kushirikiana na Wizara zinazohusika isaidie katika upatikanaji huduma ya maji na barabara katika eneo la kituo cha huduma za mifugo (*ZAASO*) Kianga. Katika hatua ya utekelezaji Wizara inashirikiana na kutoa misaada kwa Taasisi ya *ZAASO* na Taasisi hiyo inawatumia wafanyakazi wa wizara katika kutekeleza kazi zake. Eneo hilo hivi saa limekwishapata visima viwili vya maji pamoja na *pump* zake.

Mhe. Mwenyekiti, maagizo ya Kamati yalitokana na ripoti ya kamati ya mwaka 2012/2013 maalum kwa Kisiwa cha Pemba. Agizo la kwanza, kutokana na hali mbaya ya nyumba ya Wizara iliyopo Mkoroshoni, kamati inashauri kwamba nyumba hiyo ivunjwe matofali na mabati ya nyumba hiyo yahifadhiwe na baadae Wizara itafute fedha kwa ajili ya ujenzi mpya wa nyumba katika eneo hilo.

Katika hatua za utekelezaji, agizo hili limeshatekelezwa. Nyumba hiyo imevunjwa kwa uangalifu na zana zote zimehifadhiwa kwa matumizi ya hapo baadae, Wizara itakapoingiziwa fedha za ujenzi wa nyumba hiyo.

Agizo la pili, wananchi wanaoishi karibu na skuli ya wafugaji Ole washirikishwe katika suala la ulinzi na usimamizi wa kituo hicho. Hatua ya utekelezaji uongozi wa Idara ulikutana na Sheha wa Ole, pamoja na majirani

wanaoishi karibu na kituo hicho na kuwaomba mashirikiano katika suala la ulinzi wa kituo.

Agizo la tatu, inashauri wizara kuzizungushia uzio eneo la jengo jipya la wizara Pemba, pamoja na kupanda bustani ili kuleta haiba nzuri katika eneo hilo. Hatua ya utekelezaji agizo hili limetekelezwa na fedha imeombwa katika bajeti ya mwaka huu. Aidha, bustani imeanzishwa kwa kupanda miti ya kivuli kuzunguka jengo la wizara.

Agizo la nne, wizara iharakishe kukamilisha ujenzi wa nyumba mpya ya kulala wageni iliyopo katika eneo la jengo jipya la Wizara Wete, ili ianze kuingiza fedha katika serikali kutokana na wageni watakaokaa katika nyumba hiyo.

Hatua ya utekelezaji agizo limetekelezwa kwa kuomba fedha katika bajeti ya mwaka huu, aidha baadhi ya vifaa vimeshanunuliwa ikiwemo vitanda, meza za kulia, *dressing table*, majokofu na mapazia.

Agizo la tano, Wizara ihakikishe kuwa wanakijiji wa eneo litakalojengwa kiwanda cha kusagia mwani huko Tumbe wanafaidika kutokana na kujengwa kwa kiwanda hicho hapo baadae. Utekelezaji agizo limepokelewa na litafanyiwa kazi ujenzi wa kiwanda utakapokamilika.

Agizo la sita, Wizara iandae utaratibu wa kuifanyia ukarabati nyumba ya kituo cha wafugaji Ole, utekelezaji Wizara imelipokea agizo hili na inalifanyia kazi. Fedha za ukarabati wa kituo hicho imeombwa kupitia mradi wa *MIVAP*.

Agizo la saba, kutokana na wananchi kutokuwa na mwamko wa kupeleka mifugo yao kuchanjwa hususan mbwa, kuna haja kubwa kwa wizara kuelimisha juu ya umuhimu wa masuala mbali mbali yakiwemo chanjo za mifugo pamoja na mbinu bora za ufugaji na uvuvi. Utekelezaji mafunzo mbali mbali yamekwisha tolewa kwa wananchi 7,137 kuhusu kukinga maradhi ya mifugo. Mbinu bora za ufugaji na uvuvi na mbinu za kujikinga na ukimwi.

Agizo la nane, kutokana na kuachwa kwa nyumba ya Wizara ya Mkoroshoni kwa muda mrefu bila ya ulinzi na usimamizi mzuri, kamati imeitaka wizara kuwa makini zaidi juu ya usimamizi na utunzaji wa mali za serikali ili kuepusha upotevu na uharibifu wa mali hizo. Utekelezaji, Wizara imepokea agizo la kamati na kulifanyia kazi katika maelekezo yote yaliyotolewa kuhusu nyumba ya Mkoroshoni ambayo uharibifu ulianza miaka mingi iliyopita. Aidha, Wizara imepanga mikakati kwa kudhibiti vyema miundombinu mengine ikiwa pamoja na nyumba ya Ole na josho la Makangale.

Agizo la tisa, kutokana na kubainika kupandwa miti na wananchi waliovamia la Nziwengi, kamati iliitaka Wizara kushirikiana na Mamlaka husika akiwemo Sheha wa eneo hilo kuhakikisha kuwa miti iliyopandwa katika eneo hilo inan'golewa kwa vile eneo hilo limetengwa na limeshapimwa na serikali kwa ajili ya kukarantini mifugo.

Utekelezaji, ni kweli baadhi ya wananchi walikwishaanza kupanda miti katika eneo la karantini ya Nziwengi. Wizara imeshirikiana na Sheha wa Shehia ambayo amechukua hatua ya kung'oa miche hiyo na hivi sasa eneo halijavamiwa kwa aina yoyote.

Agizo la mwisho kabisa, kamati imeitaka Wizara iwe karibu zaidi na kamati kwa kushirikiana na baadhi ya wajumbe wa kamati katika shughuli zake mbali mbali muhimu, ili wajumbe hao wapate nafasi ya kufahamu mambo muhimu ya Wizara na inapohitajika waweze kutoa ushauri katika kuendeleza shughuli za Wizara kwa maslahi ya taifa.

Utekelezaji, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina ushirikiano mkubwa na wajumbe wa Kamati. Pia, Wizara itaendelea kuwatumia wajumbe wa kamati katika shughuli zake mbali mbali muhimu, ili waweze kutoa ushauri mzuri.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wako wa ripoti. Waheshimiwa wajumbe muda tulio nao ni dakika 20. Mhe. Waziri wa Uvuvi na Mifugo ana maagizo 28 na ili atimize anahitaji dakika zaidi 40. Kwa msingi huo basi ninahisi ni vyema tukasitisha shughuli zetu hapa tulipofikia kwa siku ya leo ili kesho asubuhi tuweze kuja kuendelea zaidi.Baada ya maelekezo hayo, sasa naomba kuahiriksha Baraza hili hadi kesho tarehe 31/01/2014 siku ya Ijumaa saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 1.23 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 31/01/2014 saa 3.00 asubuhi)